KUCHUNGUZA UHALISIAJABU NA DHAMIRA KATIKA RIWAYA ZA KUSADIKIKA NA ADILI NA NDUGUZE

ZUHURA ALI ABDALLA

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI) CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2019

UTHIBITISHO

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa, ameisoma tasnifu hii yenye mada: ***Kuchunguza Uhalisiajabu na Dhamira katika riwaya za Kusadikika na Adili na Nduguze***na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kupatiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Kiswahili Fasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....

Profesa Emmanuel Mbogo

(Msimamizi)

.....

Tarehe

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama kazi nzima au sehemu ya tasnifu hii bila kibali cha maandishi kutoka kwa mtafiti aukwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

IKIRARI

Mimi, **Zuhura Ali Abdallah,** nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu binafsi, na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au shahada nyingine yoyote.

.....

Saini

.....

Tarehe

TABARUKU

Kwa heshima na taadhima, naitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu wapenzi mama yangu Mwamize Abeid Juma na baba yangu Ali Abdallah Juma kwa kunizaa, kunilea na kunisomesha bila ya kuchoka. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu (S.W) awasamehe makosa yao na awajaalie wawe miongoni mwa waja wa Peponi kwa rehema na mapenzi yake (Amiin).

SHUKURANI

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu (S.W) kwa kuniumba kuwa kiumbe binaadamu na kunijaalia uzima, afya, uvumilivu, uwezo, busara na hekima kwa kuifanya kazi hii ya utafiti hadi kukamilika. Kwa ufupi nastahiki kusema: Alhamdulillah Rabbil Alamiin. Namuomba Mwenyezi Mungu (S.W) anijaalie ziada za kheri.

Pili, shukurani zangu za dhati ziwafikie wazazi wangu wapenzi: kwa juhudi zao za kunizaa, kunilea na kunisomesha bila ya kuchoka hadi nikafikia katika ngazi hii ya elimu. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awasamehe makosa yao na awajaalie wawe miongoni mwa waja wa peponi kwa rehema na mapenzi yake (Amiin).

Tatu, Shukrani za pekee zimfikie Msimamizi wangu Profesa Emmanuel Mbogo, ambaye amenikuza kitaaluma na kunishauri katika kila hatua hadi tasnifu hii kukamilika. Profesa Emmanuel Mbogo amekuwa akiisimamia na kufanya kazi hii bila ya kuchoka na kunitia hamasa kubwa niweze kumaliza kazi hii kwa wakati muwafaka. Sina budi kumuombea kwa Mola amlipe malipo mema (Amiin).

Shukurani nyingi ziufikie uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kuanzia makao makuu Dar es Salaam hadi tawi la Pemba. Kwa sababu hawa ni wengi naomba niwataje baadhi kwa niaba ya wote. Ninaowataja hapa ni Dkt. Muhamed Omary Maguo, Dkt. Hadija Jilala, Dkt. Zelda Elisifa, Dkt. Hilda Pembe, mwalimu Bakari Kombo Bakari na mwalimu Nassor Ali Suleiman.Pia natoa shukrani zangu kwamwalim Sharif Juma Fakih na wengineo. Walimu wote hawa walinisaidia kwa njia moja ama nyengine hadi kukamilika kwa tasnifu hii.

Mwisho napenda kuishukuru familia yangu. kwa kunishauri, kunitiamoyo, busara, juhudi, hamasa na uvumilivu wao mkubwa katika kipindi chote cha masomo hadi sasa kwa pale walipokuwa hatuko pamoja kwa sababu ya masomo, hakika walitambua kuwa elimu ni ufunguo wa maisha na wala elimu haina mwisho.

.

IKISIRI

Utafiti huu unahusu *Kuchunguza Uhalisiajabu na Dhamira katika riwaya za Kusadikika na Adili na Nduguze.* Lengo kuu ni "Kuchunguza Uhalisiajabu na Dhamira katika *Kusadikika na Adili na Nduguze."* Riwaya hizi ziliandikwa na Shaaban Robert. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu kwa lengo la kwanza na swali la kwanza la utafiti. Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji imetumika kwa lengo la pili na swali la pili la utafiti huu. Mbinu iliyotumika kukusanyia data ilikuwa ni mbinu ya Usomaji Makini mbapo mtafiti alizisoma kwa kina riwaya teule huku akidondoa data ambazo hatimae zilijibu maswali ya utafiti huu. Data za utafiti huu zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa mkabala wa kimaelezo na kitakwimu. Kwa ujumla utafiti huu uliongozwa na malengo mawili na maswali mawili ya utafiti. Lengo la kwanza lilikuwa: Kubainisha vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Lengo hilo limekwenda sambamba na swali la kwanza la utafiti lisemalo: *Ni Vipengele vipi vya Uhalisiajabu vilivyobainishwa katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze?*Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa riwaya teule zimetumia vipengele vya uhalisiajabu kama vile; utatizaji wa wakati, masimulizi ya kihalisiajabu, usawiri wa wahusika wa kihalisiajabu, motifu za safari za kihalisiajabu, mitindo ya uumbuzi na udenguzi, na mandhari ya kihalisiajabu. Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa: Kubainisha dhamira za uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Lengo hilo limewiana na swali la pili la utafiti huu lisemalo: Ni dhamira zipi za uhalisiajabu zilizobainishwa katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze?* Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha dhamira mbalimbali za uhalisiajabu kama ifuatavyo: Umuhimu wa sheria, uongozi mbaya, ukweli, ukombozi, umuhimu wa huduma za kijamii, ulafi, wivu na choyo. Riwaya ya *Adili na Nduguze* imebainisha dhamira za: Usaliti, migongano ya mifumo ya kiuchumi ulimwenguni, ukoloni, ukweli, uongozi bora na utabaka.

YALIYOMO

UTHIBITISHO ii

HAKIMILIKI iii

IKIRARI iv

TABARUKU v

SHUKURANI vi

IKISIRI …. viii

YALIYOMO ix

ORODHA YA MAJADWELI xv

ORODHA YA VIFUPISHO xvi

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Usuli wa Mada 1

1.3 Tatizo la Utafiti 3

1.4 Malengo ya Utafiti 5

1.4.1 Lengo Kuu 5

1.4.2 Malengo Mahsusi 5

1.5 Maswali ya Utafiti 5

1.6 Umuhimu wa Utafiti 6

1.7 Mipaka ya Utafiti 6

1.8 Muundo wa Tasnifu 7

1.9 Hitimisho 8

SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA 10

2.1 Utangulizi 10

2.2 Ufafanuzi wa Dhana Muhimu 10

2.2.1 Dhana ya Uhalisiajabu 10

2.2.1.1 Vipengele vya Uhalisiajabu 14

2.2.1.1.1 Uhalisiajabu na Mtindo na Mbinu za Kisimulizi 14

2.2.1.1.2 Mgotanisho wa Uhalisia na Njozi za Fantasia 15

2.2.1.1.3 Michezo na Utatizaji wa Dhana ya Wakati 15

2.2.1.1.4 Mitindo ya Udenguzi na Uumbuzi 16

2.2.1.1.5 Umahuluti wa Kitamaduni na Kitanzu na Mwingilianomatini 16

2.2.1.1.6 Usawiri wa Wahusika, Utambulisho na Mawanda ya Kihusika 17

2.2.1.1.7 Ishara na Uashiriaji na Suala la Uchimuzi 18

2.2.1.1.8 Uhalisiajabu na Suala la Ontolojia 18

2.2.2 Dhana ya Dhamira 19

2.3 Mapitio ya Kazi tangulizi 21

2.3.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Nadharia ya Uhalisiajabu katika riwaya ya Kiswahili 21

2.3.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Riwaya za Shaaban Robert 24

2.4 Pengo la Utafiti 31

2.5 Mkabala wa Kinadharia 31

2.5.1 Nadharia ya Uhalisiajabu 32

2.5.2 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji 35

2.5.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji 36

2.5.2.2 Mapungufu ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji 39

2.6 Hitimisho..... 40

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI 41

3.1 Utangulizi..... 41

3.2 Umbo la Utafiti 41

3.3 Eneo la Utafiti..... 42

3.4 Walengwa wa Utafiti 42

3.5 Sampuli na Usampulishaji 42

3.6 Ukusanyaji wa Data 43

3.6.1 Data za Msingi 43

3.6.2 Data za Upili 44

3.7 Mbinu za Kukusanya Data..... 44

3.7.1 Mbinu ya Usomaji Makini 44

3.7.2 Mbinu ya Upitiaji wa Nyaraka..... 45

3.8 Uchambuzi wa Data..... 46

3.8.1 Mbinu ya Mkabala wa Kimaelezo 46

3.9 Zana za Kukusanyia Data 46

3.9.1 Shajara..... 46

3.9.2 Kompyuta..... 47

3.9.3 Simu ya Mkononi..... 47

3.10 Hitimisho..... 47

SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI 49

4.1 Utangulizi 49

4.2 Usuli wa Mwandishi, Shaaban Robert 49

4.3 Muhtasari wa Riwaya ya Kusadikika 52

4.4 Muhtasari wa Riwaya ya Adili na Nduguze 55

4.5 Vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze 57

4.5.1 Vipengele vya Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kusadikika 57

4.5.1.1 Utatizaji wa Wakati 58

4.5.1.2 Masimulizi ya Kihalisiajabu 59

4.5.1.3 Usawiri wa Wahusika, Utambulisho na Mwanda wa Kihusika 60

4.5.1.4 Motifu za Safari za Kihalisiajabu 64

4.5.1.5 Mandhari za Kihalisiajabu 65

4.5.2 Vipengele vya Uhalisiajabu katika Riwaya ya Adili na Nduguze 68

4.5.2.1 Mtindo wa Udenguzi na Uumbuzi 68

4.5.2.2 Mtindo wa Kihalisiajabu 70

4.5.2.3 Masimulizi ya Kihalisiajabu 72

4.5.2.4 Usawiri wa Wahusika, Utambulisho na Mwanda wa Kihusika 74

4.5.2.5 Motifu za Safari za Kihalisiajabu 79

4.5.3 Mandhari za Kihalisiajabu 82

4.6 Dhamira za uhalisiajabu katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze 86

4.6.1 Dhamira za Uhalisiajabu katika riwaya ya Kusadikika 87

4.6.1.1 Dhamira ya Ukandamizaji na Unyonyaji 87

4.6.1.2 Dhamira ya Maendeleo na Ukuaji wa Huduma bora za Kijamii 89

4.6.1.3 Dhamira ya Tamaa na Uchoyo 90

4.6.1.4 Dhamira ya Uongozi Mbaya 92

4.6.1.5 Umuhimu wa Elimu ya Uanasheria 94

4.5.1.6 Dhamira ya Ukombozi 97

4.6.1.7 Dhamira ya Ubadhirifu wa Mali ya Umma 100

4.6.2 Dhamira za Uhalisiajabu katika riwaya ya Adili na Nduguze 103

4.6.2.1 Dhamira ya Uongozi bora 103

4.6.2.2 Dhamira ya Uongozi Mbaya. 104

4.6.2.3 Dhamira ya Wivu na Husda 105

4.6.2.4 Dhamira ya Ukoloni 107

4.6.2.5 Dhamira ya Itikadi 108

4.6.2.6 Dhamira ya Utabaka na Usaliti 110

4.6.2.6. 1 Manyani 110

4.7 Hitimisho 113

SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 115

5.1 Utangulizi 115

5.2 Muhtasari 115

5.2.1 Lengo Mahsusi La Kwanza 117

5.2.2 Lengo Mahsusi la Pili 118

5.3 Hitimisho 118

5.4 Mapendekezo 119

5.4.1 Mapendekezo ya Kitaaluma 119

5.4.2 Mapendekezo kwa Serikali 119

MAREJELEO 121

ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli 01: Muhtasari wa Vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya Kusadikika 67

Jadweli 02: Muhtasari wa Vipengele vya Uhalisiajabu katika Adili na Nduguze 85

Jadweli 03: Muhtasari wa jumla wa vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze 86

Jadweli 04: Muhtasari wa Dhamira za Uhalisiajabu katika riwaya ya Kusadikika 102

Jadweli 05: Muhtasari wa Dhamira za Uhalisiajabu katika Adili na Nduguze 112

Jadweli 06: Muhtasari wa jumla wa Dhamira za Uhalisiajabu katika riwaya za Kusadikika na Adili na Nduguze 113

ORODHA YA VIFUPISHO

BAKIZA	Baraza la Kiswahili Zanzibar.
CHAKAMA	Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki
Dkt	Daktari
Khj	Kama hapo juu
M.A	Master of Art.
MUM	Muslim University of Morogoro:
OUT	Open University of Tanzania.
SAW	Swalallahu Alaihi Wasalaam.
SUZA	State University of Zanzibar.
S.W	Subhana Wataala.
TATAKI	Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
TUKI	Taasisi ya Ukuzaji Kiswahili.
UK	Ukurasa

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Sura hii ni sura tangulizi iliyobainisha na kuelezea kwa kina vipengele vya kiutangulizi ambavyo niUsuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na umuhimu wa utafiti. Vilevile, sura hii imefafanua mpango wa tasnifu na kumalizia na Hitimisho.

1.2 Usuli wa Mada

Wamitila (2013), anaeleza kuwa uhalisiajabu ni dhana tata kutokana na oksimora iliyopo kwenye jina la dhana yenyewe - uhalisia na maajabu au mazingaombwe. Uhalisia ambao unahusu kuwasilisha na kuakisi uhalisi kama ulivyo ulimwenguni, unaegemezwa kwenye nadharia ya mwigo au uhalisia wa maisha halisi.

Kanuni kuu katika uhalisia ni ile ya ushabihi kweli. Mazingaombwe au maajabu kwa upande wake hukiuka mipaka ya uhalisi kwa kuhusisha hali, matendo, mielekeo au matukio yanayovuka mipaka ya “ukawaida” wa uhalisi. Maajabu au mazingaombwe ni dhana inayoweza kutumiwa kueleza chochote kinachokiuka ujarabati zikiwemo imani za kidini, ushirikina, migani, visasili na kadhalika (Hart na Ouyang, 2015).

Wamitila (khj), anafafanua kuwa ugumu mwingine wa kuieleza dhana ya uhalisiajabu ni kutokana na sifa ambazo zinahusishwa na mikondo au matapo mengine ya fasihi kama uhalisiafifi, ulimbwende, usasa na usasaleo/usasabaadaye nakadhalika. Wamitila (ktj), anataja kazi ambazo ni za kiuhalisiafifi lakini zina sifa zinazohusishwa na uhalisiajabu. Zamora na Faris (1995) katika Wamitila (2013),

wanaeleza kwambakatika matini za kihalisiajabu matukio yasiyokuwa ya kawaida si jambo rahisi na dhahiri bali ni tukio la kila siku linalotokea, kukubalika, na kuwa sehemu ya urazini na matukio ya uhalisia wa kifasihi. Maajabu au mazingaombwe si matukio ya kiwazimu bali ya kikaida.

Zamora na Faris (khj), wanaendelea kueleza kuwa, uhalisiajabu unaweza kuangaliwa kama mwendelezo wa uhalisia hasa kwa kuwa kimsingi unajihusisha na suala la hali ya uhalisi pamoja na uwasilishaji. Hata hivyo, unatofautiana na uhalisia wa kijadi kwa kuwa haudhibitiwi na misingi ya urazini unaohusishwa na kipindi cha baada ya utaalimifu wa kimagharibi. Hali hii inatokana na ukweli kwamba uhalisiajabu unavunja mipaka ya hali ya kawaida ya kuwako kwa kazi za fasihi. Herman na wenzake (2005), katika Wamitila (khj) wanauona uhalisiajabu kama ni utanzu. Mkabala huu wa kuangalia uhalisiajabu kama ni utanzu pia unaoungwa mkono na Zamora na Faris (khj). Mawazo haya yanaenda kinyume na mawazo ya Waliaula (2010), ambapo anauona mkabala wa uhalisiajabu kama nadharia.

Miongoni mwa vipengele vinavyohusishwa na uhalisiajabu kama vinavyojadilliwa na Wamitila (2013), ni pamoja na mbinu za kisimulizi za matukio yasiyokuwa ya kawaida, njozi au fantasia, michezo na utatizaji wa dhana ya wakati ambapo kwa kiasi kikubwa hutumia wakati wa kivisasili, matumizi ya mitindo ya udenguzi na uumbuzi. Pia, kazi za kiuhalisiajabu huwa na sifa ya umahuluti wa kitamaduni, kitanzu na mwingilianomatini, wahusika huwa ni wa kinjozi, visasili au fantasia na matendo yao hayadhibitiwi kamwe na kanuni wala sheria za maisha ya kawaida. Vilevile kunakuwa na ishara na usitiari na mfumo mzima wa uashiriaji ambazo zinatatiza suala la ubainishaji wa maana ya kifasihi ya kazi inayohusika. Aidha, kazi

za kiuhalisiajabu huwa na sifa ya kiontolojia, yaani ni mkondo unaoruhusu ukiukaji wa kazi wa kaida au mipaka ya kitanzu, kisiasa, kijiografia, kihistoria, au hata kiontolojia yaani hali ya kuwako ya kazi inayohusika.

Wamitila (2013), anaeleza kuwa katika fasihi ya Kiswahili ya baadhi ya kazi zinazohusishwa na uhalisiajabu ni: *Nagona* na *Mzingile* (E. Kezilahabi), *Babu Alipofufuka, Dunia Yao*, na kwa kiasi fulani *Nyuso za Mwanamke* (Said A. Mohamed), *Bina- Adamu!* na *Musaleo!* na labda kwa kiasi fulani *Dharau ya Ini* (K. W. Wamitila), *Ziraili na Zirani* (William Mkufya) na *Shimo la Maangamizi* (H. P. Simai). Wamitila anaendelea kusema kuwa kazi za fasihi za hivi karibuni zina sifa ya uhalisiajabu. Hata hivyo, anaamini kuwa hata kazi za mwanzo mwanzo za Fasihi Andishi ya Kiswahili zinasifa za uhalisiajabu. Anataja *Kusadikika, Kufikirika* na *Adili na Nduguze* za Shaaban Robet kuwa ni mifano ya kazi zenye mitindo ya kiuhalisiajabu.

Kwa hali hiyo utafiti huu umedhamiria kufanya uchunguzi wa kina katika riwaya za Kiswahili za Shaaban Robert za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze,* ili kuona namna mtunzi huyo alivyoumba/ alivyofumbata matumizi ya uhalisiajabu katika kusanii kazi hizo. Sambamba na hilo matumizi ya dhamira yamezingatiwa kama msingi mwengine muhimu wa kufikia mada husika ya utafiti huu.

1.3 Tatizo la Utafiti

Kulingana na mada ya utafiti huu isemayo: *Kuchunguza Uhalisiajabu na Dhamira katika riwaya za Kusadikika* na *Adili na Nduguze.* Mtafiti alitalii maandishi kadhaa na kubaini kuwa wataalamu mbalimbali wametafiti riwaya za Shaaban

Robert katika vipengele vya Fani na Maudhui na kutoa mitazamo yao tofauti. Miongoni mwa watafiti hao ni pamoja na Zamora (1995), Mbatiah (2002), Waliaula (2010), Wamitila (2013), Mwanzandi (2013), Salim (2015) na Saleh (2015), ambapo kila mmoja akiwa na malengo tofauti. Kwa mfano, Waliaula (2010), analinganisha uhalisiajabu katika riwaya ya *Dunia Yao* na ile ya Gunter Grass ya *The Tin Drum*. na kubaini kuwa riwaya hizi zimefanana katika matumizi ya kiuhalisiajabu. Anaueleza uhalisiajabu kwa kutumia neno uhalisiamazingaombwe kama nadharia. Anaonesha mfano wa uhalisiajabu alionao mhusika Oskar katika *The Tin Drum* kwamba uwezo wake wa kupasua vioo kwa kitendo cha kuimba tu ni mfano wa uhalisiajabu. Pia, Oskar anabakia kuwa mhusika wa kihalisiajabu kutokana na mhusika huyo kukataa mwenyewe kukua na kuamua kubaki akiwa kitoto cha miaka mitatu. Aidha, anajifanya mjinga na mpumbavu ingawa akiwa hivyo anao uelewa wa kina wa masuala ya kifalsafa, kifasihi na matini tata za kinadharia. Mhusika mwengine wa kihalisiajabu ni Raguna ambaye anaouwezo wa kuona mpaka ndani nyoyo za watu.

Ingawa Waliaula (khj) amelinganisha uhalisiajabu katika riwaya ya *Dunia Yao* na ile ya *The Tin Drum*, hata hivyo bado kuna maswali ya kujiuliza kuhusu uhalisiajabu pamoja na dhamira na vipengele vyake katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze* ambavyo ndio msingi wa maswali ya utafiti huu. Maswali hayo ni pamoja na: Mosi; Ni vipengele vipi vya uhalisiajabu vilivyobainishwa katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze?* Ni dhamira zipi za uhalisiajabu zilizobainishwa katika riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze?* Hivyo basi, kama tulivyoona hapo awali kwamba baadhi ya riwaya za Kiswahili zimefumbata mtindo wa uhalisiajabu.

Kutokana na maswali hayo, tatizo la utafiti huu ni: Kuchunguza uhalisiajabu na dhamira katika riwaya za Shaaban Robert za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umegawanywa katika malengo ya aina mbili: Lengo la jumla/ kuu na malengo mahsusi kama ifuatavyo:

1.4.1 Lengo Kuu

Kuchunguza uhalisiajabu na dhamira katika riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.*

1.4.2 Malengo Mahsusi

Utafiti huu una malengo mahsusi mawili yafuatayo:

i. Kubainisha vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.*

ii. Kubanisha dhamira za uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*.

1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:-

i. Ni vipengelevipi vya uhalisiajabu vilivyobainishwa katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze?*

ii. Ni dhamira zipi za uhalisiajabu zilizobainishwa katika riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze?*

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Umuhimu wa utafiti huu umejikita katika nyanja kuu mbili:

Kinadharia: Utafiti huu utatoa mchango katika taaluma ya fasihi kinadharia. Utawawezesha wasomaji wa kazi hi kuelewa namna ya kuchambua uhalisiajabu na dhamira zilizomo katika riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.* Wasomaji wanatarajiwa kupata maarifa yatakayowawezesha kuelewa namna uhalisiajabu unavyojidhihirisha katika riwaya za Kiswahili. Pia wasomaji watapata kuelewa namna nadharia ya Uhalisiajabu inavyoweza kufanyiwa uchambuzi katika riwayafasihi ya Kiswahili.

Kitaaluma: Utafiti huu umetarajiwa kuongeza maarifa hasa katika nadharia na mbinu za utunzi wa riwaya hususani za Kiswahili. Aidha, utafiti huu umeweza kutumika katika taaluma ya fasihi, hususani zile ambazo zimetumia mbinu ya kiuhalisiajabu. Kwa mantiki hiyo utafiti huu utakuwa ni marejeleo ya wahadhiri, walimu na wanafunzi wa ngazi mbali mbali. Pia, utafiti huu utaweza kuwachochea watafiti wengine kutupia jicho katika riwaya za Kiswahili ili kuchunguza mbinu za kiuhalisiajabu katika riwaya hizo..

1.7 Mipaka ya Utafiti

Shaaban Robert ameandika kazi nyingi za fasihi hasa zinazohusu utanzu wa ushairi na riwaya. Miongoni mwa riwaya zilizoandikwa na Shaaban Robert ni pamoja na:

Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini (1949), *Adili na Nduguze* (1951), *Kusadikika* (1981), *Kufikirika* (1983), *Wasifu wa Siti Binti Saad* (1991) Siku ya Watenzi Wote (1968), Utu Bora Mkulima (1968). Utafiti huu umejikita katika mada isemayo: *Kuchunguza Uhalisiajabu na Dhamira katika riwaya za Kusadikika na Adili na Nduguze*. Sababu ya uteuzi wa mwandishi huyu, mtafiti ametambua vizuri kuwa Shaaban Robert ni mwandishi mahiri na gwiji katika Fasihi ya Kiswahili ambaye ametoa mchango mkubwa katika kuendeleza fasihi hiyo. Sambamba na hilo, riwaya hizo teule zimebainika kutumia mbinu za uhalisiajabu na dhamira kwa kiwango ambacho mtafiti anaamini kinakidhi mada ya utafiti huu.Riwaya nyengine zimetumika kama ni kazi tangulizi na nyongeza muhimu za kukazia maarifa kulingana na malengo, maswali na mada ya utafiti. Hii ni kwa sababu isingekuwa rahisi kuchunguza riwaya zote alizotunga Shaaban Robert au za waandishi wengineo.

1.8 Muundo wa Tasnifu

Utafiti huu wenye mada isemayo: *Kuchunguza Uhalisiajabu na Dhamira katika* riwaya za *Kusadikika na Adili na Nduguze* umegawanywa katika sura kuu tano (5) zifuatazo:

Sura ya Kwanza; Utangulizi wa Jumla: Sura hii imehusu vipengele muhimu vifuatavyo: Utangulizi, usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, muundo wa tasnifu na hitimisho.

Sura ya Pili; Mapitio ya Kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia: Sura hii imelenga vipengele vifuatavyo:Utangulizi,Ufafanuzi wa dhana muhimu, mapitio ya

kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia: Nadharia ya Uhalisiajabu na na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na hitimisho.

Sura ya Tatu; Mbinu za Utafiti: Sura hii imewasilisha vipengele vifuatavyo: Utangulizi, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data, mbinu za ukusanyaji wa data, mbinu za uchambuzi wa data, kuaminika, kuthibitika kwa data za utafiti na hitimisho.

Sura ya Nne; Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data za Utafiti: Sura hii imejadili vipengele vifuatavyo: Utangulizi, usuli wa mwandishi Shaaban Robert, muhtasari wa riwaya ya *Kusadikika*,na riwaya ya *Adili na Nduguze,* vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*, Dhamira za uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze* na mwisho ni hitimisho.

Sura ya Tano; Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo. Sura hii imezungumzia vipengele vya msingi vifuatavyo: Muhtasari wa kila sura (sura ya kwanza hadi sura ya tano) kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti huu. Sura imetoa hitimisho. Hitimisho hilo limeonesha kwamba Shaaban Robert ametumia vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya teule. Pia, kwa kiwango kikubwa dhamira za riwaya ya *Kusadikika na Adili na Nduguze* zimejidhihirisha kupitia vipengele vya uhalisiajabu. Mwisho sura imemalizia kwa kutoa mapendekezo.

1.9 Hitimisho

Kwa hakika, sura hii imekuwa na thamani kubwa katika kuimarisha utafiti huu. Hii ni kwa sababu imefafanua kwa kina vipengele vya msingi vya kiutangulizi katika

utafiti huu. Vipengele vilivyojadiliwa ni pamoja na: Usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti ambayo utafiti huu ulikusudia kuyajibu na umuhimu wa utafiti. Sura hii pia imejadili juu ya muundo wa tasnifu na kumalizia na Hitimisho. Sura inayofuata ni Mapitio ya Kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii inalengo na shabaha ya kuchambua na kufafanua vipengele vya msingi vinavyohusika na maandishi yanayohusiana na kazi hii ya utafiti. Vipengele vilivyoangaziwa ni pamoja na: Ufafanuzi wa dhana muhimu, mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia.

2.2 Ufafanuzi wa Dhana Muhimu

Katika utafiti huu, dhana muhimu zimezingatiwa na kutolewa ufafanuzi wa kina kwa lengo la kuimarisha na kufanikisha malengo na maswali ya utafiti. Dhana za msingi zilizozingatiwa ni uhalisiajabu na dhamira. Ufafanuzi wa dhana hizo ni kama ifuatavyo.

2.2.1 Dhana ya Uhalisiajabu

Kama ilivyokwishaelezwa katika sura ya kwanza kuwa dhana ya uhalisiajabu ni changamano. Baada ya kupitia machapisho yaliyokuja na fikira na mawazo kuhusiana na suala la uhalisiajabu na vigawanyo vyake bado ni tata. Hii ni kwa sababu hadi sasa hakuna mgawanyo rasmi unaobainisha tanzu anuai za uhalisiajabu. Kwa mantiki hiyo, watafiti wamekuwa wakitofautiana katika kulijadili suala hili.

Mathalan Mutiso (2012) alifanya uchunguzi kuhusu mada ya *“Hirizi katika jamii za Waswahili”*. Katika uchunguzi huo Mutiso (khj) amebainisha kuwa hirizi pia ni sehemu ya uhalisiajabu ambapo visawe vyake ni pamoja na kinga, zindiko, hijabu, uchawi, pagao, sihiri, uganga (wa kuvaa mwilini), ndumba, urogaji, ulozi, uchomozi,

ramli, dawa, uwanga, uramali, mburuga, fungo nakadhalika. Hivyo uchambuzi wa uhalisiajabu hujikita kuchunguza namna vipengele hivi vinavyojidhihirisha katika kazi husika.

Mutiso (khj), alifanya uchambuzi wa namna utenzi wa Mwana Fatuma unavyonesha matumizi ya vipengele vya uhalisiajabu. Pia alifanya uchambuzi kuhusu utenzi wa Kiatu ambao unahusu kiatu cha Mtume Muhammad (S.A.W). Katika uchambuzi wake ameonesha namna kiatu kinavyoweza kuwa na nguvu za kiuhalisiajabu. Kiatu hicho kiliweza kutumika kama nguvu za kukinga, kuponya na hata kuweza kuondoa dhiki na matatizo miongoni mwa watu. Mutiso (khj) alishadidia uchambuzi wake huku akichambua uhalisiajabu uliomo katika kiatu katika jamii za Barahindi. Amesisitiza kwa kusema kuwa inaaminika kwamba kiatu kikiwekwa juu ya nyumba ya maskini na kisigino chake kuelekea juu, kiatu hicho huilinda nyumba hiyo. Pia katika jamii hiyohiyo inaaminika kuwa mchawi anaweza kusimamisha uvumaji wa upepo wa tufani na kunyesha kwa mvua ya mawe akiipiga mvua hiyo kwa kutumia kiatu. Katika jamii ya Wajapani inaelezwa kuwa Wajapani huamini ya kwamba mtu anaweza kupata nuksi iwapo atavaa viatu vipya na kwendea msalani. Matukio kama haya yote yanasifa ya uhalisiajabu kutokana na kuibua maajabu kwa vile hukiuka uhalisia wa kijamii.

Hart na Ouyang, (2015), wanasema kuwa uhalisiajabu ni dhana tata kutokana na oksimora iliyopo kwenye jina la dhana yenyewe - uhalisia na maajabu au mazingaombwe. Uhalisia ambao unahusu kuwasilisha na kuakisi uhalisi kama ulivyo ulimwenguni, unaegemezwa kwenye nadharia ya mwigo au uhalisia wa maisha halisi. Kanuni kuu katika uhalisia ni ile ya ushabihi kweli. Mazingaombwe au

maajabu kwa upande wake hukiuka mipaka ya uhalisi kwa kuhusisha hali, matendo, mielekeo au matukio ambayo yanavuka mipaka ya “ukawaida” wa uhalisi. Maajabu au mazingaombwe ni dhana inayoweza kutumiwa kueleza chochote kinachokiuka ujarabati zikiwemo imani za kidini, ushirikina, migani, visasili na kadhalika.

Wanjiru (2013), alipokuwa akifanya utafiti unaohusu mada isemayo *“Kuchunguza Uhalisiajabu katika Tamthiliya ya Ngoma ya Ng`wanamalundi”*anamnukuu Mbatiah (2001), akifafanua, istilahi ya uhalisiajabu na kusema imetumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo, mitindo ya uhalisiajabu imeelezwa kwa njia ya moja kwa moja kama kwamba ni mambo ya kawaida. Wasanii wanaotumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa, ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokana na maisha ya kawaida ya jamii inayohusika. Wanjiru (khj) ameendelea kutilia mkazo kuwa, uhalisiajabu huhusishwa zaidi na nchi zinazoendelea kutoka Bara la Afrika, Marekani ya Kusini na Asia.

Mawazo haya ya Wanjiru (khj), yanatatiza kuhusu chimbuko la uhalisiajabu. Tuonavyo ni kwamba mawazo haya yanatatiza kutokana na ukweli kwamba masuala ya uhalisiajabu kama vile; uchawi, hirizi, uganga, visasili vya kiuhalisiajabu havikuanza katika sehemu maalumu ulimwenguni bali hutokea katika jamii yoyote. Hivyo basi, tunaamini kwamba kila jamii ina vipengele vya uhalisiajabu ambavyo hujitokeza.

Waliaula (2010), anasema kuwa uhalisia mazingaombwe unapaswa kueleweka kwa kadiri fulani, kama mkabala wa kuwakilisha uhalisia kwa kukiuka mipaka, kuhujumu au kuvuruga usimulizi mbali na kukaidi kaida za lugha na ingawa ni mkabala wa

kifasihi unaonasibishwa zaidi na waandishi wa Amerika Kusini, umepenya kwingi duniani huku fasihi za janibu mbalimbali zikizungumzwa kwa dayalojia hii. Waandishi katika Afrika Mashariki waliotumia uhalisia katika kazi zao za awali kama vile Ngugi wa Thiong'o mwishowe wameishia kusombwa na wimbi hili la uhalisiamazingaombwe hasa katika riwaya yake ndefu ya '*Wizard of the Crow*' (2005).

Kwa misingi hiyo, maelezo ya Hart na Ouyang, Wamitila, Wanjiru na Waliaula (wameshatajwa) yamekuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu kwa kuwa yametoa ufafanuzi ambao umeweka wazi vipengele vya uhalisiajabu ambayo ndiyo mtafiti alivyokusudia kuvitafiti. Dhana ya uhalisiajabu ndio msingi muhimu katika kuimarisha utafiti huu na kufikia lengo la utafiti. Kwa sababu hiyo, utalii wa machapisho mbalimbali ulilenga kutambua kwa undani dhana ya uhalisiajabu. Hata hivyo mtafiti amebaini kuwa mtazamo wa uhalisiajabu una utata kueleweka wazi wazi. Kama alivyosema Wamitila (2013), moja ya ugumu wa kueleza uhalisiajabu ni kutokana na sifa ambazo zinahusishwa na mikondo au matapo mengine ya fasihi kama uhalisiafifi, ulimbwende, usasa na usasaleo/usasabaadaye nakadhalika.

Kwa hali hii Wamitilia (khj) amependekeza msingi wa kuvibainisha vipengele vya uhalisiajabu katika mkabala wa kifasihi kwa kuangalia Uhalisiajabu na Mtindo, Mbinu za Kisimulizi, Michezo na Utatizaji wa Dhana ya Wakati, Mgotanisho wa Uhalisia na Njozi za fantasia, mitindo ya udenguzi na uumbuzi, umahuluti wa kitamaduni na kitanzu na mwingilianomatini, usawiri wa wahusika, utambulisho na mawanda ya kihusika, ishara na uashiriaji na suala la uchimuzi na Uhalisiajabu na suala la ontolojia. Kwa sababu ya umuhimu wa mawazo haya mtafiti ameona ipo

haja ya kufanyiwa uchambuzi wa kina na hatimae kupata data zinazohusishwa na vipengele hivi vya uhalisiajabu.

Dhana ya uhalisiajabu ndio msingi muhimu katika utafiti huu kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti. Katika hatua inayofuata, mtafiti ameunga mkono mawazo ya Wamitila (2013) alichambua kwa kina vipengele vya uhalisiajabu kama ifuatavyo:

2.2.1.1 Vipengele vya Uhalisiajabu

Wamitila (2013) ameweka wazi kuwa uhalisiajabu una vipengele viingi. Baadhi ya vipengele hivyo ni kama vifuatazo:-

2.2.1.1.1 Uhalisiajabu na Mtindo na Mbinu za Kisimulizi

Wamitila (khj) ameeleza kuwa, sifa mojawapo ya kimsingi katika riwaya ya kihalisiajabu ni kuwepo kwa sifa na ukiushi wa kiwango kikubwa katika sawia ya kisimulizi. Kazi ya kihalisiajabu huwa na usimulizi unaokiuka mipaka ya urazini na ujarabati wa kawaida. Ingawa msomaji anaweza kuipata faida kubwa ya kazi yenyewe yapo matukio ambayo yanavuka mipaka ya ukawaida huo. Msomaji ameshawishiwa na msimulizi kukubali kuwa matukio yaliyomo katika ulimwengu wa hadithi ni matukio ya kawaida licha ya kwamba yanakiuka kanuni za kawaida anazozifahamu kutokana na uzoefu wake katika ulimwengu halisi. Wamitila (khj), anatoa mfano wa masimulizi katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001) ya Said Ahmed Mohamed, anamtarajia msomaji wake aukubali uwezekano wa gari kupaa angani ili kuepuka msongamano wa magari au kusafiri kwenda kwa babu yake kwa njia ya miujiza.

2.2.1.1.2 Mgotanisho wa Uhalisia na Njozi za Fantasia

Kazi zenye mielekeo ya uhalisiajabu huwa na sifa za kinjozi. Suala la njozi linaweza kufungamanishwa na mielekeo ya ndoto au motifu za ndoto hasa kutokana na mvurugiko wa matukio na usimulizi wake. Huu umekuwa msingi wa baadhi ya wananadharia wa uhalisiajabu kujaribu kuonesha uhusiano wa karibu uliopo kati ya nadharia hii na nadharia za saikolojia zinazohusishwa na wataalamu kama Carl Gustav Jung (Wamitila, 2013). Hii ni kusema kwamba watunzi wa kazi za fasihi wenye mielekeo ya kihalisiajabu huyasawiri maisha katika ulimwengu wa kindoto ambao kwa kawaida kuaminika kwake huwa kumekengeushwa na uhalisia wa kijamii. Kutokana na ndoto hizo ndimo tunamopata ujumbe na kile anachokieleza mtunzi.

Hii ni kusema kwamba katika kazi za uhalisiajabu masuala ya ndoto huwa yanasawiri uhalisia wa jamii. Muotaji katika kazi za uhalisiajabu huwa anatupatia ujumbe ambao unayachora maisha ya jamii husika. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kusadikika*Shaaban Robert amemtumia mhusika Sapa ambaye anaota ndoto inayomuonesha kuwa iwapo Salihi ataomba lolote bila ya kugawana sawa sawa dua ya Salihi haitokubaliwa. Kupitia tukio hili msanii ameonesha namna choyo na husda inavyoathiri watu kupatwa na kile wasichokitaraijia. Ndio maana Sapa anapata upofu kutokana na uchoyo wake.

2.2.1.1.3 Michezo na Utatizaji wa Dhana ya Wakati

Suala la wakati ni muhimu katika uchunguzi wa matini za kifasihi. Wamitila (kashatajwa), anasema kwamba riwaya ya kiuhalisiajabu hutumia wakati kwa namna isiyokuwa ya kawaida. Sifa moja wapo ni mparaganyiko na mchanganyiko wa dhana

nzima ya wakati kiasi kwamba msomaji anahisi wakati unaorejelewa si wakati anaouelewa bali ni wakati wa kivisasili. Anatolea mfano katika riwaya ya *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991), za E. Kezilahabi wahusika wanazungumzia wakati kwa njia isiyokuwa ya kawaida. Katika riwaya ya *Nagona* wahusika wanaokumbana nao msimulizi wanamueleza kuwa wamemsubiri kwa karne. Inawezekana pia wakati kufungamanishwa na wakati mwengine kwa kiasi ambacho wakati uliopo unafananishwa na wakati uliopita.

2.2.1.1.4 Mitindo ya Udenguzi na Uumbuzi

Kazi za uhalisiajabu huwa kazi umbuzi *(subversive)* na mwelemeo wake wa kuwa kila kitu katika umoja huchochea ukinzani na umoja wa miundo ya kitamaduni, kisiasa, hali ambayo inawavutia sana waandishi wa fasihi ya baadaukoloni. Udenguzi pia huweza kupatikana kwa kiwango cha kimuundo wa msuko. Riwaya za aina hii huvunjavunja muundo wa msuko ambao umezoeleka katika riwaya za kihalisia. Ile kaida ya usababishi na matokeo ambayo ni kaida ya msingi sana katika msuko wa jadi wa riwaya, inapuuziliwa mbali katika riwaya ya aina hii. Kwa mfano, ni vigumu kuyaeleza matukio ya msimulizi katika riwaya ya *Nagona* na ile ya *Mzingile*. Hii inatokana na ukweli kwamba kaida yenyewe ya usababishi imedenguliwa na tokeo limedenguliwa na kuvunjiliwa mbali.

2.2.1.1.5 Umahuluti wa Kitamaduni na Kitanzu na Mwingilianomatini

Waandishi wanaoandika kwa msingi huu wa kiuhalisiajabu wanashiriki na kujihusisha kwenye usemezano na mazungumzo ya kifasihi kwa kiasi kikubwa. Wamitila (kashatajwa), amewanukuu Herman na wenzake (2005), wakieleza kuwa Riwaya ya uhalisiajabu inahusishwa kwa kiasi kikubwa na muingilianomatini wa sifa

za kitamaduni za jamii na maeneo mbali mbali. Sifa ya umahuluti wa kitamaduni inapatikana katika fasihi hii kwa mapana sana. Sifa hii ya umahuluti wa kitamaduni imechukuliwa na baadhi ya wataalamu kama mojawapo ya sifa zinazowavutia waandishi wengi wanaoandika kwenye muktadha wa baadaukoloni kuupendelea mkabala huu kama bunilizi zao.Kwa mfano, Kezilahabi ni mmoja wa waandishi mashuhuri anayeandikia kwa kutumia mbinu ya uhalisiajabu. Mwandishi huyu aliamua kuchota mbinu hii hasa baada ya kazi zake kama vile Rosa Mistika kupigwa marufuku zikidaiwa kwamba zimeelezea masuala machafu wazi wazi. Kutokana na rungu hilo la dola pamoja na lawama kutoka kwa baadhi ya wahakiki Kezilahabi ametumia mbinu ya uhalisiajabu katika riwaya zake za *Nagona* na *Mzingile* ambapo katika riwaya hiyo maudhui yale yale yaliomo katika riwaya ya *Rosa Mistika* yanajitokeza lakini kwa mtindo wa uhalisiajabu.

2.2.1.1.6 Usawiri wa Wahusika, Utambulisho na Mawanda ya Kihusika

Wamitila (2013), anasema kuwa wahusika ni dira muhimu sana katika muundo wa riwaya yoyote. Riwaya ya kihalisia huwasawiri wahusika wake katika misingi ya kimuhakati au kimemisia kwa kuwatumia watu wa kawaida kama misingi ya usawiri huo. Hali hii ni tofauti na usawiri wa wahusika katika kazi za kihalisiajabu ambapo ontolojia au hali ya kuwako ya wahusika kihalisia inahusisha visasili, njozi au fantasia na matendo yao hayadhibitiwi kamwe na kanuni wala sheria na maisha ya kawaida kama ilivyo kwa wahusika wa kihalisia.

Pili, wahusika wanaopatikana katika kazi hizo hawaelekei kudadisi misingi ya matukio ya kimazingaombwe ambayo yanautawala ulimwengu wao. Kwa mfano, Wamitila (ktj), amemtolea mfano mhusika Kakulu katika riwaya ya *Mzingile* ambaye

haelekei kudadisi kudenguliwa kwa dhana ya matokeo ya kimaajabu katika maisha yake na wala hadadisi kudenguliwa kwa dhana ya wakati.

Aidha, katika riwaya ya kihalisiajabu si ajabu kwa wahusika wanaopatikana kwenye ulimwengu wa wafu kuingiliana moja kwa moja na wahusika wanaopatikana kwenye ulimwengu wa wanaoishi. Mathalani, sifa hii inapatikana kwenye riwaya ya *Nagona* ambapo kwenye Ngoma Kuu wahusika kama Marx, Freud na wengine wanashiriki. Matukio haya yanasisitiza kuwa katika uhalisiajabu kunakuwa na suala la kibunilizi.

2.2.1.1.7 Ishara na Uashiriaji na Suala la Uchimuzi

Wamitila (2013), amefafanua kwamba uhalisiajabu ni mkondo ambao unatambulishwa na mtindo kwa kiasi kikubwa. Suala la mbinu za lugha na mitindo ya kimuundo linachukua nafasi kubwa katika uchunguzi wa nadharia na mkondo huu. Mojawapo ya changamoto kubwa anayokumbana nayo msomaji wa kazi za uhalisiajabu ni kutokana na mtindo wake, hasa matumizi yake ya ishara, usitiari na mfumo mzima wa uashiriaji ambao unatatiza suala la ubainishaji wa maana ya kifasihi inayohusika. Riwaya za Kezilahabi za *Nagona* na *Mzingile* ni miongoni mwa riwaya za kihalisiajabu ambazo zinatatiza kupata maana kutokana na matumizi ya ishara zake.

2.2.1.1.8 Uhalisiajabu na Suala la Ontolojia

Wamitila (2013), amesema kwamba uhalisiajabu ni mkondo unaoruhusu ukiukaji wa kazi ya kawaida au mipaka ya kitanzu, kisiasa, kijiografia, kihistoria au hata ki-ontolojia yaani hali ya kuwako kwa kazi inayohusika. Baadhi ya wachambuzi wa nadharia hii wanadai kuwa hali hii ya kuwako kwa ontolojia inaweza kuangaliwa

kama msingi wa kuainisha mikondo ya uhalisiajabu. Wamitila (khj), anamuelezea Zlotchew (2007), kama anavyonukuliwa na William Spindler (1993), ambaye anaueleza uhalisiajabu wa ki-ontolojia kama aina mojawapo ya uhalisiajabu. Anasema kuwa mkondo huu unawasilisha matukio yasiyokuwa ya kawaida.

Waliaula (2010), anasema kuwa, ingawa inaweza kudaiwa kwamba kazi zaShaaban Robert kama vile *Kusadikika* (1951), na *Kufikirika* (1961), zilikuwana sifa fulani za uhalisiamazingaombwe, Wamitila (khj) anasisitiza mchango mkubwa wa Euphrase Kezilahabi katika kuleta upya katika ulingo wa Fasihi ya Kiswahili. Anaongeza kuwa, ulinganisho wa Fasihi ya Kiswahili na fasihi ya janibu mbalimbali kama vile unaotekelezwa kwenye makala ya Wamitila (2013), ndio njia mwafaka ya kuandamana ili kuuwezesha uhakiki kuwa na dayalojia ya kilimwengu ambayo Fasihi ya Kiswahili yenyewe tayari inashiriki kwa mapana na marefu.

Kwa hakika ufafanuzi wa sifa hizi za uhalisiajabu umekuwa na tija sana katika kuendeleza makusudio ya kufikia mada ya utafiti huu. Uchambuzi wa vipengele hivyo umekuwa ni muongozo muhimu ambao umesaidia sana utafiti huu. Hii ni kwa sababu matumizi ya vipengele vya kiuhalisiajabu vimechangia sana katika kuibua dhamira za uhalisiajabu katika riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze* ambao ndio msingi wa kufikia malengo, maswali na mada ya utafiti huu.

2.2.2 Dhana ya Dhamira

Ndungo na Wafula (1993), wamesema kwamba dhamira ni sehemu moja tu ya maudhui ya kazi ya fasihi. Hivyo dhamira ni kiini cha suala linalozungumzwa na mwandishi (msanii) katika kazi ya fasihi. Waandishi hawa wamezigawa dhamira

katika makundi mawili, nayo ni dhamira kuu na dhamira ndogo ndogo. Kwa mfano, unaweza kuwa na dhamira ya vita vya ukombozi, dhamira ya ujenzi wa jamii, utu bora, uvivu na ulanguzi.

Mawazo ya Ndungo na Wafula (khj) yametusaidia sana katika utafiti wetu namna ya kubaini dhamira katika kazi zilizotafitiwa. Hii ni kutokana na kwamba, waandishi hao wametoa mifano ya dhamira zinazojitokeza katika kazi za fasihi. Kwa hivyo, mtafiti amechukua maelezo hayo kama ni mwanzo wa kutafiti dhamira katika kazi teule.

Naye Sengo (1999), anaelezea kuwa dhamira ni sehemu ya maudhui, na maudhui ni yale yasemwayo na maandishi wa kazi za fasihi. Dhamira ya mtunzi ya asili yaweza kuwa ni mgogoro wa ndoa, maandishi yakatoa dhamira kadhaa juu ya kugongana wenyewe kwa wenyewe viongozi wa juu wa serikali.

Sengo (ameshatajwa) anaungana na Ndungo na Wafula (washatajwa) kuhusiana na dhamira. Mtafiti anakubaliana na mawazo hayo. Hata hivyo, ufafanuzi wa Sengo umeingia ndani zaidi kuhusiana na suala la dhamira, kwa sababu anafafanua zaidi kwamba mgogoro ndio unaoibua dhamira katika kazi za fasihi. Kauli hii ya Sengo imemsaidia mtafiti kuchunguza muelekeo wa kihalisiajabu uliyojitokeza katika kazi teule ili kubainisha dhamira zilizomo. Jambo hili ni wazi kwamba limesaidia kukamilisha madhumuni ya utafiti huu.

Ni ukweli ulio wazi kwamba, matumizi ya dhamira yameongeza ufanisi katika mada hii. Hii ni kwa sababu maelezo ya Ndungo na Wafula pamoja na Sengo (ktj)

yamezidi kutilia mkazo juu ya umuhimu wa dhamira katika kuimarisha malengo, maswali na mada ya utafiti huu isemayo: “Kuchunguza uhalisiajabu na Dhamira katika riwaya ya*Kusadikika* na *Adili na Nduguze”*.

2.3 Mapitio ya Kazi tangulizi

Katika utafiti huu mapitio ya kazi tangulizi yamegawanywa katika sehemu mbili kuu: Mosi, Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu nadharia ya Uhalisiajabu katika riwaya ya Kiswahili. Pili, Mapitio ya kazi tangulizi kuhusu riwaya za Shaaban Robert.

2.3.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Nadharia ya Uhalisiajabu katika riwaya ya Kiswahili

Nadharia ya Uhalisiajabu imefanyiwa utafiti na wanautafiti na wataalamu mbalimbali na kudhihirisha usadifu wake. Katika uhakiki wa kazi mbalimbali za fasihi hasa ya Kiswahili ikiwemo utanzu wa riwaya. Miongoni mwa watafiti kuhusu nadharia hiyo ambayo ndio msingi wa nadharia teule katika mada ya utafiti huu ni kama wafuatao:

Waliaula (2010), katika makala yake: *“Uhalisia na Uhalisimazingaombwe: Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum”* Katika makala hiyo, mtafiti alilinganisha uhalisiajabu katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006) ya Said A. Mohamed na ile ya Gunter Grass ya *The Tin Drum* (1962). Mtafiti huyo ameueleza uhalisiajabu kwa kutumia neno uhalisiamazingaombwe kama nadharia ambapo riwaya hizi zimelinganisha na kulinganua mtindo wa ujumi wa kisasa baadaye. Kazi hizi za kisanaa zinatumia mbinu za uhalisiajabu kama nyenzo za kuakisia jamii kwa kubirua hali halisi ya udhaifu, kuyumbayumba na ukosefu wa uthabiti na udumifu katika

maisha ya Afrika na Ulaya. Katika makala hii Waliula amegundua kuwa riwaya hizi zimeingiliana katika vipengele vya kuchora uhalisia na uhalisiajabu.

Pamoja na kwamba kazi ya Waliula (khj) imeegemea mkabala wa kiulinganishi katika kazi alizoziteua huku akitilia mkazo kuwa uhalisiajabu ni nadharia. Kazi yake imetoa uelewa wa namna ya kuchunguza uhalisiajabu katika riwaya teule za *Kusadikika* na *Adili naNduguze*kwa mkabala wa uhalisiajabu. Katika utafiti huu, imedhihirisha wazi namna wanafasihi wanavyoweza kuvitumia vipengele vya uhalisiajabu katika kazi za fasihi. Pia, mtafiti ameona namna matumizi ya vipengele vya uhalisiajabu vinavyotumiwa na mtunzi kupekeleka ujumbe kwa jamii kwa kuzingatia mada ya utafiti.

Wanjiru (2013), alifanya utafiti: *"Kuchunguza uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya ya Babu Alipofufuka na Watu wa Gehenna."* Katika utafiti huo alifikia hitimisho kwamba kazi alizozitafiti zimetumia sifa bainifu za uhalisiajabu kama nyenzo za kuakisi na kuangaza hali halisi ya udhaifu, kuyumbayumba na ukosefu wa uthabiti na udumifu katika Afrika na ulimwengu wote. Kwa jumla, utafiti huu umetilia mkazo kwamba, uhalisiajabu ndio nguzo kuu ya uendelezaji wa riwaya hizi katika uwasilishaji wa dhamira na maudhui. Dhamira kuu ya kuangaza uozo katika jamii na adhabu yake imefanikishwa kupitia uhalisiajabu katika vipengele vya wahusika na mandhari ambapo maudhui mbalimbali yamebainika.

Kazi ya Wanjiru (khj) ingawa haikujikita katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*, hata hivyo kazi hiyo imekuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu imechunguza namna matumizi ya uhalisiajabu yanavyojidhihirisha

katika riwaya alizoziteua kwa kutumia nadharia ya uhalisiajabu ambayo ndio msingi wa nadharia husika katika utafiti huu. Matumizi ya nadharia ya uhalisiajabu ndio yaliyotumika katika kufanikisha ubainishaji wa vipengele vya uhalisiajabu na dhamira katika riwaya teule ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*.

Wamitila (2013), aliandika makala yenye anuani *"Mikakati ya uhalisiajabu katika fasihi ya Kiswahili.* Katika makala hiyo ameeleza dhana ya uhalisiajabu, historia, sifa za uhalisiajabu huku akitoa mifano katika riwaya za Kiswahili kama vile riwaya za *Kichwa Maji*, *Nagona*, *Mzingile*, *Nyuso za Mwanamke* na *Dunia Yao*, na kuzilinganisha na kazi za kihalisiajabu za Kimagharibi. Wamitila (khj), amefikia hitimisho kwamba kamwe hatuwezi kuchunguza uhalisiajabu katika riwaya ya Kiswahili bila ya kurejelea kazi za Kimagharibi.

Mawazo haya ya ulazima wa urejelezi kama yanavyoelezwa na Wamitila (kashatajwa) yanahitaji kujadiliwa kwa kina ili kuona iwapo kuna ukweli wa ulazima huo. Aidha, ameeleza kuwa kazi ambazo zinaakisi uhalisiajabu sio tu za ulimwengu wa kibunifu, pia tajriba au uzoefu wa msomaji mwenyewe na kwa hali hii huitajirisha fasihi yenyewe. Makala haya yana umuhimu mkubwa katika utafiti huu kwa sababu yametoa uelewa wa kina juu ya dhana ya uhalisiajabu katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili na zile za kilimwengu. Pia, tumepata uelewa wa namna ya kuzishughulikia data zilizokusanywa katika riwaya teule kwa mkabala wa uhalisiajabu kwa kuzingatia malengo, maswali na mada ya utafiti huu.

Naye Nyambunga (2005), ameshughulikia *"Uhalisiajabu katika riwaya ya Musaleo na Babu Alipofufuka"*. Utafiti huu ulitilia mkazo"Sifa za Kiuhalisiajabu katika

riwaya ya *Musaleo* na *BabuAlipofufuka*." Katika utafiti huo kumeelezwa sifambalimbali za uhalisiajabu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa wahusika ambao walijengwa kiuhalisiajabu. Kazi hii pia ilikuwa na mchango mkubwa katika kukamilisha utafiti huu. Hii inatokana na kwamba baada ya kutalii kazi hio, mtafiti aliendelea kukuza maarifa hasa katika utumiaji wa nadharia ya uhalisiajabu ambayo ndio msingi wa mada ya utafiti huu kwa kurejelea riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*

Kwa ujumla uchambuzi kuhusu kazi tangulizi ambazo zimewahi kufanyiwa ufafanuzi wa vipengele na dhana ya uhalisiajabu kama mkabala wa fasihi ni nyingi.Hivyo basi kazi hizo zimekuwa na thamani kubwa katika kuimarisha utafiti huu kwa kuzingatia malengo na maswali ya mada ya utafiti isemayo: *Kuychunguza uhalisiajabu na dhamira katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze.*

2.3.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Riwaya za Shaaban Robert

Utafiti kuhusu riwaya za Shaaban Robert umefanywa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwa waliotafiti ni: Kezilahabi (1976), Senkoro (1976), Ponera (2010), Kabeja (2013), Maina (2013), Ambrose (2014), Saleh (2015), na Salim (2015).Ufafanuzi wa tafiti hizo ni kama zifuatazo:

Senkoro (1976),aliandika makala inayoitwa *"Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili,"* kwa ujumla aliangalia athari za utamaduni katika riwaya za Kiswahili, pamoja na mambo mengine, alifafanua kwamba riwaya ya *Adili na Nduguze* ina umbo la ngano na wahusika wake ni pamoja na watu, majini na mashetani. Pia,

ameeleza kuwa Shaaban Robert amezikashifu dini za Kiafrika kwa kuwa zina mila za kuabudu mizimu.

Kuhusu maelezo haya ya Senkoro (1976), Saleh (2015), amesema yanafaa kujadiliwa kwa kina, kwasababu aliyoyasema yanaonyesha kuwa, hakuangalia mila, desturi, silka pamoja na utamaduni wa Afrika, kwa wakati ambao ulikuwa haujapata athari kubwa za wageni walioingia Afrika. Makala ya Senkoro (khj) imesaidia sana kusukuma mbele utafiti huu na kufanya ufikie lengo lililokusudiwa kwa kurejelea riwaya teule ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.* Utafiti huu ulimfaidisha mtafiti kupata uelewa wa namna ya kubaini dhamira zinazojadiliwa na Shaaban Robert katika riwaya hizo. Kwa hivyo, mtafiti alichunguza ni kwa namna gani dhamira za kihalisiajabu zilivyobainishwa katika riwaya teule ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.*

Chuachua na wenzake (2009), waliandika makala inayoitwa *"Shaaban Robert Vita na Ukoloni."* Katika makala hiyo walifanya uchambuzi katika vitabu vya Shaaban Robert na kuthibitisha kuwa kazi za Shaaban Robert zimejaa ukoloni. Kwa kuonyesha ni namna gani wakoloni walitesa, kuwakandamiza pamoja na kuwanyonya watu weusi kwa miaka kadhaa. Katika uchambuzi wao, walionyesha dhamira ya kupinga ukoloni na kutafuta ukombozi kwamba imetamalaki katika riwaya za *Kusadikika* (1951), *Kufikirika* (1959), na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1949)

Kazi hii pia ilikuwa zana katika kufikia malengo ya utafiti huu kutokana na kuchambua dhamira muhimu za wakati wa ukoloni na mara tu baada ya ukoloni

ambapo ni wakati riwaya teule zilipoandikwa. Pia,Chuachua na wenzake (washatajwa) walifanya uchambuzi wa baadhi ya vipengele kama vile mandhari na wahusika ambavyo vipengele hivyo pia vilishughulikiwa katika utafiti huu. Kwa hali hii tulipata uelewa wa haraka kuhusu matumizi ya vipengele vya uhalisiajabu na dhamira kama vilivyotumiwa na Shaaban Robert katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*.

Kezilahabi (1976) alifanya utafiti katika mada;"*Shaaban Robert, Mwandishi wa Riwaya."* Matokeo ya utafiti wake yameonesha kuwa Shaaban Robert ni mtunzi wa riwaya mwenye uoni wa mbali zaidi ikilinganishwa na waandishi wengine wa Riwaya (Kezilahabi, 2011).Jambo linaloonesha kuwa Shaaban Robert ni mtunzi wa riwaya mwenye kuona mbali ni ile hali ya dhamira katika riwaya zake kusawiri hali za maisha si kwa jamii ya Watanzania peke yake lakini hata jamii mbalimbali za Afrika na ulimwenguni kote. Dhamira zinazoonekana kuwa ni za kilimwengu katika riwaya za Shaaban Robert ni pamoja na; usawa wa kijinsia, utawala wa sheria, umiliki sawa wa rasilimali miongoni mwa wananchi na ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi yanayohusu maisha yao ya kila siku.

Utafiti wa Kezilahabi (khj) haukuhusu kuchunguza uhalisiajabu katika riwaya za Shaaban Robert, jambo ambalo halikuwa lengo la utafiti wake, ila maelezo yake kuhusu dhamira zinazopatikana humo yamemsaidia mtafiti kuchambua dhamira zinazowasilishwa kupitia vipengele vya uhalisiajabu ndani ya riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze* ambazo ndio msingi wa utafiti huu.

Mjema (1990), aliandika makala yenye kichwa, "*Kusadikika*." Katika makala hiyo amechambua dhamira na baadhi ya vipengele vya kifani vinavyojitokeza katika riwaya hiyo. Miongoni mwa dhamira alizozichambua ni uongozi mbaya, utawala usiozingatia sheria, unyonyaji, rushwa na ufisadi. Kwa upande wa fani ameeleza kwa ufupi kuhusu matumizi ya lugha, muundo, mtindo, mandhari na wahusika.

Uchambuzi Mjema (khj) wa dhamira na vipengele vya fani umesaidia sana mtafiti katika kufikia madhumuni ya utafiti huu. Kwa mfano, amewazungumzia wahusika ambao wanapatikana katika riwaya hizo ingawa hakuwatazama kwa mkabala wa uhalisiajabu kama ambavyo utafiti huu umehusu. Hata hivyo, maelezo yake yamesaidia sana kuwafahamu vizuri wahusika katika riwaya ya *Kusadikika* ambayo utafiti huu umechunguza ukihusisha na riwaya ya *Adili na Nduguze* ambayo haikuchunguzwa na mtafiti tangulizi. Jambo hili limesaidia kurahisisha uchunguzi huu hasa katika kipengele cha uumbaji wa wahusika ambacho ni miongoni mwa kipengele cha uhalisiajabu.

Kezilahabi (2011), alifanya utafiti uliolenga *"Kuchunguza itikadi katika riwaya za Shaaban Robert."*Matokeo ya utafiti wake yameonesha kuwa riwaya za Shaaban Robert zimesheheni itikadi mbalimbali kama vile, ujamaa, ubepari, ukombozi na mapinduzi. Anasema kuwa itikadi hizi zinajitokeza kwa kiasi kikubwa katika riwaya za Shaaban Robert kwa sababu alikuwa ni mtu aliyeamini katika haki sawa kwa wanadamu wote. Kutokana na imani hiyo aliyokuwa nayo ndipo akawataka wanadamu wote kupendana na kuishi kwa pamoja. Itikadi ya ukombozi na mapinduzi zimejengwa katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* kupitia mandhari dhahania iliyojengwa katika akili ya msomaji ikiwa na lengo la kukwepa nguvu ya

dola. Itakumbukwa kwamba, riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika* ziliandikwa katika kipindi cha ukoloni na serikali ya kikoloni haikuwa tayari kukosolewa na mtu yeyote.

Kazi hii ilisaidia utafiti huu kwa sababu imechunguza masuala ya kiitikadi kama yanavyodokezwa na Kezilahabi. Mtafiti alibaini kwamba Shaaban Robert aliamua kutumia ishara nzito ikiwa ni pamoja na matumizi ya mbinu za uhalisiajabu ili kukejeli na kukosoa matendo ya wakoloni katika bara la Afrika Tanzania ikiwemo. Kwa mfano, Shaaban Robert katika riwaya ya *Kusadikika*amemtumia mhusika Jeta, mfalme wa nchi ya Majuju ambaye anakula mawe, majabali na maji mengi lakini mara kwa mara amekuwa akilia kiu na njaa. Msanii ameonesha namna wakoloni walivyokuwa hawatosheki kadri wanavyolinyonya na kulikandamiza bara la Afrika. Hakunashaka utafiti huo umekuwa na umuhimu mkubwa wa kuendelea kutilia mkazo matumizi ya nadharia ya uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze* ambazo ndio msingi wa mada ya utafiti huu.

Kyando (2013), aliandika makala iliyohusu *"Kuchunguza majina sadifa ya wahusika katika riwaya za Kusadikika na Kichwamaji."* Katika utafiti wake huu amebainisha kuwa majina waliyopewa wahusika yanalandana na vitendo, tabia, mwenendo na hulka zao na hivyo kuibua dhamira kupitia wahusika wa riwaya husika. Kazi hii ya Kyando (khj) ilakuwa na manufaa makubwa katika utafiti huu kwasababu imetusaidia kuelewa kuwa majina ya wanayopewa wahusika katika fasihi andishi yanasaidia sana katika kusawiri dhamira za mtunzi.

Ingawa halikuwa lengo la Kyando (khj) kubainisha matumizi ya uhalisiajabu kupitia wahusika, lakini kule kueleza tu dhamira kutokana na wahusika hao, kulimpatia mtafiti mwanga zaidi katika kuchunguza wahusika kwa mkabala wa uhalisiajabu katika riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze* ili kutimiza malengo ya utafiti huu.

Ambrose (2014), alifanya utafiti "Kuchunguza dhamira za kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert za *Kusadikika* na *Kufikirika*." Matokeo ya utafiti wake pamoja na mambo mengine umeelza dhamira mbalimbali kama uongozi katika jamii (uongozi mzuri na mbaya), utii wa sheria, kujifunza mambo kutoka jamii nyengine na masuala ya jinsia, amani, umoja na mshikamano.

Matokeo ya utafiti wa Ambrose (khj) yalikuwa na mchango mkubwa katika kupeleka mbele utafiti huu kwa sababu ulionesha dhamira mbalimbali hasa za kisiasa zinazopatikana katika riwaya za *Kusadikika* na *Kufikirika*. Kwa mnasaba huoutafiti huo umeengeza nguvu ya kufikia malengo na maswali ya mada ya utafiti kwa kurejelea riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*

Salim (2015), alifanya utafiti wenye anuani inayosema *"Kuchunguza ufasihi simulizi ndaniya hadithi ya Kusadikika na Adili na Nduguze."*Katika utafiti huo alichunguza namna Shaban Robert alivyochota tanzu na vipengele vya fasihi simulizi katika kuzisaniiriwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Pia, katika utafiti huu alichunguza dhamira zilizojitokeza ndani ya riwaya teule. Salim aligundua kuwa riwaya za Shaban Robert zimetumia vipengele kadhaa vya fasihi simulizi katika kuibua dhamira. Vipengele hivyo vya fasihi simulizi vilivyotumiwa na msanii ni pamoja na methali, misemo, hadithi za fasihi simulizi, wahusika wa fasihi simulizi na

mandhari ya fasihi simulizi. Kwa upande wa dhamira alizozigundua zinawiana na zile alizozigundua mtafiti katika utafiti huu ambapo amezitaja ni pamoja na ukoloni, uongozi mbaya, husda na choyo, ukosefu wa huduma za kijamii, utabaka, choyo nakadhalika.

Utafiti wa Salim (ameshatajwa) ulikuwa na manufaa makubwa katika kufikia malengo ya utafiti huu. Hii ni kwa sababu kazi alizozishughulikia ndizo ambazo zilishughulikiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, utafiti wake ulikuwa ni tofauti na huu. Hii ni kwa sababu yeye alichunguza ufasihi simulizi katika riwaya hizo kwa mkabala wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji lakini utafiti huu ulichunguza vipengele vya uhalisiajabu na Dhamira katika riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*kwa mkabala wa nadharia ya Uhalisiajabu na Mwitiko wa Msomaji.

Saleh (2015), alichunguza mada isemayo:“*Kuchunguza Ufasihi Simulizi katika riwaya ya Kusadikika na Wasifu wa Siti Biti Saadi*. Katika utafiti huo aligundua kuwa riwaya hizo zina matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi ambavyo ni dhana iliyofumbata dhamira za mtunzi. Utafiti huu pia ulitowa uelewa wa namna ya kuzichambua data zilizokusanywa katika riwaya ya *Kusadikika*. Pia, uchambuzi wake ulilingana na utafiti huukwa vile Saleh (khj) alichunguza namna vipengele vya fasihi simulizi vinavyoibua dhamira kama alivyochunguza mtafiti katika utafiti huu usemao Kuchunguza uhalisiajabu naDhamira katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Hii ni kusema kwamba kupitia utafiti huu pia mtafiti aliona namna dhamira zinavyoweza kuibuliwa kupitia mitindo ya kisanii kama vile uhalisiajabu.

Kwa hakika mtafiti ametalii machapisho kadhaa ambayo yanahusiana na mada husika. Kwa kufanya hivyo mtafiti ameweza kupata uelewa wa kina kuhusu mada ya utafiti huu. Pia, mtafiti amebaini kuwa watafiti waliotangulia walivyozungumzia kuhusu uhalisiajabu na dhamira na namna walivyowasilisha data zao. Vile vile, baada ya kupitia kazi hizo kwa kina mtafiti amebaini umuhimu mkubwa wa kazi tangulizi hizo ambazo makusudio yake ni kuhusisha na nadharia ya uhalisiajabu pamoja na riwaya teule za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.*

2.4 Pengo la Utafiti

Mtafiti ametalii maandiko kadhaa na kubaini kuwa hakuna mtafiti aliyeshughulikia moja kwa moja suala la uhalisiajabu katika riwaya za Shaaban Robert. Watafiti na waandishi wachache wamejaribu kulieleza suala la dhamira na fani, na kuacha vipengele vingine vidogo vidogo vinavyohusiana na uhalisiajabu katika kazi za riwaya teule za Shaaban Robert. Watafiti na waandishi hawa wamechambua dhamira na fani na kuonyesha ujumla wake, bila ya kuonyesha namna uhalisiajabu unavyojidhihirisha ndani ya kazi hizo. Hivyo utafiti huu umeona kuna pengo linalotoa nafasi ya kuchunguza uhalisiajabu na dhamira katika riwaya za Shaaban Robert, ili kubaini jinsi msanii huyo alivyotumia vipengele vya uhalisiajabu na dhamira katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.*

2.5 Mkabala wa Kinadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu na Mwitiko wa Msomaji katika uchambuzi wa data. Nadharia hizo zimechaguliwa na mtafiti baada ya kutathmini kwa kina na kugundua kwamba zimemuwezesha mtafiti kufikia hitimisho la utafiti huu. Nadharia hizi zimefanyiwa ufafanuzi kama ifuatavyo:

2.5.1 Nadharia ya Uhalisiajabu

Wamitila (2003), ameeleza kuwa uhalisiajabu ni dhana iliyobuniwa na msanii wa Ujerumani, Franz Roh katika kitabu chake *Nach-expressionismus, magischer Realismus* na inahusishwa na waandishi wa Marekani ya Kusini au hata nchi zinazoitwa Ulimwengu wa tatu na hutambulishwa na sifa mbalimbali. Sifa hizi ni za kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya kiajabu au kichawi kwa namna ya moja kwa moja na kwa namna inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida tu. Amesema kuwa, mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana.

Waliula (2010), akimnukuu Abrams (1999), anasema istilahi ya ‘uhalisiamazingaombwe’ ambayo mwanzoni ilitumika kuwahusu wachoraji katika miaka ya 1920, inatumika kufasili kazi za bunilizi za kinathari za Jorge Luis Borges wa Argentina, na halikadhalika kazi za waandishi kama vile Gabriel Garcia Marquez wa Kolombia, Isabel Allende wa Chile, Gunter Grass wa Ujerumani, Italo Calvino wa Italia, na John Fowles wa Uingereza. Waandishi hawa wanakutanisha uhalisia uliochongwa kwa njia maalum katika ruwaza inayobadilika badilika daima, huku wakiwakilisha matukio ya kawaida na maelezo ya kina sambamba na vipengele vya kifantasia na kindoto, na kwa kutumia mambo yaliyotokana na visasili na hekaya.

Wanjiru (2013), ameeleza kuwa hoja kwamba Roh ndiye mwasisi wa uhalisiamazingaombwe imepingwa au kurekebishwa na wahakiki kama vile Christopher Warnes (2006) anayedai kwamba, matumizi ya awali kabisa ya istilahi ya ‘uhalisiamazingaombwe’ yanapatikana katika maandishi ya mshairi Fridrich Freiherr von Hardenberg, maarufu kwa lakabu ya kishairi Novalis. Warnes (khj)

anasema kuwa, Novalis hakuikuza mno dhana ya uhalisiamazingaombwe pamoja na kwamba alikuwa wa kwanza kuitumia. Labda ndio sababu wengi humtaja Roh (ktj) aliyeitumia kinadharia kauli ya uhalisiamazingaombwe mwaka 1925 kama mwasisi wa istilahi hii. Green(2009),anasisitiza kwamba, mitindo na misingi ya uhalisiajabu katika fasihi kimatendo ilikuwa ya awali zaidi hasa katika kaida za Kiramsia (Romantism) ambapo masimulizi “yaliweka sambamba matukio ya kiajabuajabu na yale ya kawaida”.

Njogu na Wafula (2007), wamesema kuwa uhalisiamazingaombwe ni nadharia ambayo inakiuka sifa za uhalisia kama zilivyozoelezwa na waandishi wa karne ya kumi na tisa na ishirini. Katika uhalisiajabu, matukio yasiyoaminika (ya kifantasia) husawiriwa. Mambo ya kiajabu yanaelezwa kwa namna ya moja kwa moja na kuonekana kuwa ya kawaida. Hali ya kushangaza na kuogofya huwasilishwa kuwa ya kawaida katika uhalisiajabu; ndoto na uhalisi vinachanganywa.

D’Haen (2005), ameeleza kwamba uhalisiamazingaombwe ni tawi mahsusi la usasabaadaye *(postmodernism),* linaloonyesha sifa za usasabaadaye kama vile kujirejearejea, uziada uliopindukia uanuwai, mseto wa vitu, mwingilianomatini, kuchezea na kuyumbisha uthabiti wa wahusika na usimulizi vilevile kumchanganya msomaji kwa makusudi na hali kadhalika kufuta mipaka kati ya dhana, vitu au hali tofauti.

2.5.1.1. Mihimili ya nadharia ya Uhalisiajabu

Wanjiru (2013), alitalii kazi za wataalamu mbalimbali waliowahi kuzungumzia uhalisiajabu kama; Zamora (1993), (1995), Danow (1995), Cooper (1998), na

Encarta encyclopedia (2002), na kugundua nadharia ya uhalisiajabu ina mihimili kama ifuatayo:

i. Matokeo ya kiajabuajabu yanayoonekana ya kawaida, pia huwa na hali za kushangaza, kuduwaza na kuogofya.

ii. Uhalisi na ndoto vinachanganyika. Hakuna mipaka ya uhalisi na ndoto katika uhalisiajabu. Labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni.

iii. Mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa huvunjwa, manaake ni kuwa wanauhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu kama vile jamii, nchi au bara moja.

iv. Wakati na mahali zina uhusiano wa kiduara badala ya kistari. Inamaanisha kwamba jambo linaweza kujirudia kwa sura nyingine mahali pengine.

v. Uhalisiajabu umefungamana na sanaajadi kama vile visasili. Visasili ni hadithi zinazoeleza asili ya watu na matukio fulani.

vi. Matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Mtindo wa baadhi ya tanzu za fasihi simulizi hutumika. Jambo hili hufanywa kwa kumpeleka msomaji kwenye safari ya hali na matukio ya kikweli na yanayowezekana. Aidha, wasanii hutumia mbinu ya ukumbukaji na rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili.

vii. Mazingira ni sehemu muhimu sana katika aina hii ya fasihi. wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi

hurejelewa.Vilevile, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu.

viii. Uhalisiajabu unapinga uhusiano wa kadhia zinazotendeka katika maisha ya mtu kiutengano. Hali mbali mbali kama vile uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na utamaduni huonekana zikiingiliana.

Ni muhimu kueleza kwamba, katika utafiti huu, si mihimili yote ambayo itatumika. Mihimili itakayotumika ni ile tu, itakayofaa zaidi kufafanua riwaya tunazozichunguza ili kuweza kuangaza dhana ya uhalisiajabu. Riwaya hizo ni *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*

2.5.2 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Wafula na Njogu (2007), wamesema nadharia ya Mwitiko wa Msomaji iliasisiwa na James na wenzake katika miaka ya 1960-1970. Waasisi hawa ni Wajerumani, wanaamini kuwa kazi ya fasihi inapaswa kutazamwa kwa kulingana na mila, desturi na utamaduni wa msomaji. Kwani msomaji ana uhuru wa kutafsiri kama aonavyo kutokana na uzoefu wake, na si kutokana na uzoefu wa mwandishi. Wananadharia hawa wanaweza kuwekwa katika matapo matatu ambayo:

i. Wale wanaoangazia kwenye tajriba za kipekee za msomaji. Hawa ni pamoja na C. C. Lewis, (1961), Stanley Fish (1967), na Normana Holland (1968), ambao walikuwa Wamarekani.

ii. Wale wanaofanya majaribio ya kisaikolojia kwa kikundi maalumu cha wasomaji. Hawa ni Reuven Tsur, Richarad Gerring, David Miall na Donald Kuiken

iii. Wale wanaochukulia kwamba wasomaji wote wa kazi ya fasihi wataipokea kwa njia iliyosawa.

Hata hivyo, Njogu na Wafula (2007), wanasema Stanley Fish anadai kwamba sanaa ya maneno haichanganuliwi kwa kutumia mikakati ya jaribio la kisayansi. Anayefanya jaribio la kisayansi huweka mpaka wa kihisia na kimawazo kati ya nafsi yake na jambo linalomshughulisha.Wananadharia hao wanaeleza kuwa kazi ya fasihi inajikita katika ishara na taswira. Kutokana na ishara na taswira hizo matini za kifasihi huwa hazina maana moja bali zinakuwa na maana zaidi ya moja. Msingi mkuu wa nadharia hii ni kwamba kazi yoyote ya sanaa hurejelea kazi inayosomwa kwa fasili ili ithibitishwe kuwa kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji wa kazi ya fasihi. Aidha, hubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi yanavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji.

2.5.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Njogu na Wafula (2007), wanasema wananadharia ya Upokezi huuliza maswali ambayo kwayo misingi ya nadharia hii imejiegemeza. Maswali hayo ni kama haya yafuatayo:

i. Kuna uwiano wowote kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyoihakiki?

ii. Je, kila kazi ya fasihi ina maana kufuatana na msomaji binafsi na namna anavyoichukulia?

iii. Kuna wasomaji ambao husoma na kufasiri kazi za fasihi vizuri zaidi kuliko wasomaji wengine.

iv. Msomaji hutumia vigezo gani kujijulisha iwapo mawazo yake juu ya kazi fulani yanafaa au hayafai?

Kinoti (2012), anamnukuu Adena Rosmarin katika Murfin (1999), ambaye ameeleza kwamba kazi ya fasihi ni kama kinyago ambacho hakijakamilika na kwa hivyo mchongaji hujaribu kukikamilisha. Kwa hivyo, Kinoti (khj) amebainisha mihimili ya Mwitiko wa Msomaji kama ifuatayo:

i. Msomaji huikamilisha kazi ya sanaa kwa kuijaliza kwa usomaji makini au kwa kuidhalilisha kwa usomaji wa kiholela. Iser na Fish katika Njogu na Wafula (2007), wanadai kwamba kazi ya fasihi huwa na mapengo mengi ambayo msomaji hushurutika kutunga matini mpya ambazo zimechochewa na kuzalika kutokana na matini asili zilizoko kwenye kurasa.

ii. Nadharia hii inasisitiza athari za kazi za fasihi juu ya akili na maarifa ya mwandishi. Wasomaji hufasiri athari hizo kupitia njia tofauti tofauti kutegemea:

    a) Tofauti kati ya matini na hisia za kibinafsi za msomaji.

b) Namna matini inavyoelekeza au kutatiza mwitiko wa msomaji. Sifa inayozua usomaji mzuri ama mbaya wa kazi ya fasihi.

iii. Wananadharia hii wamebainisha njia mbili za usomaji wa kazi za fasihi:

a) Njia inayofafanua na kusisitiza mawazo ambayo kitambo yamejuilikana na kutambuliwa na msomaji.

b) Kuwasilisha kazi ya fasihi kimafumbo ili kumchochea msomaji kujitafutia na kujiamulia ujumbe uliomo katika kazi aliyoisoma. Kwa hivyo, mafumbo hayo yanapaswa kusomwa na msomaji mara kadhaa ili kupata ujumbe uliokusudiwa.

iv. Usomaji ni tendo linalofanywa na kutekelezwa na msomaji kwa wakati maalumu, kwamba wakati wa kusomwa kwa matini huathiri maana ya matini hiyo.

v. Msomaji anayetumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji hufuata hatua tatu, nazo ni:

a) Hurejelea kazi inayosomwa kwa tafsiri ili ithibitishwe kwamba kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji.

b) Hubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji.

c) Hudhihirisha maoni ya msomaji yanafungamana na mada muhimu za hadithi.

vi. Nadharia hii inazingatia usomaji, msomaji na upokezi.

2.5.2.2 Mapungufu ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Salim (2015) amesema, nadharia ya Mwitiko wa Msomaji imeelezwa kuwa na mapungufu kutokana na kuiona kazi ya fasihi kutokuwa na maana mpaka pale inapoingia mikononi mwa msomaji. Kwa mantiki hiyo, msomaji asiyekuwa makini anaweza kuipa kazi husika maana finyu.

Pamoja na mapungufu ya nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.mtafiti aliamini kwamba nadharia hiyo imemwezesha kuzihusisha dhamira za uhalisiajabu na uhalisia wa maisha ya kijamii. Hivyo basi mtafiti amezichagua nadharia za uhalisiajabu na Mwitiko wa Msomaji ili kuongoza utafiti huu. Katika utafiti huu nadharia ya uhalisiajabu imemwongoza mtafiti kubainisha vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya teule ambapo ndio lengo mahsusi la kwanza linalokwenda sambamba na swali la kwanza la utafiti huu. Vilevile nadharia ya Mwitiko wa Msomaji imetumika kubainisha dhamira za uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*ikiwa ndio lengo mahsusi la pili linalohusiana na swali la pili la utafiti huu.

Kwa muhtasari, Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Utafiti huu ulikuwa na malengo mawili. Lengo la kwanza lililenga kubainishavipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.*Lengo hili liliongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu. Lengo la pili linahusu kubainisha dhamira za uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Lengo hili liliongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.

2.6 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amefanya mapitio ya kazi tangulizi kuhusu vipengele kadhaa vinavyohusiana na mada ya utafiti. Sura hii imeanza kwa utangulizi, pia imeelezea dhana ya uhalisiajabu na dhamira. Vile vile, sura hii imetalii maandishi kadhaa kuhusu riwaya za Shaaban Robert kwa nia ya kubainisha pengo la maarifa lililoshughulikiwa katika utafiti huu. Mapitio haya yameonesha kuwa hakuna mtafiti aliewahi kufanya utafiti kwa nia ya kuchunguza uhalisiajabu katika riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Kutokana na hali hiyo mtafiti aliona kuwa kuna nafasi ya kufanya utafiti ili kujaza pengo hilo la maarifa kwa kuchunguza uhalisiajabu na dhamira za mtunzi katika riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Sura hii pia imefanya uchambuzi wa nadharia ya Uhalisiajabu na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambazo zimeongoza utafiti huu. Mwisho, sura hii imetoa hitimisho. Katika sura ijayo itahusu mbinu za utafiti vilivyotumika katika utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Lengo kuu na la msingi la sura hii ni kujjadili vipengele vya msingi vya mbinu za utafiti vifuatavyo: Eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, mbinu za ukusanyaji data, uthabiti na kuaminika kwa data, mbinu za uchambuzi wa data na hitimisho.

3.2 Umbo la Utafiti

Utafiti huu ulitumia umbo la kimaelezo kwa kiasi kikubwa. Enon (1999), utafiti husemwa kuwa una umbo la kimaelezo pale data zinapokusanywa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Katika umbo la kimaelezo kwa kawaida data huwa haziwasilishwi kwa kutumia tarakimu. Hivyo, data za utafiti huu zilikusanywa na kuchambuliwa kwa njia ya kimaelezo na kitarakimu kwa kiwango kidogo sana kwa lengo la kufanya muhtasari wa malengo na maswali ya utafiti huu. Mtafiti alichagua mbinu hizi kwa sababu aliona ni njia muafaka katika kuchambua na kuwasilisha data zinazohusu uhalisiajabu.

Salim (2015), anamnukuu Robson, (2007), usanifu wa utafiti ni mfano wa ramani inayoonesha namna utafiti utakavyofanyika hatua kwa hatua hadi pale utakapokamilika. Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu ambapo aliteua riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze* ili kuchunguza uhalisiajabu na dhamira za uhalisiajabu vinavyotumiwa na Shaaban Robert katika riwaya teule.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ni utafiti wa maktabani. Hivyo basi, utafiti huu umefanyika katika maktaba teule zifuatazo: Maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), na maktaba kuu Zanzibar. (zote tawi la Pemba) Sababu ya kuchagua maeneo hayo ni kwamba mtafiti aliamini atapata machapisho mbalimbali yanayohusiana na utafiti huu.Hivyo mtafiti amechagua maeneo hayoakiwa na imani kubwa kwamba zitamwezesha kupata data za utafiti huu ipasavyo.

3.4 Walengwa wa Utafiti

Kwa mujibu waEnon (1998),anasema kuwa walengwa wa utafiti ni jumla ya watu, wanyama au vitu ambavyo vimekusudiwa kufanyiwa utafiti. Kundi lengwa ndilo ambalo hujumuishwa katika matokeo ya utafiti. Kwa hiyo, walengwa wa utafiti huu ni riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Mtafiti amechagua riwaya hizo kwa sababu aliamini kuwa kuna matumizi ya uhalisiajabu na dhamira ndani yake. Hivyo, ilionekana ipo haja ya kufanya utafiti huu ili kuweka wazi malengo na maswali ya mada ya utafiti huu.

3.5 Sampuli na Usampulishaji

Enon (1998) ameeleza kuwa, usampulishaji ni kitendo cha kuchagua kikundi kidogo cha vitu au watu kutoka kundi lengwa ili litumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lote linalotafitiwa. Katika taaluma ya utafiti kundi hili dogo huchaguliwa ili kutoa data na hatimae kuliwakilisha kundi kubwa linalotafitiwa kwa kuwa sio rahisi kutafiti kundilengwa zima. Zipo mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa katika uteuzi wa sampuli, lakini utafiti huu ulitumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu.

Uteuzi wa madhumuni maalumu hufanyika kwa kutegemea malengo mahususi ya mtafiti. Kwa kutumia mbinu ya madhumuni maalumu mtafiti huteua sampuli yake kwa kuamini kwamba itajibu maswali ya utafiti (Powell na Conway, 2004). Katika kutoa maelezo zaidi kuhusu mbinu hii Kombo na Tromp (2006) wanasema, ni uteuzi ambao mtafiti kwa makusudi hulenga kuteua kundi la vitu/watu ambao ameamini kuwa ni raslimali aliyoitegemea katika utafiti wake. Mbinu hii humpa mtafiti uhuru katika kuteua sampuli ambayo aliamini itawezesha kujibu maswali ya utafiti.

Mbinu ya uteuzi wenye madhumuni maalumu ilitumika kuteua riwaya za *Kusadikika na Adili na Nduguze* miongoni mwa riwaya nyingi zilizotungwa na Shaaban Robert. Riwaya hizo ziliteuliwa kutokana na uelewa wa awali wa mtafiti kwamba, ni riwaya zilizofumbata vipengelembalimbali vya uhalisiajabu. Kwa hali hiyo data zilizokusanywa zimepelekea kufanikisha malengo na kujibu maswali ya utafiti huu.

3.6 Ukusanyaji wa Data

Katika utafiti wowote ule wa kitaaluma huwa kunakuwa na data za msingi/awali na data za upili/fuatizi. Katika utafiti huu mtafiti alikusanya data za msingi na za upili ili kuweza kukamilisha malengo na maswali ya utafiti huu wenye mada: *Kuchunguza Uhalisiajabu na Dhamira katika riwaya za Kusadikika na Adili na Nduguze.*

3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti. Kwa kawaida data hizo huwa hazijakusanywa kama sehemu ya utafiti mwengine wowote (Furlong, 2000). Young (1984), amesema kwamba data za msingi zinapofanyiwa uchambuzi na kuandikwa kama sehemu ya tasnifu hugeuka na kuwa data za upili.

Data za msingi za utafiti huu zilikusanywa kutoka riwaya teule za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*.

3.6.2 Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo tayari zilikwishakusanywa na watafiti wengine kwa ajili ya kutimiza malengo ya utafiti wao na kuandikwa katika ripoti, makala, majarida, wavuti na vitabu, tayari kwa ajili ya kusomwa kama marejeleo katika maktaba mbali mbali (Creswell, 2009).Katika utafiti huu, data za upili zimekusanywa kupitia tasnifu , makala, majarida na vitabu vyenginevyo vyenye uhusiano na mada ya utafiti huu na kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiti.

3.7 Mbinu za Kukusanya Data

Kothari (1990) ameeleza kuwa.mbinu ya ukusanyaji wa data kuwa ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kufanikisha lengo lake la utafiti. Utafiti huu ulikusanya data zake kwa kutumia mbinu yausomaji makini maktabani na mbinu ya upitiaji wa nyaraka. Mbinu ya usomaji makini ilitumika kukusanya data za msingi na mbinu ya upitiaji wa nyaraka ilitumika katika kukusanya data za upili.

3.7.1 Mbinu ya Usomaji Makini

Mbinu ya Usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data kutoka katika machapisho yaliyoteuliwa (Kothari, 1990). Mbinu hii hufanyika kwa mtafiti kukusanya data kwa kusoma matini teule huku akinukuu data kutegemea malengo ya utafiti wake. Salim (2015), amesema kuwa hii ni mbinu ya usomaji makini kwa sababu mtafiti husoma

kazi hizo tena na tena mpaka pale anapojiridhisha kuwa sasa amepata data alizokuwa anazihitaji katika kukamilisha malengo ya utafiti wake.

Data za msingi katika utafiti huu ndizo zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini kutoka katika riwaya teule za Kusadikika na Adili na Nduguze. Katika kufanikisha zoezi la ukusanyaji wa data, mtafiti aliandaa daftari maalumu ambalo aliligawanya katika sehemu kuu mbili na kila sehemu ikiwa na kichwa cha habari kinachohusiana na malengo mahususi na maswali ya utafiti huu. Hii ilirahisisha zoezi la ukusanyaji wa data ambapo mtafiti alipobaini maneno, sentensi au aya katika riwaya teule inayohusiana na utafiti husika basi aliyadondoa katika daftari hilo kama lilivyopangwa.

3.7.2 Mbinu ya Upitiaji wa Nyaraka

Neno “nyaraka” kama lilivyotumika katika utafiti huu linarejelea machapisho na maandiko mbali mbali yanayopatikana katika maktaba. Kwa ujumla mbinu ya upitiaji wa nyaraka maktabani ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti kudurusu machapisho yanayohusiana na mada yake ya utafiti kwa uzingativu (Kothari, 1990).Data za upili pamoja na kutumika katika kushadidia hoja zitokanazo na data za msingi katika uchambuzi wa data pia hutumika katika uandishi wa sura ya pili ya tasnifu inayohusika na “mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Data za upili katika utafiti huu zilikusanywa kutoka katika machapisho yanayopatikana katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), na maktaba kuu Zanzibar (zote tawi la Pemba). Katika maktaba hizi, mtafiti amesoma makala, ripoti, tasnifu, majarida,

vitabu na maandishi pepe katika wavuti na tovuti zinazohusiana na mada ya utafiti wake.

3.8 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data kwa mujibu wa Kothari (2013), ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Katika utafiti huu mbinu ya chambuzi wa data itakayotumka ni Mbinu ya Mkabala wa Kimaelezo na kitarakimu.

3.8.1 Mbinu ya Mkabala wa Kimaelezo

Kombo na Tromp (2006), wamesema kwamba uchambuzi wa data kwa mkabala wa kimaelezo ni ule unaofanyika kwa njia ya maelezo. Katika mkabala huu data hukusanywa, kuwasilishwa na kufanyiwa mjadala kwa njia ya maelezo. Hii ni kusema kwamba mkabala huu huwa hautumiitarakimu katika kuziwasilisha data. Hivyo basi, utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaelezo na Kitakwimu / kitarakimu kwa kiwango kidogo sana ili kurahisisha ufahamikaji na kuweka muhtasari wa data zilizowasilishwa na kuchambuliwa na kwa kuzingatiamalengo na maswali ya utafiti huu.

3.9 Zana za Kukusanyia Data

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia zana zifuatazo:

3.9.1 Shajara

Kamusi ya TUKI (2013) wameeleza, shajara ni kitabu cha kuwekea kumbukumbu za kila siku. Zana hii ilitumika kuhifadhi kumbukumbu za data zilizopatikana katika

utafiti huu. Kwa kutumia zana hii, mtafiti alinukuu katika shajara hiyo data zilizokusanywa wakati wa utafiti kulingana na mada ya utafiti.

3.9.2 Kompyuta

Kompyuta ni zana muhimu na ya msingi sana ambayo mtafiti aliitumia tangu mwanzo hadi mwisho wa utafiti wake. Kompyuta ni mashine ya kielektroniki inayotumika kuhifadhi na kusarifu taarifa zinazoingizwa ndani yake (BAKIZA, 2010).Mtafiti aliitumia zana hii kuchapa kazi yake ya utafiti, kuhifadhi data, kutafuta machapisho na maandiko mbalimbali yahusuyo utafiti huu yanayopatikana katika tovuti na wavuti mbalimbali.

3.9.3 Simu ya Mkononi

Simu ni chombo kinachopokea na kupeleka taarifa sehemu mbalimbali kutokana na mitambo yake ilivyosukwa kitaalamu. Pia, simu hutumika kurekodi mazungumzo, kuandika ujumbe, kupiga picha na kufanya kazi nyingine mbalimbali hata za mahesabu. Katika utafiti huu,simu ilitumika kuingia katika wavuti na kupitia machapisho yanayohusiana na mada ya utafiti. Simu iliyotumika ni aina ya “Smartphone.”

3.10 Hitimisho

Sura hii imehusu mbinu za utafiti. Katika sura hii imejadiliwa kuwa eneo la utafiti ni katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na maktaba kuu Zanzibar (zote, tawi la Pemba). Walengwa wa utafiti huu ni riwaya za Kiswahili za Shaaban Robert: *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.* Mbinu za usampulishaji zilizotumika ni mbinu ya uteuzi wa madhumuni

maalumu. Aidha wateuliwa ni riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Sura hii pia imebainisha na kujadili mbinu zilizotumika kukusanya data za utafiti huu ambazo ni; mbinu ya mapitio ya machapisho. Aidha, mbinu iliyotumika kuchambua data za utafiti huu ni mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui. Katika sura inayofuata imehusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti huu.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii imewasilisha na kuchambua data zilizopatikana katika utafiti huu kuhusiana na mada ya utafiti. Utafiti huu ulilenga kuchunguza uhalisiajabu na dhamira katika riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Sura hii imekusudia kuweka wazi vipengele vya msingi vifuatavyo: Usuli wa mwandishi - Shaaban Robert na muhtasari wa riwaya teuleza *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Vile vile sura imekusudia kufanya uchambuzi wa kinawa data za utafiti kwa kuzingatia malengo mahsusi na maswali ya utafiti huku uchambuzi ukiongozwa na nadharia teule. Mwisho sura itamalizia kuweka Hitimisho la sura nzima.

4.2 Usuli wa Mwandishi, Shaaban Robert

Ponera (2010), Garnier (2012), Kombo na wenzake (2014), wameeleza kuwa, Shaaban Robert anatokana na kabila la Kiyao kwa upande wa babu zake ambao walitokea Tunduru mkoani Ruvuma. Yasemekana babu yake Shaaban Robert alikuwa mchuuzi na pia tabibu aliyejulikana kwa jina la Kanduru. Jina hili lilidhaniwa kuwa ni la Kiyao.Mama yake aliitwa Mwanamwema; kwa kifupi Mwema binti Mwidau. Huyu alikuwa katika ukoo wa kina Mzee Mwalimu Kihere wa Kihere, Machui kabila ya Wamwamwende, moja ya makabila ya Kiswahili ya mwambaowa Pwani ya Afrika Mashariki.

Shaaban Robert alizaliwa Januari mosi, 1909 kwenye Kijiji cha Vibambani, jirani na Machui, kilomita 10 kusini mwa mji wa Tanga. Asili ya jina Robert ni mwajiri wa babu yake ambae aliitwa 'Roberto' asili yake kutoka Italia. Bibi yake Shaaban

alipokuwa na ujauzito alikuwa akianika uduvi katika ufukwe wa Bahari ya Hindi mjini Dar es Salaam, eneo la Kurasini katika shamba la minazi. Uchungu ulimshika huko huko ufukweni na alipofika nyumbani akajifungua mtoto wa kiume. Watani walimuita jina la ufukwe kwa sababu ya kazaliwa kwake ufukweni. Lakini baadaye akaitwa Roberto jina ambalobaadaye alijiita Robert.

Shaaban Robert alisoma jijini Dar es Salaam tangu mwaka 1922 hadi mwaka 1926 katika shule ya msingi ya Kichwele (sasa Uhuru Mchanganyiko). Alikuwa mtu wa pili kati ya wanafunzi kumi na mmoja waliofaulu mitihani yao na kupewa cheti cha mtihani wa mwisho wa darasa la nne la Kiingereza wakati huo ulioitwa “Central School Leaving Certificate examination.”Shaabani Robert hakuwa na elimu kubwa kishule bali alijielimisha mwenyewe kwa njia ya posta na kwa kujisomea vitabu. Barua zake zinaonesha kuwa alikuwa akilipia masomo ya posta kutoka Uingereza na Afrika Kusini. Huenda tabia hii ya kusoma ndio iliyomsukuma kuwa mwandishi.

Wakati wa uhai wake Shaaban Robert alifanya kazi ya ukarani wa serikali. Shaaban Robert alianza kazi ya ukarani katika idara ya forodha. Alianzia Pangani huko mkoa wa Tanga na kuhamishiwa katika vituo mbalimbali kama vile Moshi na Arusha, kisha akarudishwa Tanga tena, kabla ya kupelekwa Dar es Salaam na Kwale. Kutokana na utendaji mzuri, Shaaban Robert alipanda cheo kutoka ngazi ya Daraja la III la juu alilokuwa nalo mwaka 1929 hadi Afisa utumishi mwenye Daraja la II mwaka 1944. Alipata pia kuwa mjumbe wa asasi mbalimbali zilizohusu lugha, taaluma na utawala. Miongoni mwa asasa alizowahi kuwa mjumbe ni Kamati ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (Kuanzia mwaka 1953), Bodi ya Lugha ya Tanganyika, Chama cha Majadiliano cha Tanga, na Halmashauri ya Mji wa Tanga.

Vile vile, alipata kutunukiwa tunzo ya uandishi ya Margaret Wrong Prize, tunzo ya Mjumbe wa Himaya ya Kiingereza na Tunzo ya Mwandishi Bora ya Wizara inayosimamia utamaduni Tanzania (1987).

Kuhusu maisha yake katika fasihi, Shaaban Robert alianza kujidhihirisha mapema kuwa na kipaji cha uandishi wa kazi za fasihi. Alianza kwa kuchapisha mashairi na insha fupi katika gazeti la mambo leo na magazeti mengine katika miaka ya 1930. Kazi yake ya kwanza kabisa iliyopatikana ilichapishwa katika gazeti la Mambo Leo la Februali 1932 uk. 34. Ni barua kwa mhariri yenye jina la “Hirizi ya Shilingi Mia.” Tawasifu yake mwanzo ambayo haikuchapishwa iliandikwa mwaka 1936. Wakati wa vita vya pili vya dunia mwaka 1939 hadi 1945 alianza kutunga *Utenzi wa Vita vya Uhuru* na Utenzi huu alianza kuuchapisha mwaka 1941 kwa mfululizo katika gazeti la Mambo Leo kwa kipindi chote cha vita. Bilashaka utenzi huo wenye beti 3000 ndiyo ulimpa umaarufu mkubwa kama mwandishi kwa utawala wa kikoloni. Utenzi huo baadae ulichapwa kama kitabu munamo mwaka 1961.

Katika maandishi yake Shaaban Robert alilenga sana utu, nafasi ya mwanamke katika jamii, ukombozi wa bara la Afrika, kukuza lugha ya Kiswahili, na maendeleo. Shaaban Robert ameandika riwaya tisa ambazo ni; *Utu Bora Mkulima* (1968) *Kusadikika* (1951), *Adili na Nduguze* (1952), *Maisha Yangu na Baada ya MiakaHamsini* (1949), *Wasifu wa Siti Binti Saad* (1967), *Siku ya Watenzi Wote* (1968), na *Kufikirika* (1968)

Shaabani Robert alifariki mjini Tanga tarehe 20 /06/ 1962 akiwa na umri wa mika 53 tu. Ponera (2010), anamnukuu Yusuf Ulenge (Mdogo wa Shaaban Robert) akieleza

kuwa Shaaban Robert alifariki baada ya kudhoofika afya yake kutokana na kufanya kazi kupita kiasi bila mapumziko kulikoambatana na upungufu wa damu. Taarifa nyingine zinasema alifariki kutokana na kuugua kifua kikuu. Alizikwa katika makaburi ya familia huko Vibambani, ambako pia amezikwa mama yake, mtoto wake Hussein, dada yake na jamaa zake wengine.

4.3 Muhtasari wa Riwaya ya Kusadikika

Kusadikika ni riwayailiyotungwa naShaaban Robert. Riwaya hii inasimuliya kisa cha mhusikaKarama na kushtakiwa kwake kwa kosa la kuanzisha elimu ya uanasheria katika nchi ya Kusadikika. Sura ya kwanza inahusu kesi ya utetezi wa Karama na wajumbe wake sita; Auni, Kabuli, Ridhaa, Buruhani, Fadhili na Amini, waliochaguliwa kwenda kuzitalii nchi za kigeni kwa lengo la kuleta maendeleo katika nchi ya Kusadikika, ambapo malipo na jaza yao ikawa ni kuadhiriwa na kuingizwa gerezani. Mwisho, hadithi inamalizia kwa hukumu ambapo, Karama alionekana kwamba hakuwa na hatia, bali alikuwa anataka kuisaidia nchi ya Kusadikika kwa njia ngeni. Kwa mfano, hadithi hiyo, inaanza kwa msanii kusema:

> "… Jalali Mfalme na Madiwani wakuu wa baraza. Nataka kuweka mbele yenu mashitaka ya Serikali ya Kusadikika juu ya Karama, raia mmoja alielindwa na ulinzi wa Mfalme … Alipofika mbele yangu mara ya kwanza aliulizwa kama alikuwa mwalimu wa uanasheria. Alijibu upesi kama aliyeona ametunukiwa hadhi kubwa" (uk. 1- 3).

Mfano wa hapo juu unaonesha namna msanii alivyobuni kisa ili kupata mfululizo wa matukio yatakayokamilisha kazi yake. Kwa mfano, msanii anaanza kwa kuonesha namna uongozi ulioko madarakani unavyowakandamiza watu kutokana na

kutokutenda haki. Tukio hilo ndilo linalozaa matukio mengine yanayofikisha ujumbe wa mwandishi.

Sura ya pili inayoitwa “Uana Sheria.” inaonesha hukumu ya Karama kwa hatia ya kuanzisha elimu ya uanasheria, Waziri Majivuno aliyoiita `Elimu ya kupingana na sheria, sehemu hiyo inaelezea ombi la Karama la kupewa siku sita ili kutoa ushahidi wa kile anachokisema. Tumeoneshwa mjadala mkali kuhusiana na ombi hilo, hata hivyo, Mfalme anaamuru Karama akubaliwe ombi lake.

Sura ya tatu imeitwa Mjumbe wa Kaskazini. Sehemu hii imeelezea namna mjumbe wa Kaskazini, Buruhani alivyokumbana na masaibu, hata hivyo, juhudi zake hazikuthaminiwa na Wasadikika. Mathalan, Buruhani alieleza kwamba, maendeleo huletwa na umoja na kuwepo miji safi na kukuzwa kilimo kwasababu ndio uti wa mgongo. Hata hivyo, jaza yake ikawa ni kuadhiriwa na kupewa kifungo cha maisha. Msanii anatueleza hilo kwa kusema:

Sura ya nne imeitwa Mjumbe wa Mashariki. Data zilizokusanywa katika sehemu hii zimeonesha kwamba, mjumbe wa Mashariki ni Fadhili. Mjumbe huyo, alitalii sehemu za Mashariki na kubaini kuwa, Mashariki walipiga hatua za maendeleo kwa kukomesha vita vya wenyewe kwa wenyewe kwani havileti amani ya kudumu ila ni visasilisi, kuendeleza ushirikiano, kutimiza elimu kwa wote na kuamini Mungu mmoja. Hata hivyo, kwa wasadikika wasiohitaji mabadiliko, ilionekana uzushi na uongo na jaza ya Fadhili ikawa ni Gerezani

Sura ya tano imeitwa `Mjumbe wa Kusni`. Sura hii imeelezea suala la ulafi miongoni mwa viongozi. Pia, data zinadokeza mbinu zilizotumiwa na nchi za Kusini katika kupiga hatua kubwa za maendeleo. Mbinu hizo ni pamoja na heshima, uhuru wa kila raia, mgawanyo sawa wa madaraka na matumizi bora ya nguvu za vyombo vya utawala. Msanii katika sura hii ametilia mkazo umuhimu wa kuheshimu haki za kibinaadamu. Msanii ameitaka jamii iheshimu kila mtu, kuwe na haki sawa kwa kila raia, mgawanyo sawa wa madaraka na matumizi mazuri ya vyombo vya kiutawala.

Sura ya sita imeitwa “Mjumbe wa Magharibi`. Mtafiti amebaini uvunjaji wa sheria na kukosa haki kwa watu wenye kudai mabadiliko. Aidha, sura hii imedokeza umuhimu wa huduma za kijamii. Kwa mfano tumeelezwa kwamba, bila ya huduma muhimu kama maji safi, hospitali, elimu na utawala wa sheria hakuna maendeleo kwa nchi yoyote. Vile vile, sura hii imedokeza athari za wivu, uongo na uchoyo kama ulivyompata “Sapa” kwa dua ya Salihi, ambapo Sapa anapata upofu kama ni matokeo ya choyo chake.

Sura ya saba imeitwa `Mjumbe wa Mbinguni`. Sura hiyo, imeelezea safari ya Ridhaa, mjumbe wa Mbinguni. Katika safari hiyo, mnaelezwa kwamba kila raia aheshimiwe. Aidha, sura imetilia mkazo kupinga dhuluma, matendo ya wivu na uchoyo, umuhimu wa mabadiliko katika jamii na bidii katika kazi. Pia, sura hiyo imedokeza imani ya mwandishi ya kuwapo kwa maisha baada ya kufa.

Katika sura ya nane, tumeelezewa safari ya mjumbe wa Aridhini. Mjumbe huyo ni Amini. Amini ameelezewa kwamba, alisafiri kwa ndege aina ya Mangera kutoka Kusadikika hadi ardhini. Pia, sehemu hii inasukumwa mbele kwa marejeo ya Amini.

Ambapo imeelezwa kuwa, Wasadikika hawakuwa tayari kupokea mabadiliko kama vile; kutengeneza bandari, viwanja vya ndege na barabara. Sura imemalizia kwa Karama kuonesha kwamba amemaliza ushahidi wake.

Sura ya mwisho ya riwaya ya *Kusadikika* imepewa jina la “Hukumu” Sura hiyo ndiyo inayotoa hitimisho ya kazi hiyo. Sura imeonesha kwamba Karama alikuwa hana hatia. Aidha, wajumbe sita nao walikuwa hawana hatia.

4.4 Muhtasari wa Riwaya ya Adili na Nduguze

Adili na Nduguze ni riwaya ambayo iliandikwa na Shaaban Robert. Riwaya ya *Adili na Nduguze* ilitungwa wakati wa ukoloni. Kwa mara ya kwanza ilitoka kama kitabu mwaka 1952. Katika kazi hii, kuna mtindo wa visasili ambavyo vimetumia wahusika wadudu, manyani, majini, wafalme na hata binadamu wa kawaida kama vile Adili. Matukio yameendelezwa kupitia kisa cha Adili na nduguze ambao waligeuzwa manyani kwa laana ya jini Huria kutokana na wivu na husda uliowasukuma kumtosa baharini ndugu yao.

Hivyo basi, kiini cha riwaya hii kmeaundwa na wahusika watatu ambao ni Adili pamoja na Hasidi na Mwivu ambao ni ndugu zake wa kuzaliwa. Matukio ya riwaya hii yamejengwa na wahusika hawa. Shaaban Robert amesawiri muundo wa riwaya hii kupitia utetezi ambao Adili ameutoa kwa kosa lililomfikisha mbele ya Mfalme, kosa la kuwanyanyasa wanyama. Maelezo yake yanatubainishia baadaye kuwa nyani wale wawili walikuwa ni Hasidi na Mwivu ambao walipata adhabu hiyo kutokana na ukatili waliomfanyia Adili wa kutaka kumuua kwa kumtosa baharini.

Kwa ujumla riwaya hii imesaniiwa ikiwa na uhalisiajabu ambao umekiuka matukio ya uhalisia ya kijamii ukweli ni kwamba kazi hii pia ina uhusiano mkubwa sana na jamii halisi ya watu kama mtunzi mwenyewe alivyodokeza katika utangulizi wake asemapo:

> “Mambo hasa yaliyotiliwa mkazo ndani yake ni ardhi na mimea yake, machimbo na hazina yake, biashara na faida yake; safari na manufaa yake: utajiri na baraka yake; ahali na heshima zao; na ndugu na matendo yao. Mambo haya huhusu watu wengi kama si dunia nzima” (uk. v).

Shaaban Robert anatoa maoni kuhusu aina ya viongozi wanaopaswa kuongoza nchi zetu ambazo zinakabiliwa na matatizo mengi. Anatumia sura nzima kueleza hili kupitia sifa za Mfalme Rai ambaye anatumia busara na maarifa katika kuwaongoza Waghaibu. Sifa hizo ndizo zinazofanikisha kuwepo kwa makusanyo mazuri ya kodi pamoja na maelewano na upendo baina ya watu wa Ughaibu. Uongozi bora, ndiyo kiini cha upendo na umoja katika jamii. Sifa za wema, kushiriki katika kazi, huruma na utoaji wa hukumu kwa kufuata misingi ya haki ndizo sifa alizotuonesha mtunzi kwamba zinafaa wawe nazo viongozi wetu kwa ajili ya ustawi wa jamii zetu.

Sura nyingi za kazi hii zimeundwa na suala la upendo wa dhati. Adili amewaonesha upendo ndugu zake hata pale wanapomtendea uovu uliokithiri. Hata kuwaadhibu baada ya wao kugeuzwa nyani, anasikitika na kusita kuitekeleza adhabu hiyo hadi pale alipoadhibiwa na jini ndipo anaamua kuitekeleza kwa shingo upande. Adili amewakilisha kilele cha uadilifu na upendo ambacho Shaaban Robert anataka wazazi wote wawafundishe watoto wao. Katika kazi hii pia mtunzi amejitokeza wazi kuonesha faida za utu ambao unatokana na nguzo ya imani ya dini maridhawa.

Analiwasilisha wazo hili kwa kutumia kitushi ambacho kinatuonesha jinsi jamii ya watu waliokataa kufuata misingi ya dini elekezi ilivyogeuka kuwa mawe. Aliyesalia katika mji huo ni Mwelekevu pekee ambaye alikubali kuyafuata maelezo na misingi ya dini elekezi na kuachana na dini ya kuabudu mizimu. Mambo hayo yote mazito kama vile umuhimu wa dini, upendo, ukarimu na uongozi bora yamewasilishwa katika kazi hii kwa kutumia uhalisiajabu.

4.5 Vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze

Mada ya utafiti huu imehusu: *Kuchunguza uhalisiajabu na Dhamira katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze*. Utafiti huu umeongozwa na malengo mahsusi mawili yanayokwenda sambamba na maswali mawili ya utafiti. Lengo mahsusi la kwanza lilikuwani: Kubainisha vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.* Lengo hilo limewiana na swali la kwanza la utafiti huu lisemalo: Ni vipengele vipi vya uhalisiajabu vilivyobainishwa katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze?* Kwa kuzingatia lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu, uwasilishaji na uchambuzi wa data umefanyika kikamilifu ukihusishwa na nadharia ya Uhalisiajabu kama ifuatavyo:

4.5.1 Vipengele vya Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kusadikika

Lengo mahsusi la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni Kubainisha vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.* Lengo hilo limekwenda sambamba na swali la kwanza la utafiti huu lisemalo: Ni vipengele vipi vya uhalisiajabu vilivyobainishwa katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze?* Ili kufanikisha lengo na kujibu swali hilo, mtafiti aliweza kuchambua kwa kina

vipengele hivyo vya uhalisiajabu na kuanza na riwaya ya *Kusadikika* pamoja na kuhusisha na nadharia ya uhalisiajabu kama ifuatavyo:

4.5.1.1 Utatizaji wa Wakati

Data zimeonesha kwamba msanii ametumia kipengele cha utatatizaji wa wakati kuwa ni kipengele cha Uhalisiajabu. Katika riwaya ya *Kusadikika* mwandishi ameonesha namna muhusika Majivuno kwa muda wa miaka kumi iliyopita alivyowahi kusikia mnong`ono kuhusu habari za Karama. Majivuno akiwa ndani ya mahakama anaeleza hivi:

> Jalali mfalme na madiwani wakubwa wa baraza nataka kuweka mbele yenu mashtaka ya serikali ya Kusadikika mbele, juu ya Karama, raia mmoja anaelindwa na ulinzi wa mfalme, lakini si muaminifu, anafaidi haki na mapendeleo ya utawala huu, lakini hana shukurani… miaka kumi iliopita tangu mnong'ono wa kwanza ulipofika katika sikio langu…alisema kuwa mshtakiwa alidai kuwa hukumu chache sana zilikuwa za haki… Baada ya usemi wa waziri, baadhi ya watu wachache waliokuja barazani kusikiliza kesi hii walimsikitikia mshtakiwa lakini wengi walikuwa wakinong'onezana kuwa msiba wa kujitakia hauna kilio (uk. 1 - 7).

Katika nukuu hiii msanii ametusawiria namna waziri Majivuno alivyofikisha mashitaka mbele ya baraza ya Kusadikika. Ili kuchagiza kile anachokizungumzia mbele ya Wasadikika ameutatiza wakati kwa lengo la kuionesha hadhira kuwa haipaswi kuliachia suala linalofanywa na Karama kwa sababu ni suala la muda mrefu.

Uhalisiajabu, umetumiwa na msanii ili kuonesha namna tabaka la juu linavyopindisha sheria. Utatizaji wa wakati ni moja kati ya vipengele vya uhalisiajabu kama asemavyo Wamitila (2013), kwamba katika kazi za uhalisiajabu

wakati huwa hausongi mbele. Hivyo muda wa miaka kumi alioutaja Waziri Majivuno ulionekana hauendi. Nadharia ya uhalisia ajabu imetumika ili kuakisi ukubwa wa tatizo na urefu wa muda uliotumika na kwamba swali la muda mrefu kama huu lazima lkomeshwe kwa hatua kali.

4.5.1.2 Masimulizi ya Kihalisiajabu

Vutagwa (2013), anamnukuu Wamitila (2008), akieleza kuwa riwaya za kihalisiajabu hazina mipaka wazi ya mawanda ya kisimulizi. Huweza kufuata matukio ya ulimwengu wa kidhanifu ama ulimwengu wa njozi ambapo matukio hayo hufuata kanuni zile zile za ulimwengu wa kihalisia. Data zimeonesha kuwa Shaaban Robert ametumia kipengele hiki cha kimasimulizi ndani ya riwanya ya *Kusadikika* kama kipengele cha Uhalisiajabu. Hali hii inajidhihirisha katika riwaya ya *Kusadikika.*Mwandishi amesimulia namna wajumbe sita walivyofanya safari kutoka Kusadikika na kwenda nchi jirani. Kwa mfano mtafiti ameeleza namna Amini, mjumbe wa ardhini alivyosafiri kwa kutumia ndege aina ya Mangera kutoka Kusadikika hadi ardhini na wakati wa kurudi, alisafirikwa kutumia ndege Mangera . Mwandishi anasema:

> “Aminialishuka katika Ardhi kwa msaada uliopatikana kwa hila kwa Mangera,Ndege wakubwa kabisa walishao katika Ardhi lakini walalao Kusadikika. Wakati wa kuenda chini Amini alijifunga bila ya kujulikana juu ya paja la Mangera aliyekuwa amelala fofofo usiku kulipokucha ndege huyo aliamka akaruka mpaka chini. Alitua ziwani. Nusu ya mapaja yakeilikuwa majini. Kwa hivi Amini alijifungua, akaogelea bila ya kuonekana mpaka ufukweni”. (uk.46).

Kwa kurejelea nadharia ya Uhalisiajabu mtafiti ameona kuwa masimulizi ya safari za wajumbe sita katika nchi ya Kusadikika yanalandana na msingi wa nadharia ya

Uhalisiajabu unaoona kuwa katika kazi za kihalisiajabu mipaka ya kimaeneo huwa inavunjwa vunjwa. Katika hadithi hii mtafiti ameona namna mipaka kati ya duniani na mbinguni inavyovunjwa kiasi ya kwamba msomi anashindwa kuelewa mpaka uliopo katika mandhari hii.Pia uhalisiajabu anaouona mtafiti ni matumizi ya masimulizi ya visasili kama wasemavyo Njogu na Wafula (2007), kwamba uhalisiajabu kwa kiasi kikubwa hujikita katika hadithi za visasili. Vile vile matumizi ya ndege Mangera ni moja kati ya matumizi ya uhalisiajabu kama mtafiti alivyoeleza kwamba katika kazi za kihalisiajabu kunakuwa na matumizi ya wahusika wadudu, wanyama na ndege.

4.5.1.3 Usawiri wa Wahusika, Utambulisho na Mwanda wa Kihusika

Katika riwaya ya *Kusadikika* wahusika kadhaa wamesawiriwa wakiwa na sifa za kihalisiajabu. Kwa mfano, mhusika Sapa na Salihi wamechorwa na msanii wakiwa wahusika wa kiuhalisiajabu. Mwandishi amesimulia kwamba Sapa alipata upofu kutokana na wivu na choyo dhidi ya Salihi. Katika kisa hicho mtafiti ameeleza kwamba Salihi alikuwa na sifa ya kuomba chochote kwa Mungu na papo hapo dua yake ilikuwa inakubaliwa. Hivyo alikuwa anapata kile alichokiomba. Sapa alipoona hivyo aliingiwa na choyo na wivu na kumwambia Salihi kwamba ameota ndoto, tangu sasa iwapo Salihi ataomba dua na kutogawana sawa sawa kile atakachokiomba kati ya Sapa na Salihi dua yake haitokubaliwa kabisa. Sapa alimueleza mpango huo Salihi. Bila tatizo lolote Salihi alikubaliana na mawazo hayo. Ili kupata mashiko madhubuti tuliandikiana mbele ya Kadhi. Mara tu baada ya makubalianao hayo, Salihi aliinua mikono juu na kuomba dua wawe vipofu kwa sababu hapendi kuyaona

maasi na dhulma zinazotendeka duniani. Papo hapo wote wawili wakawa vipofu. Kisa hiki kinasimuliwa hivi:

> "… Mabwana nyinyi ni kina nani, na asili ya upofu wenu ni nini? Kipofu wa pili akajibu Bwana wangu mwema, mimi naitwa Sapa na mwenzangu ni Salihi. Salihi haombi neno akalikosa.... kwa sababu hii tuliafikiana kushirikiana kila kitu atakachokiomba tukaandikiana hati mbele ya kadhi. Hati ya Mkataba wetu ulipokwisha andikwa nilifurahi sana kuwa shauri langu limefaulu, lakini pale pale mwenzangu aliinua mikono yake juu akaomba upofu, na kabla sijatanabahi, sisi sote wawili tukawa vipofu…" (uk. 29-30).

Katika kisa hiki mtafiti ameona namna Sapa na Salihi walivyosawiriwa kuwa mhusika wa kiuhalisiajabu kutokana na wahusika hawa namna wanavyopata upofu. Maajabu yanayotokea hapa ni kwamba katika uhalisia watu hawakubali kuomba upofu. Hivyo mhusika huyu amesawiriwa kuonesha athari za wivu na choyo.

Vile vile, wajumbe sita wa Kusadikika wamesawiriwa kiuhalisiajabu. Katika riwaya hii tunaelezwa namna wajumbe hawa walivyopata idhara na kutiwa kifungoni mmoja baada ya mwengine. Hata hivyo, kadri ambavyo alihitajika mjumbe mwengine walikuwa wanaendelea kujitokeza bila kujali kile kilichowakuta watangulizi wao (uk. 28).

Maajabu yanayojitokeza kupitia wahusika hawa ni kwamba walikuwa hawaogopi wala hawarudi nyuma kutokana na kile kinachotokea katika nchi ya Kusadikika. Wahusika hawa walilenga kuisaidia Kusadikika ili kuona kuwa nchi hiyo imepata maendeleo. Huu ni ujasiri wa aina yake katika kufanya ukombozi. Kama asemavyo Salim (2015), kwamba ili kuleta ukombozi wa aina yoyote ile lazima watu wawe

wajasiri na kujitoa mhanga. Leo hii jamii nyingi zinashindwa kuleta ukombozi kwa sababu watu si wajasiri.

Vile vile, Waziri Majivuno amesawiriwa kuwa ni mhusika wa uhalisiajabu. Majivuno aliamini kwamba kidole chake kidogo cha ncha kina akili kuliko Wasadikika wote. tabia hii ya kujifadhilisha imemfanya awe na majivuno na hata kuitwa jina la Majivuno. Pia, aliamini kuwawatu wasio na mvi huwa ni dalili ya ujingamtupu (uk. 8-11). Majivuno ni mhusika anayetuibulia maajabu. Maneno yake ya kujivuna yanatuonesha maajabu ya mtu kama yeye ambaye ni kiongozi lakini aliamini kwamba mvi ndio hekima kwa mwanadamu na mtu asiye na mvi ni dalili ya ujinga mtupu. Pia, mhusika huyu anaamini kwamba kila kitu anakitambua yeye. Wasadikika wote hawana akili kama alizonazo. Huyu ni mhusika ambaye amekiuka uhalisia wa kijamii.

Pia, Karama ni mhusika wa uhalisiajabu. Karama amewafanya Wasadikika wote wamuajabie kutokana na kitendo chake cha ujasiri cha kuanzisha elimu ya uanasheria katika Kusadikika jambo ambalo lilikuwa ni kosa la jinai katika nchi hiyo. Mtafiti ameeleza kwamba Karama amekirimiwa ulimi wa ufasaha, ubongo wa hekima na moyo wa ushujaa. Kutokana na vipawa hivyo, anafanikiwa kujiokoa yeye mwenyewe na kuwaokowa wajumbe wengine sita. Msanii anatueleza kwa kusema:

> "…Twaona kwamba mshitakiwa hana hatia, ila alikuwa akitafuta njia yakuisaidia sheria ya Kusadikika kwa njia ngeni. Mfalme alisema,"Taibu, hiyo ni hukumu njema… zaidi ya hayo, natoa amri kuwa watu sita waliotajwa katika hukumu hii – Burhani, Fadhil, Kabuli, Auni, Ridhaa na Amini – wafunguliwe mara moja. Inasikitisha sana kuwa dhuluma juu ya watu hawa hazikutengenezwa mpaka leo…" (uk. 50-51).

Katika nukuu hii, mtafiti amebaini namna Karama alivyokuwa na uwezo wa maajabu. Uwezo huu umewafanya Wasadikika kumshangaa. Wengi walimuajabia kutokana na kutaka kuikomboa jamii yake na dhulma na ukandamizaji uliokuwa ukifanywa na watawala. Bila ya kujali hatari iliyomkabili kutoka kwa tabaka tawala.

Vile vile, uhalisiajabu umejitokeza kwa mhusika Mfalme Jeta.Mwandishi ameeleza kuwa taifa hili lilikuwa ni taifa lenye watu walafi kabisa. Kwa Majuju kila kitu kigumu kilikuwa laini. Muhusika Kabuli alipopelekwa mbele ya Mfalme Jeta mto mrefu na mpana ulikuwa ukitiririka katika kinywa chake kikubwa sana. Hakuna tone la maji lililokwepa kuingia katika kinywa cha Mfalme Jeta. Miamba, chuma, magogo na tani milioni nyingi za samaki zilikuwa zikitiririka katika kinywa chake lakini kila dakika moja alikuwa analia “kiu” “njaa.” (uk. 25-26).

Uhalisiajabu mwengine umejitokeza kupitia mhusika Mfalme Jeta. Kuhusu mfalme huyu msanii ameeleza kuwa Kabuli alipopelekwa mbele ya Jeta alitaka kumla hata Kabuli. Hili ni tukio lakuajabisha kutokana na kitendo cha binadamu kutaka kumla binadamu mwengine. Hali hii ilipelekea kuzuka kwa mapambano kati ya majeshi ya Mfalme Jeta na raia. Kabuli sasa akawa katika hatari ya kuangamia. Mapambano hayo yaliendelea hadi kila kitu kilichokuwa na uhai kikaangamizwa, akabakia Kabuli tu (uk. 26).

Mtafiti anaporejelea nadharia ya uhalisiajabu ameona namna wahusika hawa (kama Sapa na Salihi, Karama na Majivuno na wajumbe sita) wameonesha namna walivyokwenda sambamba na nadharia hii kutokana na kuchorwa wakiwa na sifa ambazo zimekiuka uhalisia wa kijamii. Ikiwa ni moja wapo kati ya msingi wa

nadharia hiyo inavyoeleza kuwa kazi za kihalisiajabu mara nyingi zinaibua matendo ya kuajabisha. Hivyo wahusika hawa wameonyesha matendo yaliyokusanya usanii wa kazi za kihalisiajabu.

4.5.1.4 Motifu za Safari za Kihalisiajabu

Uchambuzi huu wa data zilizokusanywa katika riwaya ya *Kusadikika* umeonesha kwamba riwaya ya *Kusadikika* imetumia motifu za safari za kihalisiajabu. Mathalani, mwandishi anaisanii kazi yake kwa simulizi la motifu za safari za wajumbe sita yaani; Burhani: Mjumbe wa Kaskazini, Fadhili: Mjumbe aliyetalii Mashariki, Kabuli: Mjumbe wa nchi za Kusini, Auni: Mjumbe wa Magharibi, Ridhaa: Mjumbe wa Mbinguni na Amini: Mjumbe wa Ardhini. Uchambuzi wa data umeonesha kwamba safari hizi zina sifa za kihalisiajabu. Kwa mfano,Amini ni mjumbe aliyesafiri kutoka Kusadikika hadi Aridhini kwa kutumia ndege aina ya Mangera. Ndege wakubwa kabisa walishao Aridhini na walalao *Kusadikika*. Msanii ametusimulia safari hii kwa kusema:

> “Amini alishuka katika aridhi kwa msaada uliopatikana kwa hila kwa Mangera, ndege wakubwa kabisa walishao katika Ardhi lakini walalao Kusadikika. Wakati wa kuenda chini Amini alijifunga bila ya kujuilikana juu ya paja la Mangera aliyekuwa amelala fofofo usiku. Kulipokucha ndege huyo aliamka akaruka mpaka chini. Alitua ziwani nusu ya mapaja yake yalikuwa majini. Kwa hivyo, Amini alijifungua akaogelea bila ya kuonekana mpaka ufukweni….” (uk. 40).

Amini ni mjumbe wa aridhini. Alisafiri kutoka nchi ya Kusadikika hadi Aridhini ili kutalii mambo mbali mbali ambayo yangeweza kuisaidia Kusadikika kupiga hatua ya maendeleo. Aminibaada kurudi safari yake alieleza kuwa mamlaka za aridhini zimepata maendeleo makubwa. Mandhari hii inatuibulia maajabu. Hii ni kwa sababu

katika maisha ya uhalisia hakuna masimulizi ambayo ameyaelezea Amini yaliyowahi kupita katika hisia za binadamu za maisha ya Aridhini.

Safari hii imebeba maajabu kutokana na kukiuka uhalisia wa kijamii. Watu huwa hawasafiri kwa kutumia ndege kama alivyofanya Amini. Kwa mantiki hiyo kuna uhalisiaajabu na hivyo kufanya safari hii kuwa ni ya kufikirika tu. Wazo hili linathibitishwa na Wamitila (2013), anavyoeleza kwamba sifa na motifu za kisafari zinazojitokeza katika riwaya ya *Adili na Nduguze*, *Kusadikika* na *Kufikirika* zinahusishwa na Uhalisiajabu.

Kwa kurejelea nadharia ya Uhalisiajabu tumeona kuwa matukio ya safari zinazoendwa na wajumbe wa Kusadikika zimelandana na nadharia ya Uhalisiajabu. Kama inavyoelezwa kuwa katika kazi za kihalisiajabu mambo yasiyokuwa ya kawaida huchukuliwa kama ya kawaida katika visa vya kihalisiajabu. Safari zinazoongozwa na wanyama kama vile ndege Mangera imeonekana ya kawaida katika kazi za kihalisiajabu lakini imekiuka uhalisia wa kijamii. Pia, mtafiti amebaini kuwa kazi zenyekujikita katika mwelekeo wa nadharia ya uhalisiajabu hutumia wanyama na ndege kama sehemu ya usanii. Hiki ndicho alchokigundua ndani ya riwaya ya *Kusadikika.*

4.5.1.5 Mandhari za Kihalisiajabu

Madumulla (2011), anaeleza kwamba mandhari katika kazi za fasihi ni mahala ambapo tukio linatendeka. Mandhari katika kazi za fasihi huweza kuwa halisi au ya kidhahania. Utafiti huuu umegundua kuwa riwaya ya *Kusadikika* imetumia mandhari ya kufikirika ambayo inaelea juu ya anga. Kwa mfano, mwandish ameeleza kuwa:

> “Kusadikika ni nchi ambayo kuwako kwake ni kwa kufikirika kwa mawazo tu (uk. viii).

Katika mfano huu tumeelezwa kwamba, mandhari ya *Kusadikika* ni ya kidhahania ambayo inaibua uhalisiajabu. Msanii ameichora nchi ya Kusadikika ili kuwakilisha nchi yoyote ya Kiafrika yenye sifa kama vile uongozi mbaya, ukosefu wa huduma za kijamii, utabaka, vita vya wenyewe kwa wenyewe na maovu mengine. Msanii ametusimulia mandhari ya nchi ya Kusadkika kwa kusema kuwa, nchi hiyo imezungukwa na mipaka sita. Kimsingi msanii ametuchorea uhalisiajabu wa aina fulani. Kuhusu nchi ya Kusadikika msanii ameeleza hivi:

> Nchi hiyo iko katika mipaka sita. Kwa upande wa Kaskazini imepakana na upepo wa kaskazi, na kwa upande wa Kusini imepakana na upepo wa kusi. Mashariki imepakana na matlai na Magharibi mpaka wake ni upepo wa umande. Kwa kuwa nchi wenyewe inaelea katika hewa kama wingu zaidi ya kupakana na pepo nne hizo, ina mipaka mengine miwili yenyewe ni hii. Kwa juu nchi hiyo imepakana na mbingu na kwa chini imepakana na Ardhi (uk. 1).

Kusawiriwa kwa mandhari ya Kusadikika kunaibua maajabu. Kwanza hakuna nchi ambayo inaelea juu ya anga katika ulimwengu wa uhalisia. Pili, Kusadikika ina mipaka sita kinyume na nchi nyengine za uhalisia ambazo mipaka yake huwa ni minne tu badala ya sita. Vile vile, mtafiti amebaini kwamba, kuna matumizi ya mandhari ya mto ambayo maji yake yanakwenda kwa kasi kubwa. Matumizi ya mito na safari kama hizo, kama ilivyosemwa hapo awali, ni miongoni mwa mandhari yaliyochotwa kutoka visasili ambavyo hatimae huibua sifa za uhalisiajabu. Mandhari haya yamesimuliwa hivi:

> “Kutahamaki aliteleza akatumbukia katika mkondo wa mto uliokuwa ukikimbia kwa nguvu na upesi kama umeme. Miongoni mwa vitu vingi vilivyokuwa vikielea katika mkondo huo lilikuwamo gogo moja la wastani. Auni alishika gogo hilo kwa mikono yake miwili… Alijibiwa `Hapa ni Iktisadi, nchi ya utajiri na faraja kwa kila mtu. Fumbua macho yako utazame, ulitumbukia katika maangamizi ya matumizi, yaani mto mmoja kati ya mito ya uharibifu…” (uk. 31-32).

Mtafiti kwa kurejelea nadharia ya Uhalisiajabu, amebaini kuwa moja kati ya msingi wa nadharia hiyo ni matumizi ya mito, maziwa, bahari nakadhalika. Kwa mantiki hiyo matumizi ya mandhari haya ya mito ni upenyezi unaofanywa na msanii ili kuibua sanaa yenye sifa za kihalisiajabu katika ulimwengu wa uhalisia.

Kwa hakika vipengele vya uhalisiajabu vimekuwa na umuhimu mkubwa katika kutimiza lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu kwa mnasaba wa riwaya teule ya *Kusadikika.* Kwa kurejelea nadharia ya uhalisiajabu vipengele vya uhalisiajabu ambavyo mtafiti amevibaini na kuvichambua ni pamoja na Utatizaji wa wakati, masimulizi ya kihalisiajabu, usawiri wa wahusika, utambulisho na mwanda wa kihusika, motifu za safari za kihalisiajabu, na mandhari za kihalisiajabu.

Jadweli 01: Muhtasari wa Vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya Kusadikika

Nambari	**Vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya Kusadikika**
01	Utatizaji wa wakati
02	Masimulizi ya kiuhalisiajabu
03	Usawiri wa wahusika, Utambulisho na Mwanda wa kihusika
04	Motifu za safari za kiuhalisiajabu
05	Mandhari za Kiuhalisiajabu

Chanzo: Data kutoka riwaya ya *Kusadikika*. Septemba, 2018

4.5.2 Vipengele vya Uhalisiajabu katika Riwaya ya Adili na Nduguze

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni;Kubainisha vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*.Lengo hili liliongozwa na swali la kwanza la utafiti huu lisemalo “Ni vipengele vipi vya uhalisiajabu vimebainishwa katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*?Ili kufikia lengo hilo na hatimae kulijibu swali hilo, mtafiti amebaini na kufanya uchambuzi timilifu wa vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Uchambuzi wa vipengele hivyo umeongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu kama ifuatavyo:

4.5.2.1 Mtindo wa Udenguzi na Uumbuzi

Wamitila (2013), anasema kazi za kihalisiajabu huwa ni kazi umbuzi na mwelemeo wake wa kuwa kila kitu katika umoja huchochea ukinzani wa umoja wa miundo ya kitamaduni, kisiasa, hali ambayo inawavutia sana waandishi wa fasihi ya Baadaukoloni na hata waandishi wa kike.Riwaya ya *Adili na Nduguze*imetumia vipengele vya udenguzi ikiwa ni kipengele kimojawapo cha uhalisiajabu. Kwa mfano, moja kati ya mtindo wa udenguzi na uumbuziambao umejitokeza ni kupitia hadithi ya mfalme Rai. Hadithi hiyo, inaeleza kwamba Mfalme Rai alikuwa ni Mfalme wa aina ya pekee, aliyepata hadhi ya kutawala watu, wanyama na majini kwa uadilifu mkubwa na kwa sababu hiyo alikuwa akipendwa na kila kiumbe. Msanii analisimulia hilo kwa kusema:

> “Rai, mfalme wa Ughaibuni, alikuwa mfalme wa aina ya pekee duniani… tabia yake ilijigawa katika theluthi tatu mbali mbali kama rangi ya ngozi ya pundamilia…kwa theluthi ya kwanza alikuwa msuluhivu akapendwa na watu. kwa theluthi ya pili alifanana na Daudi akaheshimiwa kama mtunzaji mkuu wa wanyama na kwa theluthi ya tatu alikuwa kama Suleiman akatiiwa na majini” (uk. 01) .

Nukuu la hapo juu linaonesha kwamba masimulizi hayo ni mfano wa udenguzi wa uhalisiajabu kutokana na ukweli kwamba Mfalme Rai amekiuka mipaka ya kiuhalisi kutokana na sifa yake ya kutawala majini na hata wanyama jambo ambalo linakiuka uhalisi wa kijamii. Kama asemavyo Wamitila (2013), kwamba kazi za kihalisiajabu huwa kazi umbuzi na muelemeo wake wa kila kitu kuwa katika umoja huwa inaibua ukinzani wa kiutamaduni. Katika riwaya hii, sauti ya msimulizi imelenga kudengua mawazo ya utawala uliopo ambao umekuwa ukiwagawa wanajamii katika makundi kadhaa bila ya kujali haki na usawa. Kwa hivyo anautaka utawala utawale kwa misingi ya haki na usawa ili kujenga upendo miongoni mwa raia wake.

Pia, mtafiti aligundua kwamba msanii ametumia udenguzi wakati anapomtumia Adili kama msimulizi wa hadithi ya mfalme Rai, baraza, na manyani. Katika masimulizi hayo, tumepata udenguzi wa kimtindo kutokana na kujichomoza kwa hadithi ndani ya hadithi. Kwa mfano, ndugu wa Adili kugeuzwa manyani, kisa cha Mji wa mawe, kisa cha Adili kutoswa baharini, wokovu wake na kurejeshwa ndugu wa Adili kuwa binadamu tena. Mfano wa hadithi hiyo ilianza kama hivi:

> Sasa kisa baada ya kisa juu ya manyani kilisimuliwa … katika kisa cha kwanza Adili alisema kuwa manyani yale mawili yalikuwa ndugu zake. Baba yao alikuwa mmoja, baba yao aliitwa Faraja. Faraja alikuwa mtoto pacha. Wakati wa kuzaliwa pacha hiyo mtoto mmoja alikufa pakabakia mmoja, huyo aliebaki aliitwa faraja kwa sababu aliwafariji wazazi wake katika msiba wa ndugu zake… Baada ya kuvaa nguo walikaribishwa sebuleni, wakati ule hali yao bado ilikuwa dhaifu sana kwa uchovu na njaa. Chakula kililetwa katika sinia moja ya dhahabu iliyonakishiwa kwa dhahabu na fususi, walitafadhalilishwa kula chakula wakala mpaka wakashiba. Adili aliyageukia manyani akauliza kama yaliosemwa yalitokea au hayakutokea, manyani yaliziba nyuso zao kwa viganja vya mikono yao kwaaibu (uk. 9-13).

Mfano uliopo hapo juu ni udenguzi uliofanywa na msanii ambao umetuibulia maajabu ya ndugu zake Adili kutokana na kuwa walikuwa binadamu na sasa ni manyani. Mtafiti anakubaliana na mawazo haya ya kidenguzi kama Vutagwa (2013), alivyomnukuu Faris (2004), ambae alieleza kuwa waandishi wa uhalisiajabu hutumia kipengele hiki ili kulaani, na kukashifu baadhi ya matendo ya kikoloni. Hii ni kusema kwamba fasihi ya kihalisiajabu huumulika uhalisia wa kimagharibi na hatimae kutumia matini za kihalisiajabu ili kukosoa miundo ya kikoloni na ile ya kiutamaduni yenye mitazamo finyu. Kwa mtazamo huu uhalisiajabu hukiuka misingi ya fasihi iliyozoeleka na kuonesha kuwa kuna mitindo kadhaa ya kazi za fasihi. Hivyo basi, katika simulizi hili msanii ametuonesha namna alivyoudengua mtindo ili kuusawiri uhalisia wa maisha ya kijamii katika wakati wa ukoloni.

Kwa mnasaba wa nadharia ya Uhalisiajabu, mtafitiameona kuwa udenguzi unaojitokeza hapa umelandana na muhimili wa nadharia hii. Mhimili unaosawiriwa hapa ni ule wa matukio ya kihalisiajabu kudenguliwa na hatimae kukiuka uhalisia wa kijamii. Kama tunavyoona kuwa binadamu kwa kawaida huwa hawezi kuwa nyani lakini kutokana na kazi hii ya kisanii Shaaban Robert amekengeusha wahusika hao kutoka binadamu wa kawaida na kuwafanya manyani.

4.5.2.2 Mtindo wa Kihalisiajabu

Madumulla (2011), anasema kwamba mtindo unaweza kuwa ni mchangamano wa mambo mawili, yaani wazo la msanii kwa upande mmoja na jinsi wazo hilo lilivyoelezwa. Mtindo unaweza kuwa ni tabia ya uandishi katika kipindi cha mfumo fulani wa maisha au historia ambayo ulionyesha hali, kanuni taratibu na kadhalika.

Katika riwaya ya *Adili na Nduguze* masimulizi yaliyofanywa na Adili mbele ya mfalme Rai, ili kuelezea kisa cha mgao mwengine wa mali baada ya kufilisika ndugu zake kwa kupotea mali yao baharini yanaingia katika kategoria hii. Mgao uliofanywa kwa mali kugaiwa sehemu tatu sawa sawa, mbele ya kadhi huku akiamini kuwa, umaskini unatengana hatua moja tu na utajiri. Kuhusu hili mwandishi ameeleza:

> Alisema kuwa mali hufidia roho, lakini roho haifidiwi na kitu. Salama ya maisha yao ilikuwa bora kuliko faida iliyopotea. Umaskini unatengana hatua moja tu na utajiri. Siku ya pili Adili alichukuana na ndugu zake kwa kadhi. Alipofika aliomba mali yake igaiwe mafungu matatu sawa sawa…Adili aliyageukia manyani akauliza kama yaliosemwa yalitokea au hayakutokea. Manyani yaliziba nyuso kwa viganja vya mikono yao kwa aibu (uk. 15-16).

Aidha, nukuu iliopo hapo juu ni mfano wa uhalisiajabu. Kwanza, tumepata uhalisiajabu kwa vile Adili kukubali mali yake kugaiwa tena na ndugu zake kwa mara ya pili. Tukio hili linakiuka uhalisi wa kijamii. Pili, kitendo cha manyani kupewa sifa ya kiuhalisia wa binadamu ni mbinu ya kisanii ambayo imekiuka ushabihi kweli na hatimae kuibua maajabu. Msanii anaonesha namna manyani hayo yalivyopata kile wasichokitarajia kutokana na uchoyo. Hali hii ndiyo inayoikumba jamii ambapo choyo kimekuwa kikiwatumbukiza watu katika maangamizi.

Kwa kurejelea nadharia ya Uhalisiajabu mtafiti amegundua kuwa mitindo hii ya visasili vya manyani, tandu na nyoka, Mrithi wa Mji wa Mawe vimelandana na uhalisiajabu kutokana na kukiuka uhalisia wa kijamii.Kipengele hiki kimetumika ili kuipa kazi hii misingi ya fasihi ya Afrika dhidi ya fasihi ya Kimagharibi.

4.5.2.3 Masimulizi ya Kihalisiajabu

Vutagwa (2013), amemnukuu Wamitila (2008), akieleza kuwa riwaya za kihalisiajabu hazina mipaka wazi ya mawanda ya kisimulizi. Huweza kufuata matukio ya ulimwengu wa kidhanifu ama ulimwengu wa njozi ambapo matukio hayo hufuata kanuni zile zile za ulimwengu wa kihalisia. Data zimeonesha kuwa Shaaban Robert ametumia kipengele hiki cha kimasimulizi ndani ya riwaya ya*Adili na Nduguze*kama kipengele cha Uhalisiajabu. Mtafiti amegundua kuwa kuna matumizi ya visasili kadhaa katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ambayo yana sifa za kiuhalisiajabu. Hali hii inajidhihirisha kama ifuatavyo:

Moja ya kisasili ambacho kimejitokeza katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ni kisa kinachoelezea mji uliogeuzwa mawe ambao aliutembelea Adili. Msanii ametueleza kisa cha mji huo kugeuzwa mawe, na watu wake nao kugeuzwa mawe. Tunaelezwa kwamba sababu hasa iliyopelekea mji huo kugeuka mawe ni kutokana na watu wake kuabudu mizimu, pamoja na kukataa ukumbusho pale walipoonywa na Mrefu. Katika kuelezea kisa hicho msanii anasema:

> "… Mfalme ni naibu wa Mungu duniani. Kwa hivyo ufalme ni amana kubwa. Amana hiyo ilitaka uangalifu mkubwa kwa sababu ni dhima bora iliyowekwa mikononi mwa mwanadamu.Wajibu wa kwanza wa Mfalme ni kuwa mwadilifu katika matendo yake…kwa sababu ya maisha ya milele, ibada ya mizimu ilikuwa maangamizi na uimamu wa kabwera ujinga mtupu…kwa laana iliyotamkwa na Mrefu, Miji mengine yote ya dola hii ilighariki, na kila kiumbe kilichokuwa na maisha katika Fahari kiligeuka jiwe …" (uk. 29).

Hali anayoisimulia hapa mwandishi inaibua maajabu. Hali hii haijapata kuwepo ulimwenguni. Salim (2015), anasema kuwa hadithi kama hizi ni mifano ya hadithi za kimapokeo ambazo kwa ujumla huwa zimesheheni matukio ya kiuhalisiajabu. Kama

tunavyoelezwa katika dondoo hili ule uhalisia unakiukwa na kujikita katika uhalisiajabu ambao uko kinyume na urazini wa mwanadamu. Mji unapogeuka mawe ni ishara ya laana kutoka kwa Mungu. Hata hivyo, tukio hili linakuja kutokana na watu kutofuata maelekezo ya kiongozi wao.

Saleh (2015), alipokuwa akifanya uchambuzi wa riwaya ya *Adili na Nduguze* amelielezea tukio la mji uliogeuzwa mawe kama ishara ya kuwataka watu waamini juu ya Mungu mmoja. Hata hivyo, kwa maoni yetu ni kwamba msanii katika taswira hii ya uhalisiajabu ametuonesha namna wakoloni walivyojifanya miungu watu ambao waliwalazimisha Waafrika kutii kila walililolisema vyenginevyo wangepata mateso yasiyo na mfano.

Aidha, katika riwaya ya *Adili na Nduguze* mwandishi amesimulia kisasili kinachohusu ndugu wa Adili kugeuzwa nyani. Kisa hiki kimeonesha kwamba ndugu hao walikuwa binadamu hapo kabla. Hata hivyo ndugu hao waligeuka manyani kutokana na kulaaniwa na jini Huria. Ndugu hawa walilaaniwa kwa sababu ya wivu, chuki, choyo na husuda, ambayo iliwafanya wamtose Adili baharini. Ndugu hawa wametekeleza hali hiyo bila ya kujali utu na msaada wa kila aina ambao walikuwa wakitendewa na Adili. Kisa hiki kimesimuliwa hivi:

> "… Kwa hasira kubwa Huria alinena,"Kama ungalijua hatari ya kumtosa mtu baharini, au ungalikuwa na fikira za msiba, msingalijaribu kumtosa ndugu yenu baharini au mngalikuwa na fikra za msiba, msingalijaribu kumtumbukiza ndugu yenu baharini alipolala…kwa sababu hiyo walikuwa hatarini milele. Walakini alikubali kuwasamehe kwa sharti ya kuwageuza wanyama. Aliwalaani watoke katika umbo la ubinadamu. Mara ile ndugu zake walikuwa Manyani…" (uk. 39 -40).

Matumizi ya kipengele hichi cha masimulizi yanaupenyezi wa uhalisiajabu kutokana na binadamu kugeuzwa nyani jambo ambalo lilipelekea jamii nzima akiwemo Mfalme kuingiwa na wasiwasi. Huu ni uhalisiajabu kwa sababu kisa hiki kimetambaa na kutusimulia namna binadamu walivyogeuka wanyama. Pia, uhalisiajabu katika tukio hili unajidhihirisha pale jini Huria anapojitokeza wazi wazi mbele ya binadamu na kufanya mijadala nao. Kama inavyotambulika kwamba majini hawana sifa ya kukabiliana na binadamu huku wakijadiliana katika mambo mbali mbali.

Kwa kurejelea nadharia ya Uhalisiajabu, mtafiti amebaini kwamba visasili ni miongoni mwa vipengele vya uhalisiajabu, hivyo masimulizi haya yametumika kama ni sehemu ya uhalisiajabu. Ambayo yamethibitisha ukweli kuhusu laana inayotokana na madhara ya ya wivu, chuki, choyo na husuda, ambayo hufanyiana baina ya wanandugu.

4.5.2.4 Usawiri wa Wahusika, Utambulisho na Mwanda wa Kihusika

Katika riwaya ya *Adili na Nduguze*, data zimeonesha kwamba kuna wahusika mbalimbali ambao wamesawiriwa wakiwa na sifa za uhalisiajabu. Wahusika hawa, msanii amewachota kutoka hadithi za kimapokeo ambazo mara nyingi hutumia wahusika wanyama, majini, mizimu, malaika na hata binadamu ambao husawiriwa kwa aina mbalimbali. Wahusika hawa hupewa uwezo wa kufikiri na kutenda mambo kama wafanyavyo wahusika wa kibinadamu. Hata hivyo, uhusika huu hubakia ukiwa ni wa maajabu ambao huwaakisi wanadamu wakawaida. Mawazo haya yanashadidiwa na Wamitila (2013), anaposema kwamba wahusika wa visasili huwa ni wanyama, majini, miungu nakadhalika. Kutokana na visasili kuwa na wahusika

hawa huwa zinaingia katika hadithi zenye sifa za uhalisiajabu. Moja kati ya wahusika wa uhalisiajabu katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ni wahusika manyani. Wahusika hawa walikuwa binadamu na baadae walilaaniwa na jini Huria na kuwa manyani. Baada ya hapo manyani hao waliweza kufahamu kila kitu kama walivyo watu wengine. Kwa mfano, msanii amesema:

> "Manyani yalipomuona mfalme yalifanya ishara mbili. Kwanza yaliinua juu mikono yao kama yaliyokua yakiomba. Pili yalilialia kama yaliyodhulimiwa. Ishara ya kwanza ilionyesha ombi la msaada. Na ile yapili ilionesha mashitaka…" (uk. 09).

Katika dondoo iliotangulia, mtafiti amegundua maajabu ya manyani hao wakiomba na kushtaki mbele ya mfalme. Msanii anapenyeza mawazo ya kihakiki kwa kutufumbulia fumbo ambalo amelifumba. Kipengele hiki cha uhalisiajabu kimempa fursa mtafiti kupata kuamini kwamba manyani hao wanawakilisha tabaka la chini katika jamii. Tabaka ambalo limekuwa likikandamizwa na kuonewa na watu wa tabaka la juu. Tabaka hili linapoteleza na kufanya makosa huangukia katika maangamizo makubwa ikiwa ni pamoja na kuingizwa chuo cha mafunzo ambako huko huishi kwa maisha ya dhiki pamoja na adhabu kadhaa ikiwemo kipigo kama walivyokuwa wakifanywa manyani haya.Katika kushadidia umuhimu wa ukweli katika maisha ya kila siku, msanii anawatumia manyani wanajitokeza wakati msanii anaposimulia habari ya manyani. Ili kuonesha kwamba kila siku ukweli unaushinda uongo msanii anamtumia Adili akisimulia mkasa wake mbele ya manyani hao. Iwapo anayoyasema ni uongo manyani yanapaswa kuguna na iwapo ni kweli basi manyani yanapaswa kuziba nyuso zao kwa kutumia viganja vyao. Tunasimuliwa tukio hili hivi:

> "… Adili alijibu kuwa waungwana hawasemi uongo. Atasema kweli, na manyani yatakuwa mashahidi. Maneno yake yakiwa uongo, yatakanushwa na manyani kwa mguno, lakini yakiwa kweli, manyani yatayathibitsha kwa kuziba nyuso kwa viganja vya mikono yao…" (uk. 9).

Kitendo cha manyani kuthibitisha maneno ya Adili kwa kuziba nyuso zao kwa viganja ni tukio linaloajabisha. Wanyama kama vile nyani hawana tabia ya kuthibitisha matendo kwa kuamuriwa na mwanadamu. Lengo la kutumia wahusika wa aina hii ni kuusawiri ulimwengu wa kiuhalisia kwa mtindo mpya wa kifasihi. Hapa mtafiti anaungana na mawazo ya Wamitila (2013), ambaye anasema wahusika wa fasihi simulizi kama vile wanyama, majini husawiriwa kwa mitindo ya uhalisiajabu ili kusawiri maisha ya wanajamii. Aidha utumiaji wa wahusika manyani umelandana na nadharia ya Uhalisiajabu ambayo moja kati ya msingi wa nadharia hii ni kutumia wanyama katika kusawiri maisha ya wanajamii. Hivyo basi, tukio hili limetumika ili kuonesha namna ukweli ulivyokuwa ni ngao ya mtu popote pale na wakati wowote na kila siku ukweli huwa uko juu dhidi ya uongo. Ndio maana Waswahili husema kuwa "ukweli ukidhihiri uongo hujitenga."

Vile vile, manyani wametumika kuibua maajabu katika safari ya Adili na Ikibali kuelekea Ughaibu kwa mfalme Rai. Katika safari hii mtafiti ameleza kisa cha wahusika manyani ambao walikuwa wamepanda farasi. Katika safari hii manyani walikabidhiwa farasi kila mmoja wake. Msanii analisimulia tukio hili kwa kusema:

> "…Adili alijiandaa kwa safari ya kuitikia wito wa Mfalme. Farasi watatu walitandikwa matandiko mazuri. Yeye alipanda farasi mmoja na mmoja kwa kila nyani. Ikibali alipanda farasi wake mwenyewe… vinywa vya umati wa watu vilikuwa wazi kwa kivumo cha lo salala. Wakati umefika wa mawe kusema, miti kujibu na wanyama kuwa watu…" (uk. 13).

Kwa sababu tukio hili lilikuwa na sifa za uhalisiajabu watu wote waliajabia na kuamini kuwa sasa ni wakati wa mabadiliko. Katika maisha ya uhalisia mnyama kama vile nyani hana nafasi ya kumtumikisha mnyama mwengine ili kukidhi haja zake za usafiri kama walivyofanya manyani hawa.

Katika kisa chengine ndani ya riwaya ya *Adili na Nduguze* kuna matumizi ya mhusika Tandu na Nyoka. Data zinatuonesha kwamba wahusika hawa walikuwa ni wahusika wa kiuhalisiajabu kutokana na vile walikuwa si tandu wala nyoka katika maumbile yao ya kawaida. Mwandishi anaeleza kuwa tandu alikuwa ni jini na nyoka pia alikuwa ni jini. Adili aligundua siri hii baada ya kumhurumia tandu aliyekuwa akifukuzwa na nyoka na hivyo kuamua kumsaidia kwa kumlenga jiwe nyoka huyo ambaye alikufa baada ya kusadifu kumpiga jiwe la kichwa. Hapo hapo Adili anaona maajabu baada ya tandu yule kujigeuza mtu na hatimae kupasua ardhi kwa kuioteza kidole na kuingia ndani yake. Msaniiametusimulia tukio hili kwa kusema:

> “Adili alipanda juu ya jabali. Huko aliona tandu linakimbia. Rangi yake inapendeza sana. Iling’ara kama kioo.Nyuma yake lilifuatwa mbio na nyoka anayetisha alilibana jiweni.Tandu lilitoa mlio wakusikitisha. Kwa mlio ule Adili alijua tandu lilikuwa hatarini” (uk 18).

Wakati akifanya uchambuzi wa riwaya ya *Adili na Nduguze*, Salim (2015) anaeleza tandu anawakilisha nchi au tabaka linalokandamizwa na nyoka anawakilisha nchi tajiri ulimwenguni ambazo hutumia nguvu zake ili kukandamiza na kuonea nchi changa. Katika riwaya ya *Adili na Nduguze* msanii anaisawiri kiishara hali hii kwa kusema:

> “Alighadhibika akatisha kumuonesha Huria uwezo wake. Na tangu alipotisha hivyo hakumpa nafasi hata ya uzi kupenya tundu la sindano…siku aliyokuwa tandu yeye alikuwa nyoka akamfukuza. Alipochoka kukimbia akamkamata” (uk. 36).

Mhusika mwengine aliyetumika kiuhalisiajabu katika riwaya ya *Adili na Nduguze* ni Mfalme Rai wa Ughaibuni. Tunasimuliwa kwamba Mfalme huyo alikuwa anatiiwa na binadamu, wanyama na majini. Vile vile, nchi yake ilikuwa na neema kubwa kutokana na kuongoza kwa uadilifu. Inaelezwa kwamba Rai alikuwa anathamini watu wa matabaka yote. Jambo hili lilipelekea watu wake wote kumpenda. Kuhusu Mfalme Rai tumeelezwa:

> “Tabia yake ilijigawa katika theluthi tatu mbali mbali kama ngozi ya pundamilia kwa theluthi ya kwanza alikuwa msulihifu akipendwa na watu, kwa theluthi ya pili alifanana na Daudi akaheshimiwa kama mtunzaji mkuu wa wanyama na kwa theluthi ya tatu alikuwa kama Suleman akitiiwa na majini …” (uk.01).

Huyu ni mfalme anaeajabisha. Kitendo hiki kinakengeusha msemo wa Waswahili unaosema kwamba “hakuna anayependwa na kila mtu.” Lakini hapa imetudhihirikia kwamba, watu, majini na hata wanyama wote wanampenda Mfalme Rai.

Pia, Mrefu ni mhusika wa uhalisiajabu katika riwaya ya *Adili na Nduguze*. Mhusika huyu ana nguvu na uwezo wa kimiujiza wa kuvuka bahari zote kwa miguu, kukausha samaki kwa jua na kubwa zaidi ule uwezo wa kuiangamiza miji kwa laana yake. Kuhusu sifa za mhusika Mrefu tunaelezwa hivi:

> “Mrefu alikuwa muujiza katika viumbe. Alikuwa na miguu mikubwa na mapaja manene, kiuno cha utambo na kifua kipana, na shingo yake ndefu ilichukua kichwa kikubwa. Mabega yake ya mraba yalininginiza chini mikono iliyokua na nguvu kama manjanika. Kwa kimo cha kukithiri alitembea baharini bila ya kuguswa na maji magotini…” (uk. 27).

Maelezo ya dondoo hili yametuibulia uhalisiajabu kutokana na kueleza ushujaa ambao hawi nao mtu wa kawaida katika ulimwengu wa kihalisia. Sifa kama hizi zinalingana na nadharia ya Uhalisiajabu ambapo moja kati ya msingi wa nadharia hii ni kuwa na wahusika wenye kuibua matukio ya ajabu yaani yasiyokuwa yakawaida katika ulimwengu wa uhalisia. Mawazo haya yanasimuliwa pia na msanii kwa kusema:

> "Mrefu aliyekuwa hasogeleki wala hashikiki. Uwezo usio hadhari ni kilio kibaya sana. Siku ile ilikuwa tisho na msiba, ole na maangamizi makubwa. Kwa laana iliyotamkwa na Mrefu miji mengine yote ya dola hii ilighariki (uk. 26).

Mhusika huyu ameakisi ukoloni katika bara la Afrika. Ukoloni ambao uliweza kufanya chochote kutokana na nguvu za kijeshi, nguvu za kiuchumi na nguvu za vyombo vya usafiri. Kutokana na hali hii imepelekea Bara la Afrika kubakia likiwa linakandamizwa na kunyonywa na wakoloni.

Kwa msaada wa nadharia ya Uhahlisiajabu, mtafiti ameona namna wahusika hawa wanavyoshabihiana na nadharia hii kutokana na kusawiriwa wakiwa na sifa zilizokiuka uhalisia wa kijamii. Kama moja kati ya msingi wa nadharia hiyo unavyoeleza kwamba kazi za kihalisiajabu huwa zinaibua matendo ya maajabu. Hivyo matendo ya ajabu yanayotendwa na wahusika hawa yamechota usanii wa kazi za kihalisiajabu.

4.5.2.5 Motifu za Safari za Kihalisiajabu

Data zilizokusanywa na kuchambuliwa katika riwaya teule zimeonesha kwamba riwaya hizi zimesheheni safari za kihalisiajabu. Katika riwaya ya *Adili na Nduguze,*

data zimeonesha kuna motifu za safari za kihalisiajabu. Kwa mfano, safari ya Ikibali ya kutoka Ughaibu kwenda Janibu, ambayo ilitumia farasi kama njia ya usafiri, ili kwenda kuchunguza hesabu ya kodi ilyokusanywa na Adili, na sababu ya kuchelewa.

> "Uteuzi wake ulikuwa na maana, kwa sababu, ukamilifu wa mtu duniani ni tabia njema mbali ya sifa nyengine, kila mtu bora alitakiwa kuonyesha ubora wake…Siku ya pili saa moja asubuhi, Ikibali alitakiwa kwenda Janibu. Mwendo wa saa sita kwa farasi ulikuwa kati ya Ughaibu na Janibu. Adhuhuri ilipokaribia Ikibali alikuwa amefika katika viunga vya mji aliokusudia … (uk. 4).

Safari inayoelezwa katika nukuu ya hapo juu ni safari inayoibua maajabu. Hii ni kwa sababu si kawaida ya viongozi wa dola kusafiri kwa kutumia wanyama kama vile punda na farasi kutoka nchi moja na nyengine. Kama anavyosema Salim (2015), kwamba safari nyingi za visasili vya fasihi simulizi ambazo zina sifa za uhalisiajabu hazitumii ndege za angani, gari, gari moshi na vyombo vyengine vya kisasa.

Motifu nyengine ya safari iliyo na sifa za uhalisiajabu katika riwaya ya *Adili na Nduguze* inajitokeza katika safari ya Adili na Nduguze. Mtafiti ameeleza kuwa manyani yalisafiri kwa kupanda farasi kutoka Janibu hadi Ughaibu ili kuitika wito wa Mfalme Rai. Mtafiti ameeleza kwamba manyani waliwafanya watu washangae kila walipopita. Safari hii inasimuliwa na msanii kwa kutueleza hivi:

> "Nyuma yao yaliandama manyani juu ya farasi, alistaajabu. Manyani kupandwa na mnyama ulikuwa upeo wa miujiza …Wakati umefika wa mawe kusema, mito kujibu na wanyama kuwa watu!" (uk. 9).

Katika kisa hiki uhalisiajabu umejitokeza kutokana na msanii kuwasawiri wanyama wakiwa na sifa ya kutumia wanyama wengine katika safari yao. Kama inavyotambulika kwamba wanyama kama vile farasi, punda na ngamia hutumiwa na

binadamu kwa minajili ya usafiri wao binafsi ama kusafirisha mizigo kutoka eneo moja na jengine hata hivyo katika kisa hiki tumewaona manyani wakitumia wanyama katika kurahisisha safari yao kama wafanyavyo wanadamu.

Pia, safari ya Adili na Nduguze katika riwaya ya *Adili na Nduguze* wakati walipokuwa katika misafara ya kibiashara ina matukio ya uhalisiajabu. Wakiwa safarini Adili anawaona viumbe wa ajabu, tandu aliyekuwa akifukuzwa na nyoka. Adili alipogundua kuwa tandu amekabiliwa na hatari ya kupoteza maisha Adili aliamua kufanya juhudi za kumuokoa ambapo alilenga jiwe kumpiga nyoka aliye akimfukuza tandu. Jiwe lile lilifanikiwa kumuua nyoka huyo. Papo hapo yule tandu alijigeuza kiumbe mwanamke mrembo na akapotelea aridhini kwa kupasua ardhi ile kwa kuioteza kidole chake. Msanii ametusimulia kisa hiki kwa kusema:

> “Baada ya safari ya siku moja walifika jabalini. Nahodha aliamuru kutua tanga na kutia nanga. Kisha mabaharia walitakiwa washuke jabalini kutafuta maji kwa sababu jahazini mulikuwa hamna maji hata tone moja… Adili alipanda juu ya jabali. Huko aliona tandu linakimbia. Rangi yake inapendeza sana. Iling’ara kama kioo. Nyuma yake lilifuatwa mbio na nyoka aliyetisha kabisa. Nyoka alipolifika aliliuma kichwani. Kisha alilibana jiweni. Tandu lilitowa mlio wa kusikitisha. Kwa mlio ule Adili alijua kuwa tandu lilikuwa hatarini. Mara ile moyo wake uliingiwa na huruma. Hakuweza kuvumilia. Aliokota jiwelililokaribia uzito wa ratili moja akamtupia nyoka. Jiwe lilimpiga nyoka kichwani. Ilikuwa shabaha nzuri sana. Kichwa chote kilipondeka kwa pigo moja akafa mara ile. Ghafla tandu lilijigeuza mwanadamu, yaani msichana mzuri…Baada ya hayo msichana alielekeza kidole chake cha shahada chini. Mara moja ardhi ilipasuka akaingia ndani yake, alipokwishajitia ndani, ardhi ilijifunga sawia…. (uk. 17-18).

Pia, tukio hili limebeba sifa za Uhalisiajabu. Kitendo cha tandu kugeuka binadamu na kuipasua ardhi kwa kuioteza kidole inaonesha namna tukio hili linavyokiuka uhalisia wa kijamii. Msanii ametumia kisa hiki ili kusawiri wahusika wa visasili vya

kisimulizi ambavyo kama mwandishi alivyoeleza hapo kabla kuwa wataalamu kama vile Wamitila (2013), wanaviona visasili hivyo vimesheheni matukio ya uhalisiajabu.

Mtafiti anaporejelea nadharia ya Uhalisiajabu ameaona kwamba suala la safari hizi za kuajabisha ambazo ndani yake kuna matukio ya kihalisiajabu yanalandana na nadharia ya uhalisiajabu. Katika nadharia ya uhalisiajabu mtafii ameeleza kwamba mito na wadudu huwa wanatumika. Hivyo basi katika safari hii msanii ametumia motifu za safari za aina hii kama sehemu ya vipengele vya kihalisiajabu.

4.5.3 Mandhari za Kihalisiajabu

Madumulla (2011), anaeleza kwamba mandhari katika kazi za fasihi ni mahala ambapo tukio linatendeka. Mandhari katika kazi za fasihi huweza kuwa halisi au ya kidhahania. Katika riwaya ya *Adili na Nduguze*kuna matumizi ya nyumba ya Mfalme na Malkia wa majini. Mandhari hayo, yameelezwa kuwa, yalikuwa ya aina yake; wasichana warembo, Bibi aliyejipambanua kama Malkia pamoja na majohari mbali mbali. Msanii anasema:

> “Fahamu yake iliporudi alijiona katika nyumba kubwa sana iliyokuwa nzuri ajabu. Wasichana warembo waliochangamka walikuwa watumishi katika nyumba hiyo. Miongoni mwao palikuwa na Bibi mmoja aliyejipambanua kama malkia. Huyo alikuwa juu ya kiti cha enzi, kilichopambwa na majohari mbali mbali. Rangi ya mavazi yake yalikuwa ya fua, na kichwani alivaa taji lililopigisha moyo mshindo kwa uzuri” (uk. 34).

Mandhari haya yanaibua maajabu kutokana na ndani yake kuwa na wahusika wenye sifa za uzuri na mapambo ya kushangaza. Kwa sababu hiyo hata Adili ilimfanya ashangazwe na wahusika waliokuwemo katika nyumba hiyo.

Mandhari nyengine ya uhalisiajabu ni ile inayojitokeza katika Mji wa Mawe. Katika mji huo tunaelezwa kuwa kulikuwa hakuna mtu yeyote ispokuwa mwanamke mmoja tu. Mji huo ulikuwa umejaa mawe kila sehemu. Ilielezwa kuwa mawe hayo yalikuwa watu ambao waligeuzwa mawe kutokana na laana ya Mrefu. Tunasimuliwa mandhari hii hivi:

> "Alishuka chini akaingia katika halmashauri nyengine. Hiyo kadhalika ilikuwa sawasawa na ile ya Mfalme, ila ilkuwa na madiwani wanawake watupu. Baadhi ya madiwani walikuwa wamesimama mbele ya Malkia na mikono yao vifuani, na wengine walikuwa wamepiga magoti yao chini yake kwa unyenyekevu. Walakini halmashauri hiyo ilikuwa na mapambo bora kuliko ile ya mwanzo. Palikuwa na meza pembeni, juu ya meza palikuwa na bilauri za johari" (uk. 25).

Pia, katika baraza ya sheria aliyofikishwa Adili kwa madhumuni ya kudai haki za waliodhulumiwa ni mfano mwengine wa mandhari ya uhalisiajabu. Tunaelezwa kuwa, katika baraza hiyo, Adili alikuwa mshitakiwa, manyani walikuwa mashahidi na Mfalme Rai alikuwa ni hakimu. Baraza hiyo inasimuliwa na msanii kwa kusema:

> "Baada ya kutua Adli alipelekwa mbele ya Mfalme na manyani yake. Manyani yalipomuona Mfalme yalifanya ishara mbili. Kwanza yaliinua juu mikono yao kama yaliokuwa yakiomba, pili yalilia kama yaliodhulumiwa. Ishara ya kwanza ilionesha ombi la msaada, na ile ya pili ilionesha mashtaka. Licha ya Rai hata mimi na wewe tungalifasiri hivi kama tungalikuwa kwenye baraza hiyo. Mfalme alipoona vile alitaka kujua kwa Adili sababu ya kuadhbiwa, kulishwa na kunasihiwa manyani yale kila siku, katika sababu zake alionywa kusema kweli tu" (uk. 09).

Mandhari kama hizi, pia tunakutana nazo tunaposimuliwa Hadithi Simulizi za Waswahili. Kwa mantiki hiyo, ni dhahiri kwamba mtunzi alichota visasili hivyo katika Uhalisiajabu za Uswahilini na kuijenga kazi yake. Msanii anaamini kwamba, msaada unahitajika kwa watu wa tabaka la chini. Hivyo, viongozi wanapaswa

kufanya kila juhudi ili kuwasaidia watu watabaka la chini wanapokabiliwa na matatizo.

Pia, katika riwaya ya *Adili na Nduguze*kuna matumizi ya mandhari ya baharini. Bahari hiyo inaoneshwa ina vitimbi na kila aina ya viumbe. Bahari hii imekuwa ikitumiwa na wafanyabiashara wakiabiri kutoka eneo moja na jengine. Kuhusu mandhari hii msanii anatusimulia hivi:

> "Mabaharia wote wakatafuta maji chini ya jabali. Adili alipanda juu ya jabali. Huko aliona tandu linakimbia. Rangi yake lipendeza sana. Linangara kama kioo. Nyuma yake alifuatwa mbio na nyoka aliyetisha kabisa. Nyoka alipolifikia aliliuma kichwani. Kisha alilibana jiweni. Tandu lilitowa mlio wa kusikitisha. Kwa mlio ule Adili alijua kuwa tandu liko hatarini. Mara ule moyo wake uliingiwa na huzuni. Hakuweza kuvumilia. Aliokota jwe… (uk. 18).

Mtafiti kwa kurejelea nadharia ya Uhalisiajabu, ameona kuwa mandhari hayo yamelandana na nadharia ya Uhalisiajabu. Njogu na Wafula (2007), wanaona kwamba moja kati ya msingi wa nadharia hiyo ni matumizi ya mito, maziwa, bahari nakadhalika. Kwa mantiki hiyo matumizi ya mandhari haya ya mito ni upenyezi unaofanywa na msanii ili kuibua sanaa yenye sifa za kihalisiajabu katika ulimwengu wa uhalisia.

Katika utafiti huu kwaudhati kabisa uchambuzi wa vipengele vya uhalisiajabu kama vilivyojidhihirisha katika riwaya ya *Adili na Nduguze* umetilia mkazo kufikia mada ya utafiti huu.Vipengele vya uhalisiajabu ambavyo vimejitokeza katika riwaya ya Adili na Nduguze ni pamoja na: Mtindo wa Udenguzi na Uumbuzi, Mtindo wa Kihalisiajabu, Masimulizi ya Kihalisiajabu, Usawiri wa Wahusika, Utambulisho na

Mwanda wa Kihusika, Motifu za Safari za Kihalisiajabu na Mandhari za Kihalisiajabu

Jadweli 02: Muhtasari wa Vipengele vya Uhalisiajabu katika Adili na Nduguze

Nambari	**Vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya Adili na Nduguze**
01	Mtindo wa Udenguzi na Uumbuzi
02	Mtindo wa Kiuhalisiajabu
03	Masimulizi ya Kiuhalisiajabu
04	Usawiri wa wahusika, Utambulisho na Mwanda wa kihusika
05	Motifu za safari za Kiuhalisiajabu
06	Mandhari za Kiuhalisiajabu

Chanzo: Data kutoka riwaya ya *Adili na Nduguze.* Septemba, 2018

Katika utafiti huu, kwa ujumla uchambuzi wa vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze* umefanyika ipasavyo. Vipengele vya uhalisiajabu ambavyo mtafiti amevibaini na kuvichambua ipasavyo. Sambamba na hilo vipengele hivyo vimeendana kikamifu na lengo mahsusi la kwanza na swali la kwanza la utafiti huu wenye mada: *Kuchunguza uhalisiajabu na Dhamira katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze.* Kwa upande mwengine uchambuzi wa vipengele hivyo umeongozwa na nadharia ya uhalisiajabu kwa lengo mahsusi la kwanza lisemalo: Kubainisha vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.* Lengo hilo limewiana na swali la kwanza la utafiti lisemalo: Ni vipengele vipi vya uhalisiajabu vilivyojitokeza katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.*.

Jadweli 03: Muhtasari wa jumla wa vipengele vya uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika na Adili na Nduguze*

Na.	Vipengele vya uhalisiajabu	Kusadikika	Adili na Nduguze
01	Utatizaji wa wakati	√	×
02	Mtindo wa Udenguzi na Uumbuzi	×	√
03	Mtindo wa Kiuhalisiajabu	×	√
04	Masimulizi ya Kiuhalisiajabu	√	√
05	Usawiri wa wahusika, Utambulisho na Mwanda wa kihusika	√	√
06	Motifu za safari za Kiuhalisiajabu	√	√
07	Mandhari za Kiuhalisiajabu	√	√

Chanzo: Data kutoka riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze. Septemba, 2018.

4.6 Dhamira za uhalisiajabu katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze

Mada ya utafiti huu imehusu: *Kuchunguza uhalisiajabu na Dhamira katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze.* Malengo mahsusi ya utafiti huu yalikuwa ni mawili yanayoendana na maswali mawili ya utafiti. Lengo mahsusi la pili lilikuwa: Kubainisha dhamira za uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.* Lengo mahsusi hilo limekwenda sambamba na swali la pili la utafiti lisemalo: Ni dhamira zipi za uhalisiajabu zimebainishwa katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze?* Ili kuweza kufanikisha vyema lengo mahsusi la pili na kujibu vizuri swali la pili la utafiti huu, uwasilishaji na uchambuzi wa data umefanyika kikamilifu. Uwasilishaji na uchambuzi huo umefanyika kwa kuongozwa

na nadharia ya mwitiko wa msomaji. Uwasilishaji na uchambuzi huo umefuata mtiririko maalum wa riwaya kwa kuanzia na riwaya ya *Kusadikika* na baadae *Adili na Nduguze*:

4.6.1 Dhamira za Uhalisiajabu katika riwaya ya Kusadikika

Mtafiti ili kuweza kutimiza lengo mahsusi la pili na kujibu swali la pili la utafiti huu, ameweza kuchambua data kwa uwazi na ufanisi mkubwa kama ifuatavyo:- Katika uwasilishaji na uchambuzi huo wa data, mtafiti amebaini dhamira mbalimbali za uhalisiajabu zilizojitokeza katika riwaya ya *Kusadikika*. Mtafiti amefanya uchambuzi wake huku akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji:

4.6.1.1 Dhamira ya Ukandamizaji na Unyonyaji

Ukandamizaji na Unyonyaji ni miongoni mwa dhamira za pekee na za uhalisiajabu ambazo mtafiti amezigundua katika riwaya ya *Kusadikika*. Mtafiti amebaini kuwa dhamira hii inaendelea kuakisi uhalisia wa maisha ya jamii nyingi hasa katika bara la Afrika. Kwa mfano mwandishi ameitumia mandhari ya kiuhalisiajabu ya nchi ya Kusadikika na kuibua dhamira ya ukandamizaji na unyonyaji uliokuwa unaendelea katika bara la hilo la Afrika. Kusadikika inaweza kuwakilisha nchi zozote za Bara la Afrika ambazo ziliwahi kutawaliwa na wakoloni. Nchi hizo zilishuhudia ukandamizaji na unyonyaji kutoka kwa watawala wa kikoloni. Msanii alitumia kipengele cha uhalisiajabu ambacho ni Matumizi ya mandhari ya Kiuhalisiajabu ili kufikisha ujumbe kwa jamii. Ni dhahiri kwamba ingekuwa vigumu kwa Shaaban Robert kupeleka ujumbe wa kuwasuta na kuwakosoa wakoloni bila kutumia kipengele kama hiki. Mawazo haya yanaungwa mkono na Salim (2015), alipokuwa akifanya uchambuzi wa riwaya ya *Kusadikika* na kueleza kuwa vikwazo vya dola ya

kikoloni katika Tanganyika vingepiga marufuku kuchapishwa kwa vitabu vya mwanzo mwanzo vya mtunzi huyu (Shaaban Robert) laiti si weledi wake wa usanii. Mathalani, weledi wa mwandishi huyu umejidhihirisha kwa kuchukua mandhari ya nchi inayoelea juu ya anga. Msanii anatusimulia hivi:

> "Nchi hiyo iko katika mipaka sita. Kwa upande wa Kaskazini imepakana na upepo wa kaskazi, na kwa upande wa Kusini imepakana na upepo wa kusi. Mashariki imepakana na matlai na Magharibi mpaka wake ni upepo wa umande. Kwa kuwa nchi wenyewe inaelea katika hewa kama wingu zaidi ya kupakana na pepo nne hizo, ina mipaka mengine miwili yenyewe ni hii. Kwa juu nchi hiyo imepakana na mbingu na kwa chini imepakana na Ardhi (UK. vii*)*

Nchi ya Kusadikika imeelezwa kihalisiajabu kutokana na kukiuka uhalisia wa maisha ya kila siku. Mwandishi ameeleza kwamba nchi ya Kusadikika inaelea angani kama wingu na ina mipaka sita tofauti na nchi za kihalisia ambazo huwa na mipaka katika pande minne tu. Kutokana na hali hii tumeelezwa kuwa nchi hii kuwepo kwake ni kufikirika tu. Kwa mfano, msanii anatueleza hivi:

> Kusadikika ni nchi ambayo kuwako kwake ni kwa kufikirika kwa mawazo tu (uk. Viii).

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti ameona kwamba dhamira ya ukandamizaji na unyonyaji unaofanywa na watawala wa Kusadikika unalandana na matukio ya nchi nyingi za bara la Afrika ambako watawala wake hata baada ya nchi hizo kupata uhuru wa bendera zimekuwa zikiendeleza ukandamizaji na unyonyaji huo uliokuwa ukifanywa na wakoloni.

4.6.1.2 Dhamira ya Maendeleo na Ukuaji wa Huduma bora za Kijamii

Upatikanaji wa huduma bora za kijamii hurahisisha maendeleo ya haraka katika jamii au taifa husika. Taifa lotote linalohitaji kusonga mbele kimaendeleo linawajibika kuimarisha huduma hizo za kijamii ipasavyo. Miongoni mwa huduma hizo za kijamii ni pamoja na Uwepo wa huduma bora za afya, shule na taaluma kwa ujumla, miundo mbinu ya kisasa kama barabara, viwanja vya ndege pamoja na uongozi bora. Katika utafiti huu, dhamira ya maendeleo na ukuaji wa huduma bora za kijamii imejitokeza kwa wajumbe wote sita waliotajwa na Karama kuhusiana na habari yao ya kutalii nchi na maeneo mbalimbali waliokwenda kwa lengo la kufanya utafiti ili kuiletea neema Kusadikika ingawaje mwanzoni juhudi zao hazikuthaminiwa. Wajumbe hao sita ni Amini, Auni, Burhani, Fadhili, Kabuli na Ridhaa. Mathalani Mjumbe wa Mbiguni ambaye ni Ridhaa alijitolea kwa dhati kwa ajili ya kuiletea neema nchi yake ya Kusadikika baada ya kuzuru Mbinguni. Mwandishi anaeleza:

> “Majengo ya halmashauri hizo yalikuwa ya ajabu kubwa kabisa.Yalijengwa kwa majohari bora na ya namna ya peke yake. Yaliyosakafiwa kwa dhahabu safi tupu. Majohari hayo hayakupatikana mahali popote ulimwenguni. Kila halmashauri ilikuwa juu ya uwanjampana uliokuwa na mabustani. Mabustani hayo yalivuta sana macho kwa uzuri wa maua yake ya ajabu. Sanamu zilizochorwa kwa majohari mbalimbali…(uk.38).

Mandhari hii imetumika ili kuibua dhamira ya kuonyesha jinsi mataifa makubwa kama vile Marekani, China, Uingereza, Urusi, Japani na Ufaransa yalivyopiga hatua kimaendeleo ukilinganisha na nchi zinazoendelea zikiwemo nchi za bara la Afrika. Msingi wa upatikanaji wa dhamira hii ya Maendeleo na Ukuaji wa Huduma bora za

Kijamii umetokana na kipengele cha uhalisiajabu ambacho ni Matumzi ya mandhari ya uhalisiajabu.

Mtafiti anaporejelea nadharia ya Mwitiko wa msomaji amegundua kuwa mataifa makubwa kama Marekani, China, Uengereza, Urusi, Ufaransa na Japani yamepiga hatua kimaendeleo kama vile huduma bora za afya, kipaombele katika elimu na miundo mbinu bora mfano, barabara, viwanja vya ndege nakadhalika. Hivyo basi, ili kuweza kufikia hatua kubwa za kimaendeleo, nchi zinazoendelea nazo hazina budi kuiga hatua mbali mbali zinazochukuliwa na mataifa makubwa ambazo zimesaidia kufikia maendeleo hayo.

4.6.1.3 Dhamira ya Tamaa na Uchoyo

Tamaa na Uchoyo ni miongoni mwa tabia mbaya ambazo mwanaadamu hatakiwi kuwa nazo. Ni ukweli usioshaka, kuwa katika jamii zetu baadhi ya watu wanazo tabia hizi. Watu wa aina hio si mfano mzuri wa kuigwa na mwisho wao huwa ni mbaya. Utafiti huu umebaini uwepo wa tabia hizi kupitia kwa wahusika Sapa na Salihi ambao tabia zao zilielezwa na Mjumbe wa Magharibi ambaye ni Auni. Mtafiti ametumia kipengele cha uhalisiajabu ambacho ni Matumizi ya Motifu za Safari za Kihalisiajabu kuweza kuibua dhamira hiyo ya Tamaa na Uchoyo akimueleza Auni kuwa ni mjumbe aliyetumwa kutoka Kusadikika kwenda Magharibi. Hii ni motifu ya safari ambayo lengo lake ni kuzibaini tabia mbalimbali za watu anaokutana nao na kuendelea kueleza tabia za watu mbalimbali kupitia jamii zao.

Mwandishi amesimulia kisa cha Sapa na Salihi kupitia muhusika Auni ambapo ametuonesha namna tamaa na uchoyo vinavyotawala miongoni mwa wanajamii.

Uchoyo ambao watu wanao huwapelekea kuwa waongo na wasioridhika na kile walichokipata. Mathalani, Sapa anapata upofu kutokana na kutoridhika na hatimae kusema uongo jambo ambalo linamuingiza katika janga ambalo hakulitarajia. Muhusika Sapa na Salihi ni wahusika wa uhalisiajabu katika riwaya ya Kusadikika. Imesimuliwa kuwa wahusika hawa walikuwa wanaona hapo kabla. Hata hivyo, wanapata upofu baada ya Salihi kuomba kwa Mungu kuwa ni vyema kuwa vipofu wote kuliko kuona matendo mabaya yanayoendelea ulimwenguni. Mwandishi ameweka wazi:

> "….Vipofu hawa wote walikuwa wanaume. Kipofu mmoja alikuwa mbele na wapili nyuma.Uso wa kipofu wa kwanza ulikuwa nafuraha kama uso wa bwana arusi, akaonekana kama aliyeridhika kabisa. Lakini uso wa kipofu wa pili ulikuwa umeghadhibika na kinywa chake kilijaa manung'uniko mengi kama aliyekuwa hakuridhika hata kidogo. Kila hatua aliyokwenda alibwata akailaani bahati yake. Auni alishangaa sana kwa kuona vile, akasema moyoni mwake kuwa watu hawa wana vilema namna moja, lakini mmoja amekinai na mwengine hakukinai. Ajabu kubwa ilioje hii. Afadhali niulize ili nielewe sababu yake. Baada ya kukusudia hivyo, alitamka,`mabwana, nyinyi ni kina nani, na asili ya upofu wenu ni nini? Kipofu wa pili alijibu, `bwana wangu mwema, mimi naitwa Sapa na mwenzangu ni Salihi. Salihi haombi neno akalikosa. Ameishi maisha haya tangu ujana wake, lakini vitu alivyovipata kwa maombi aliyoyafanya alikuwa hana matumizi navyo. Nilipoona hivyo nilimwambia kuwa, niliota ndoto kuwa akiomba kitu chochote tena bila…dua lake halitapokewa hata kidogo. Kwa sababu hii tuliafikiana kushirikiana kila kitu atakachokiomba tukaandikiana hati mbele ya Kadhi … Lakini pale pale mwenzangu aliinua mikono yake juu akaomba upofu, na kabla sijatanabahi, sisi sote wawili tulikuwa vipofu, kama yeye anaipenda hali hii mimi naichukia kabisa…(uk.29-30).

Kwa mnasaba wa nadharia ya Mwitiko wa msomaji kupitia mihimili yake, imempa fursa mtafiti kuihakiki hali ya jamii iliyomzunguka, kwa kutoa maoni kwamba, Tamaa na uchoyo kilivyoikabili jamii. Watu hupelekea hata kuuana kwa sababu ya tabia hizo. Wengine hujitumbukiza katika vikundi viovu kwa sababu ya tabia hizo.

Matokeo yake huwafanya watu kupata majuto baada ya athari mbaya wanazozipata kutokana na tamaa nauchoyo.

4.6.1.4 Dhamira ya Uongozi Mbaya

Maendeleo ya taifa lolote yatafikiwa endapo viongozi wa jamii au mataifa hayo watakuwa ni wenye kuwajali na kuwathamini wananchi wao na kuwaongoza katika misingi mizuri na yenye kukubalika kwa wanachi wote. Viongozi hao wanawajibu wa kusimamia haki na uadilifu kwa wananchi wote. Kinyume na uongozi bora, jamii au mataifa hayo huishi katika uongozi mbaya. Baadhi ya viongozi katika jamii mbalimbali zikiwemo za Kiafrika mfumo wao wa uongozi ni mbaya. Viongozi hao hawasimamii haki na uadilifu kwa wananchi wao na badala yake uongozi wao hujielekeza kuwa na kiburi, dharau, kejeli, uonevu na ukatili pamoja na kutokuwajali raia wao.

Katika riwaya ya *Kusadikika* mfano mzuri wa kiongozi ambaye uongozi wake ulikuwa mbaya ni Majivuno. Majivuno alikuwa waziri katika serikali ya Kusadikika. Hata hivyo, waziri huyu anaonesha maajabu kutokana na vile alivyo na upeo mdogo wa kuchambua maswala mbali mbali ya kijamii. Mathalani, upungufu wake wa elimu ulimfanya apinge mawazo ya kuanzishwa kwa elimu ya uanasheria huku akidai kuwa Karama ni mjinga kwa sababu ya weusi wa nywele zake. Majivuno anasema hivi:

> "… Mshitakiwa ana maneno mengi kama kitabu. Nakanusha kuwa ajua kitu chochote juu ya hekima. Hekima ni kitu adimu kupatikana na mtu asiye mvi. Weusi wa nywele za mshitakiwa waonyesha wazi ujinga alionao…" (uk .10).

Katika nukuu hii msanii ameibua dhamira ya uongozi mbaya. Msanii ameonesha kwamba, Kusadikika ilikuwa ikiongozwa na viongozi madikteta. Kutokana na udikteta huo walipinga kila jambo jema. Upinzani huu ulifanyika bila ya sababu za msingi. Majivuno ni mhusika aliyechorwa kuwa na sifa mbaya, ndio maana akaitwa jina hilo. Kama asemavyo Kyando (2012), kwamba Majivuno ni jina lenye maana ya kujiona maringo au kiburi. Hivyo basi, kutokana na sifa hizi Majivuno anasimuliwa akiwa na tabia hizi:

> Majivuno, mtu aliyejihisabu mwenyewe kuwa kidole chake kidogo kilikuwa na akili nyingi kuliko vichwa na miili ya Wasadikika wote ikiwekwa pamoja, alikuwa amejifunga kwa kumtosa mshitakiwa katika bahari ya maangamizi. Kwa hivi, alisema kwa werevu kuwa uanasheria ungewezekana kufasiriwa wazi wazi sana na Mudiri wa Sheria za Kusadikika kuliko mshtakiwa. Mudiri wa sheria aliotakiwa kufanya tafsiri alisema, `Uanasheria ni elimu ya kupingana na sheria (uk.13).

Mfano huo hapo juu umetuthibitishia namna jina la mhusika Majivuno, linavyosadifu na tabia za mhusika huyo. Katika usadifu wa jina hilo la muhusika Majivuno na tabia zake, mtafiti amebaini kuwa tabia na jina la Majivuno limehalisika na kipengele cha uhalisiajabu ambacho ni Matumizi ya Wahusika wa Kihalisiajabu; kwa mfano tabia yake Majivuno, kujihesabu na kujiona mwenyewe kuwa kidole chake kidogo kilikuwa na akili nyingi kuliko vichwa na miili ya Wasadikika wote ikiwekwa pamoja. Vile vile, Majivuno ametumika kuwa mhusika wa uhalisiajabu kutokana na kutumia maisha yake yote akiwa katika uongozi. Hali hii imemfanya Majivuno kuhisi kuwa watu wengine hawana akili na mwenye akili ni yeye tu. Mwandishi ametueleza hilo:

> “Waziri wa Kusadikika alikuwa mtu mwenye haiba kubwa na uhodari mwingi. Kwa hivi aliitwa Majivuno. Uwaziri wake ulianza zamani sana. Alikuwa waziri wa wafalme watatu katika nyakati mbali mbali. Babu yake mfalme anayesimuliwa aliposhika ufalme, yeye alishika uwaziri, baba yake alipokuwa nahodha wa chombo cha serikali, yeye alikuwa rubani wake; akaendelea katika hadhi hiyo mpaka enzi ya mfalme mpya…Mtu huyu alikuwa maarufu na mashuhuri lakini alijaa tadi na inda…” (uk.01).

Kupitia muhusika Majivuno, mwandishi ameonesha kwamba viongozi wengi baada ya kukalia viti vya madaraka hawataki kuondoka katika madaraka hayo. Uongozi umekuwa ukirithiwa mithili ya mali za familia. Majivuno alitumia fursa ya wazazi wake waliowahi kuwa viongozi na yeye kutaka kufuata nyayo hizo hizo.

Kwa kurejelea nadharia Mwitiko wa Msomaji, mtafiti amebaini kuwa mhusika Majivuno anaakisi viongozi wengi waliowahi kuwepo na hata wale walioshika hatamu za uongozi baada ya uhuru hasa katika bara la Afrika walikuwa na wanaendelea kuwa ni wabaya kutokana na tabia yao ya ulafi wa madaraka, majivuno na kuwadharau wananchi waliowaweka katika nafasi za uongozi. Kauli hii inathibitishwa na Armah (1951) ambaye ameona kuwa mzuri hajazaliwa. Akimaanisha kuwa pamoja na Bara la Afrika kupata uhuru bado halijapata viongozi waliobora.

4.6.1.5 Umuhimu wa Elimu ya Uanasheria

Elimu ni rasilimali adhimu katika ujenzi wa jamii bora. Elimu ndio ufunguo wa maisha bora. Elimu ni nuru na hazina iliotukuka. Katika maendeleo ya jamii yeyote elimu ndio tegemeo kubwa la mafaniko hayo. Kukosekana kwa elimu ni majanga. Umuhimu wa elimu hutegemea aina ya elimu au fani / taaluma hiyo. Katika utafiti huu, elimu ambayo mtafiti amebaini imetiliwa mkazo ni elimu ya uanasheria. Elimu

ya uanasheria imehusishwa na muhusika mkuu wa riwaya ya *Kusadikika* ambaye ni Karama. Karama ni muhusika aliyejitolea mhanga kwa ajili ya nchi yake ya Kusadikika kwa kuanzisha elimu hiyo ambayo ilikuwa imeonekana kuwa ngeni na ni jambo la ajabu lililopigwa vita na waziri mkuu Majivuno. Elimu ya Uanasheria ililenga kuwakomboa wananchi wa Kusadikika, kuwaletea maendeleo kupitia juhudi za wajumbe sita ili kuondokana na umasikini (hali ngumu ya maisha)

Karama ni muhusika aliyesawiriwa akiwa ni muhusika wa kiuhalisiajabu. Mtafiti kama alivyoeleza hapo kabla kuwa Karama aliajabiwa na Wasadikika kutokana na ujasiri wake wa kutaka kuanzisha elimu ya sheria. Kutokana na tukio hili Karama alipigania haki bila ya kujali kuwa iwapo atakamatwa na hatokuwa katika salama. Mwandishi ameeleza:

> Sheria za Wasadikika zilikuwa hazimuamuru mshitakiwa kujitetea juu ya ushahidi wa mshitaki. Aghlabu mashtaka mengi yalikubaliwa bila ya swali wala kiapo. Labda hii ndiyo sababu ya nchi yao kuitwa Kusadikika. Kama mashtaka yaliletwa mbele ya baraza na Wafalme, watoto wao matajiri, au watu wengine maarufu nguvu ya desturi hii ilifanywa mara dufu. Hapana shaka kwamba salama ya watu wadogo ilikuwa kidogo sana katika nchi hii … (uk. 7).

Kupitia muhusika Karama mtafiti ameibua dhamira ya umuhimu wa elimu ya uanasheria. Mwandishi anaamini kwamba elimu ya uanasheria ni muhimu sana katika maisha ya kila siku. Popote panapokosekana utawala wa sheria watu wema wataonekana wabaya na wabaya wataonekana wema. Pia, utawala unapokiuka sheria katika jamii kinachofuata ni unyonyaji na ukandamizaji wa tabaka la chini na kamwe nchi hiyo haiwezi kupiga hatua za maendeleo.

Kusadikika ilikosa maendeleo kutokana na kukosekana kwa utawala wa sheria. Mawazo ya watu hayakuthaminiwa na hatimae wale waliotoa mawazo hayo waliishia gerezani. Vile vile, msanii ameonesha kwamba katika jamii yoyote ambayo sheria inakiukwa tafiti za kimaendeleo hazithaminiwi. Mathalani, katika nchi ya Kusadikika wajumbe sita waliokwenda kutafiti nchi jirani waliporejea na kuwaeleza viongozi hawakuthaminiwa na hatimae waliwatia gerezani. Mwisho ilibainika kuwa hawakuwa na hatia yoyote. Msanii amesimulia hili kwa kusema hivi:

> Zaidi ya hayo, natoa amri kuwa waliotajwa katika kesi hii - Burhani, Fadhili, Kabuli, Auni, Ridhaa na Amini - wafunguliwe mara moja. Inasikitisha sana kuwa dhuluma juu ya watu hawa hazikutengenezwa mpaka leo. Gereza ni makao ya wahalifu. Watu hawa si wahalifu ila wafadhili bora. (uk 57)

Aidha, data za utafiti huu zimeonesha kwamba mwandishi anaamini watu wa tabaka la juu hupanga njama za kuhakikisha wamewaangamiza wale walio na chuki nao kutokana na kukosekana kwa sheria. Mwandishi anamtumia muhusika Majivuno ambaye amejidhatiti kumtia hatiani na kumuangamiza Karama mbele ya Mfalme wa Kusadikika.

Msanii amesema:

> “Majivuno mtu aliyejihesabu mwenyewe kuwa kidole chake kidogo kilikuwa na akili nyingi kuliko vichwa na miili ya wasadikika wote ikiwekwa pamoja, alikuwa amejifunga kwa kumtosa mshtakiwa katika bahari ya mangamizi. Kwa hivi alisema kwa werevu kuwa uwanasheria ungewezekana kufasiriwa wazi wazi sana na Mudir wa sheria za Kusadikika kuliko Mshitakiwa. Mudir wa sheria alipotakikana kufanya tafsiri alisema` Uanasheria ni elimu ya kupingana na sheria (uk. 8).

Kwa mnasaba wa nadharia ya mwitiko wa msomaji inayoongoza lengo mahsusi la pili na swali la pili la utafiti huu, nidhahiri kwamba, suala la sheria katika nchi za Kiafrika halitiliwi maanani. Kidhahiri tunagundua mizozo mingi katika jamii za Kiafrika msingi wake ni mgongano wa sheria; mathalan mivutano ya vyama vya siasa, migogoro ya wakulima na wafugaji tunayoishuhudia leo na ikiwa na maafa makubwa inatokana na sheria kuchezewa. Sheria huchezewa, bila kujali, huo ni ukiukaji wa haki za binadamu. Karama ni kiwakilishi cha wanasheria duniani wanaoandamwa na kufikwa na mengi kama kupigwa na hata kuuwawa kwa makundi ya watu wasiojuilikana. Dhamira ya umuhimu wa elimu ya uanasheria imeibuliwa kutokana na kipengele cha uhalisiajabu ambacho ni Matumizi ya Wahusika wa Kihalisiajabu.

4.5.1.6 Dhamira ya Ukombozi

Ukombozi ni msingi muhimu wa kuleta mabadilko katika jamii inayohitaji kusongambele kimaendeleo. Ukombozi huhitajika kufanyika katika jamii iliojaa maovu mbalimbali ikiwemo uongozi mbaya. Wananchi hulazimika kuwa na umoja na mashirikiano ya dhati ili kuweza kuhakikisha wanajikomboa kutoka katika madhila na kila aina ya uonevu. Katika riwaya ya *Kusadikika*, mtafiti amegundua kuwa dhamira ya ukombozi imehusishwa na wajumbe sita waliotumiwa na Karama. Wajumbe hao ni wafuatao: Burhani – Mjumbe wa Kaskazini, Fadhili – Mjumbe wa Mashariki, Kabuli – Mjumbe wa Kusini, Auni – Mjumbe wa Magharibi, Ridhaa – Mjumbe wa Mbinguni na Amini Mjumbe wa Aridhini.

Kwa ujumla wajumbe wote hao walijtolea kikamilifu kwa ajili ya taifa / jamii yao ya Kusadkika. Wajumbe hao walijitolea muhanga kuhakikisha kwamba Kusadikika

inakomboka na kuwa ni nchi yenye maendeleo makubwa. Aidha wajumbe hao katika safari zao walikumbana na vikwazo vingi mno ambavyo pamoja na vikwazo hivyo hawakukata tamaa na waliendelea na safari yao.

Mtafiti amebaini kuwa wajumbe sita hao wametumiwa kiuhalisiajabu. Wajumbe hawa walitalii nchi jirani na Kusadikika kwa safari zenye hatari ndani yake. Hata hivyo hawakurudi nyuma kwa sababu walikuwa wanania ya kuifadhili Kusadikika. Mbali na hilo wajumbe hawa waliporudi Kusadikika hawakuthaminiwa na hatimae waliadhiriwa na kufungwa jela kama wahalifu. Pamoja na miktadha hiyo pale alipohitajika kupatikana mjumbe mwengine, alipatikana kwa wepesi kuliko yule wa mwanzo. Kupatikana kwa baadhi ya wajumbe hawa msanii amesema:

> “Mtu mwenye sifa njema alitakiwa kujitokeza mwenyewe kwa ujumbe wa mashariki kama mara ya kwanza, lakini sasa mtu kama huyo alipatikana upesi sana kuliko ilivyoikitazamiwa. Mtu huyo alikuwa akijuilikana kwa jina la Fadhili. Habari ya msiba wa Buruhani ilikuwa ikijuilikana na Fadhili lakini haikumvunja moyo wake” (uk. 16-17).

Aidha, katika kufanya ukombozi lazima watu wajitoe muhanga na kupambana na misuko suko itakayo wakabili. Wajumbe sita wa Kusadikika walifikwa na misukosuko pamoja na idhara lakini hawakukata tamaa. Kwa mfano, msanii ametueleza namna Kabuli alivyokumbwa na masaibu kadhaa kwa kusema:

> “Kama ijulikanavyo, kusini ni upande wa dunia yatokako matofani makubwa na baridi kali sana. Kabuli aliyakabili mashaka hayo bila ya kigeugeu. Naam alikuwa kama mtu aliyekuwa akinywa uchungu mwingi bila kigegezi. Mara ya kwanza alikamatwa Juju, nchi ya Mfalme Jeta …” (uk. 23).

Ujasiri kama huu leo umekosekana katika jamii nyingi. Hili linatokea kwa sababu ya ubinafsi na usaliti. Ili kuleta ukombozi wa kweli hatunabudi watu kuwa majasiri. Kama asemavyo Salim (2015), kwamba ili kuleta ukombozi lazima watu wawe majasiri, wawe wamoja na wajitoe mhanga. Anawapigia mfano, wahusika Karama, Buruhani, Fadhili, Kabuli, Auni, Ridhaa na Amini, wakiwa wanajitoa mhanga, ili kuhakikisha wameleta ukombozi katika nchi ya Kusadikika.

Aidha, mtafiti ameona kwamba ili kufanikisha ukombozi, lazima watu wawe na hekima, ushujaa na ufasaha katika kuzungumza. Maneno ya busara na hekima huwafanya watu watambue ukweli. Mwandishi amemtumia mhusika Karama alifanikiwa kuleta ukombozi wa nchi ya Kusadikika kutokana na sifa alizokuwanazo za hekima, ushujaa na ufasaha wa maneno. Kwa mfano katika kulielezea hili msanii amemsimulia Karama hivi:

> “Kwa wasifu wa nje, mshitakiwa alikuwa hana umbo la kufanya mvuto kwa watu, lakini kwa wasifu wa ndani, alikuwa na ajabu tatu. Kichwa chake kilikuwa na ubongo wa hekima, kifuani alikuwa na moyo wa ushujaa, na kinywani moyo wa ufasaha. Vipawa hivi vilikuwa katika siri kubwa sana … Alijizoeza kuvitumia vipawa hivi mpaka vilikuwa tayari kutumika siku yoyote katika maisha yake…” (uk. 08).

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kupitia mihimili yake na mtazamo wa mtafiti imetilia mkazo suala la ukombozi. Mtafiti ameona kwamba Afrika, Tanzania ikiwemo inahitaji ukombozi katika viwango tafauti. Bado bara hili linahitaji ukombozi wa kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na hata fikra. Ukombozi huu ndio uliohitajika katika nchi ya Kusadikika ambayo inawakilisha bara la Afrika. Dhamira ya Uombozi imeendana na msingi wa kipengele cha uhalisiajabu ambacho ni

Matumizi ya Wahusika wa Kihalisiajabu kupitia wahusika Karama pamoja na wajumbe sita.

4.6.1.7 Dhamira ya Ubadhirifu wa Mali ya Umma

Ubadhirifu wa mali ya umma ni miongoni mwa tabia mbaya ambazo baadhi ya watu wanaziendeleza katika maisha yao ya kila siku. Tabia ya aina hii ni kikwazo kikubwa katika maendeleo ya jamii. Jamii yeyote inawajibu wa kuwapiga vita watu wenye tabia kama hiyo ili jamii hiyo iishi katika mafanikio. Mtafiti amebaini dhamira ya Ubadhirifu wa mali ya umma ambayo imejitokeza katika riwaya ya Kusadikika kupitia muhusika Mfalme Jeta. Mfame Jeta ni mfalme wa nchi ya Juju. Imeelezwa kuwa Kabuli ambaye ni mjumbe wa Kusini alifika katika nchi ya Majuju. Taifa la Majuju limeelezwa katika riwaya ya Kusadikika kuwa watu wake walikuwa ni wabadhirifu wa mali ya umma. Kutokana na tabia hiyo kila kitu kigumu kilionekana laini na kila kichungu kilionekana kitamu katika vinywa vya Majuju. Kabuli alikamatwa na kupelekwa mbele ya Mfalme Jeta na kutaka amle bila ya kugawana na wawindaji. Kitendo hiki kilisababisha kuzuka mapigano baina ya majeshi ya mfalme na raia. Kwa vita hivyo kila kitu kilichokuwa na uhai kiliangamia isipokuwa alibakia Kabuli (uk. 25-26).

Mtafiti amebaini kwamba kupitia kipengele cha wahusika wakiuhalisiajabu akiwemo Mfalme Jeta,mtafiti ameibua dhamira ya Ubadhirifu wa Mali ya Umma.Mwandishi ameonesha kwamba, kutokana na ubadhirifu wa mali ya umma uliokithiri miongoni mwa wanajamii, hasa wale walio katika ngazi za madaraka, hupelekea tabia hiyo na ulafi maovu mengi yamekuwa yakitendeka ikiwamo wizi, ujambazi, kutoa na kupokea rushwa. Matokeo yake ni kuibuka kwa mikinzani miongoni mwa wanajamii

na kulifanya taifa lisiwe na maendeleo. Hatimae kuliingiza taifa hilo katika vita vya wenyewe kwa wenyewe. Msanii anatusimulia kwa kusema:

> “Majuju ni taifa lafi na litishalo kabisa. Kila kitu kigumu kijuilikanacho duniani kilikuwa laini kama mkate kati ya meno ya Majuju; na kilichokichungu kilikuwa kitamu kama asali katika maonjo yao. Kwa ulafi uliokithiri viumbe hawa, walikuwa hawajui halali wala haramu. Kabuli alipopelekwa mbele ya Jeta alimkuta amekaa kitako midomo wazi. Mto mrefu na mpana ulikuwa ukimiminika katika kinywa chake kikubwa sana. Tone la maji hata moja halikupata nafasi ya kukiepuka kinywa hicho. tani milioni moja za mwamba, milioni moja za chuma, milioni moja za magogo na milioni nyingi za samaki, zilikuwa zikitiririka katika kinywa chake, lakini kila dakika moja, Jeta alilia kiu, njaa, kiu, njaa! Mfalme alitaka kumla Kabuli bila ya kugawana na wawinda waliomkamata. Choyo chake kikubwa kiliwaudhi wawinda, pakatokea vita baina ya majeshi ya mfalme na raia. Kwa vita hivyo, kila kitu kilichokuwa na uhai kiliangamizwa, akabakia Kabuli peke yake. Huu ulikuwa wokovu mwembamba kama unywele” (uk. 23).

Kwa kuhusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, mtafiti amegundua kuwa suala la ubadhirifu wa mali ya umma limelandana na kile kinachotokea katika ulimwengu. Mathalani, suala la rushwa na wizi wamali ya umma leo hii limekuwa ni tatizo la ulimwengu na namna ya kulipiga vita imekuwa ni sugu. Pia ubadhirifu wa mali za umma katika Bara la Afrika, Tanzania ikiwemo ni tatizo kubwa ambalo hufanya wale wenye dhamana kujilimbikizia mali za umma kwa njia zisizo halali. Harakati za mapambano ya uhujumu uchumi zilizoanzishwa na vongozi waliotangulia na waliopo akiwemo Mheshimiwa Raisi Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohd Shein dhidi ya wahujumu uchumi ni mbinu ambazo zimelenga kukomesha ubadhirifu wa mali za umma unaoendelea Tanzania.

Kwa hakika riwaya ya Kusadikika ni riwaya inayoakisi kwa ukamilifu wake dhamira sadifu ambazo zimehusiana na nadharia ya uhalisiajabu. Katika uchambuzi uliotangulia kupitia riwaya hio, dhamira za kiuhalisiajabu zimebainishwa ipasavyo kwa kuhusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Dhamira hizo ni pamoja na dhamira ya Ukandamizaji na Unyonyaji, dhamira ya Maendeleo na Ukuaji wa Huduma bora za Kijamii, dhamira ya Tamaa, Wivu na Uchoyo, dhamira ya Uongozi mbaya, dhamira ya Umuhimu wa elimu ya Uanasheria, dhamira ya Ukombozi na dhamira ya Ubadhirifu wa mali ya umma. Uchambuzi wa dhamira hizo umezingatia lengo mahsusi la pili na swali la pili la utafiti huu.

Jadweli 04: Muhtasari wa Dhamira za Uhalisiajabu katika riwaya ya Kusadikika

Nambari	**Dhamira za Uhalisiaabu katika riwaya ya Kusadikika**
01	Dhamira ya Ukandamizaji na Unyonyaji
02	Dhamira ya Maendeleo na Ukuaji wa Huduma bora za Kijamii
03	Dhamira ya Tamaa, Wivu na Uchoyo
04	Dhamira ya Uongozi Mbaya
05	Dhamira ya Umuhimu wa Elimu ya Uanasheria
06	Dhamira ya Ukombozi
07	Dhamira ya Ubadhirifu wa Mali ya Umma

Chanzo: Data kutoka riwaya ya *Kusadikika*. Septemba 2018

4.6.2 Dhamira za Uhalisiajabu katika riwaya ya Adili na Nduguze

Kwa upande mwengine mtafiti katika kutimiza lengo mahsusi la pili na swali la pili la utafiti huu, amewasilisha uchambuzi wa data na kubaini dhamira mbalimbali za uhalisiajabu katika riwaya ya *Adili na Nduguze* huku akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.

4.6.2.1 Dhamira ya Uongozi bora

Uongozi bora ni miongoni mwa msingi mkubwa katika jamii. Hapana shaka yoyote taifa lenye uongozi bora hupiga hatua mbalimbali za kimaendeleo kama vile upatikanaji wa miundo mbinu bora mfano barabara, vituo vya afya, elimu, maji safi na salama.Pia uadilifu, haki na usawa, upendo, amani na umoja huweza kupatikana katika jamii.

Katika riwaya ya *Adili na Nduguze*, mtafiti amegundua kwamba mtunzi ametumia kipengele cha matumizi ya masimulizi ya uhalisiajabu kwa lengo la kuibua dhamira ya uongozi bora aliyolenga kuifikisha kwa wasomaji wake.Nukuu hiyo hapo chini inafafanua:

> “Rai mfalme wa Ughaibuni alikuwa Mfalme wa aina ya pekee duniani…tabia yake ilijigawa katika theluthi tatu mbali mbali kama ngozi ya pundamilia …. Kwa theluthi ya kwanza alikuwa msuluhivu akapendwa na watu. Kwa theluthi ya pili alifanana na Daudi akaheshimiwa kama mtunzaji mkuu wa wanyama. Na kwa theluthi ya tatu alikuwa kama Suleiman akatiiwa na majini…” (uk 1).

Kupitia nukuu hiyo, mwandishi anatoa wito kwa viongozi wa Afrika ikiwemo Tanzania kutii na kuheshimu kanuni za uongozi bora. Pindipo viongozi wakitawala kwa misingi ya sheria watahesimiwa na kutiiwa na watu wa matabaka yote.

Kwa msaada wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, mtafiti ameona kuwa mwandishi amewakosoa watawala waliokuwepo ambao hawakulijali tabaka la chini. Watawala hao hawakupendwa na raia wao kwa sababu hawakuwa waadilifu.Mfano wa viongozi ambao wamejitahidi katika uongozi wao kuwa bora ni Mfalme wa Nchi ya Ughaibuni. Kwa hakika mfano huo unastahiki kuigwa na viongozi wengine wa mataifa mbalimbali duniani likiwemo bara la Afrika - Tanzania ikiwa ni mojawapo.

4.6.2.2 Dhamira ya Uongozi Mbaya.

Uongozi mbaya ni kitendo ambacho kinafanywa na baadhi ya viongozi ambapo katika uongozi wao huwa hawatumii sheria. Uongozi wa aina hii unapigwa vita na mataifa mengi duniani na hata Tanzania kwasababu huwafikisha watu pabaya na kuifanya nchi kushindwa kupiga hatua za kimaendeleo. Masimulizi haya ya uhalisiajabu,mtafiti ameyaona kupitia kisa cha tandu na nyoka aliowaona Adili wakati alipopanda juu ya jabali. Mwandishi amesimuliwa kuwa Adili alimuona tandu akifukuzwa na nyoka karibu kupoteza maisha. Hivyo basi, Adili alimuua nyoka ili kumsaidia tandu kwa kulenga jiwe ambalo lilimpiga nyoka kichwani na kufa hapohapo. Baada ya uokovu huu tandu aligeuka binadamu na hatimae akazama ardhini. Mwandishi amesimulia:

> “Adili alipanda juu ya jabali huko aliona tandu likikimbia. Rangi yake inapendeza sana. Linang`ara kama kioo. Nyuma yake lilifukuzwa mbio na nyoka alietisha kabisa. Nyoka alipolifika aliliuma kichwani. Kisha alilibana jiweni. Tandu lilitoa mlio wa kusikitisha. Kwa mlio ule Adili alijua kuwa tandu lilikuwa hatarini. Mara ile ile moyo wake ulingiwa na huruma. Hakuweza kuvumilia. Aliokota jiwe lililokaribia uzito wa ratili moja akamtupia nyoka. Jiwe lilimpiga nyoka kichwani. Ilikuwa shabaha nzuri sana. Kichwa chote kilipondeka kwa pigo moja akafa mara ile. Ghafla tandu liligeuka mwanadamu, yaani msichana mzuri….baada ya hayo msichana alielekeza kidole chake cha shahada chini. Mara moja aridhi ilipasuka

> akaingia ndani yake. Alipokwishaingia ndani ardhi ilijifunga sawia… (uk. 17-18).

Kupitia masimulizihaya ya uhalisiajabu Mtafiti ameibua dhamira ya uongozi wa mbaya ambao unashuhudiwa na ulimwengu. Mataifa yenye nguvu yanayogongana yakiashiriwa na tandu na nyoka. Mtafiti amebaini kuwa mwandishi hapa ametusawiria kambi mbili kuu ulimwenguni yaani ubepari na ujamaa namna zilivyokuwa katika mikinzano ya kushindana nguvu ikiwa ni pamoja na kuingia katika vita. Adili ni ishara ya nchi changa Tanzania ikiwa mojawapo hupata misaada yakufanya juhudi kubwa ya kuisaidia nchi tajiri kama vile Marekani, Uingereza, Urusi, China na Japani nakadhalika. Nyoka ameashiria ujamaa ambao ulipigwa mbiu na Urusi na hatimae kupoteza nguvu zake na tandu ameashiria ubepari ukiongozwa na nchi kama vile Marekani.

Kwa muongozo wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, mtafiti amebaini kuwa masimulizi haya ya kihalisiajabu (kisa cha tandu na nyoka) yamefananana matukio ya kiulimwengu kushuhudia vita ngumu ya dunia iliyopelekea kuzusha vita vya pili vya dunia (1939 - 1945). Vita hivi vilipelekea Urusi kupoteza nguvu ya kuwa taifa linaloongoza kuwa na nguvu duniani na hatimae nafasi hiyo kukaliwa na Marekani.

4.6.2.3 Dhamira ya Wivu na Husda

Wivu na husda ni miongoni mwa tabia mbaya ambayo hupelekea watu kutoelewana. Tabia ya wivu na husda ni tabia inayokwamisha maendeleo ndani ya jamii na hata taifa kwa ujumla.Katika riwaya ya *Adili na Nduguze,*mwandishi amesimulia kisa cha uhalisiajabu kupitia kisakale kinachoonesha kuwa asili ya manyani walikuwa binadamu na ni ndugu zake Adili. Ndugu hao waligeuzwa manyani kwa laana ya jini

Huria, kutokana na kitendo cha kumtosa Adili baharini. Masimulizi haya ya kisasili cha kihalisiajabu yanaibua dhamira ya wivu na husda. Mwandishi ametusimulia hivi:

> "Kwa hasira kubwa Huria alinena, "kama mngalijua hatari ya kumtosa mtu baharini, au mngalikuwa na fikra za msiba, msingalijaribu kumtumbukiza ndugu yenu baharini alipolala. Wauaji ninyi hamstahiki kuishi," aliwashika shingoni pamoja na mkono wa kushoto akawabana kwa nguvu ya ajabu… Aliwalaani watoke katika umbo la uanadamu. Mara ile ndugu zake walikuwa manyani" (uk. 39-40).

Katika kisakale hiki mwandishi ameonesha namna wivu na husda unavyowaathiri wanajamii. Hii ni kwasababu ameona wivu na husda hauna mwisho mwema kwa mtuisipokuwa hatma yake ni majuto na kuangamia. Siku zote mwenye wivu huwa hajali wala haoni wema unaomtendea. Hutaka kila siku mwengine asifanikiwe. Matokeo yake hujiingiza katika shimo la maangamizi. Pamoja na msaada mkubwa aliouonesha Adili kwa ndugu zake lakini kwa sababu ya wivu na husda ndugu hao hawakuthamini juhudi zake isipokuwa walitaka mwanamke aliyekuwa amempenda Adili awe wao pamoja (uk. 32-33).

Mtafiti anaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, amegundua kuwa uchambuzi huu umekwenda sambamba na tabia mbaya ya wivu na husda iliyopo katika ulimwengu wa sasahivi kutawaliwa na wivu na husda na kushindwa kusaidiana kwa jambo lolote hali ambayo inarejesha nyuma maendeleo ya watu katika jamii. Wivu na husda ni jambo baya iwapo litaendelezwa hata amani itakosekana katika jamii yoyote ile.

4.6.2.4 Dhamira ya Ukoloni

Ukoloni ni hali ya nchi moja au taifa moja kuitawala nchi au taifa jengine. Iwapo nchi itatawaliwa na wakoloni nchi hiyo inaweza kufisidika na kuingia katika majanga kwasababu nchi hiyo inakuwa haina uhuru wa kufanya au kujiamulia chochote. Mtafiti kupitia kisasili cha Mji wa Mawe ameibua dhamira ya ukoloni. Inaelezwa kwamba mji huo ulipatwa na laana na watu wake kugeuzwa mawe kutokana na muhusika Mrefu kuwataka Mfalme na raia wake katika mji huo waachane na ibada ya mizimu. Hata hivyo, muhusikaTukufu hakusalimu amri ya Mrefu, kiumbe ambae alikuwa hasogeleki wala hashikiki, na alijitapa kuwa ana ujumbe kutoka kwa Mungu. Kutokana na kitendo hiki Mrefu akaulaani mji huo na kugeuka mawe. Kuhusu hili tumesimuliwa hivi:

> “Tukufu hakujali onyo hili akaamrisha kushikwa kwa mrefu aliyekuwa hasogeleki wala hashikiki. Uwezo usiohadhari ni kileo kibaya sana. Siku ile ilikuwa ya kitisho na msiba, ole na maangamizi makubwa. Kwa laana iliyotamkwa na Mrefu, miji mengine yote ya dola hii ilighariki, na kila kiumbe kilichokuwa na maisha katika Faghari kiligeuka jiwe…” (uk. 29).

Kupitia kipengele cha masimulizi ya uhalisiajabu ya Mji wa Mawe, mtafiti ameibua dhamira ya ukoloni, ambapo amesawiri dola zenye nguvu duniani na namna zinavyopanga masharti kwa nchi changa. Nchi changa zinatakiwa kutii masharti hayo bila mjadala wowote. Nchi yoyote ile inayopinga masharti ya kikoloni imeonekana kuwa ni adui mkubwa kwa mataifa tajiri na huangamizwa.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo inaongoza lengo mahsusi la pili na swali la pili la utafiti huu, mtafiti ameona kuwa nadharia hiyo imelandana na kile kinachoshuhudiwa ulimwenguni leo hii. Nchi tajiri kama vile Urusi

naMarekani zimekuwa zikitumia nguvu za mabavu kwa lengo la kutiiwa na nchi changa, na masharti ya nchi hizo yanatakiwa yatekelezwe vilivyo, vyenginevyo huingia katika nguvu za kijeshi ambapo nchi hizo hugeuka magofu ya kihistoria. Hii ndio tunayoishuhudia katika nchi changa kama vile Siria, Misri, Iraki na Afghanistani.

4.6.2.5 Dhamira ya Itikadi

Itikadi ni mifumo tofauti ya kiuchumi, kisiasa na hata kiutamaduni ambayo huweza kusababisha mikinzano na migogoro ndani ya jamii. Katika nyakati tofauti kumeweza kujitokeza mifumo mbalimbali ya kiuchumi kama vile mfumo wa ujamaa na mfumo wa kibepari ambapo ndani yake migogoro mbalimbali huweza kujitokeza.

Kupitia riwaya ya *Adili na Nduguze* mtafiti amegunduwa kuwa mwandishi ametumia wahusika wa uhalisiajabu ambao ni tandu na nyoka na kuibua dhamira ya itikadi. Mwandishi amesema:

> "Adili alipanda juu ya jabali huko aliona tandu likikimbia. Rangi yake inapendeza sana. Linang`ara kama kioo. Nyuma yake lilifukuzwa mbio na nyoka alietisha kabisa. Nyoka alipolifika aliliuma kichwani. Kisha alilibana jiweni. Tandu lilitoa mlio wa kusikitisha. Kwa mlio ule Adili alijua kuwa tandu lilikuwa hatarini. Mara ile ile moyo wake ulingiwa na huruma. Hakuweza kuvumilia. Aliokota jiwe lililokaribia uzito wa ratili moja akamtupia nyoka. Jiwe lilimpiga nyoka kichwani. Ilikuwa shabaha nzuri sana. Kichwa chote kilipondeka kwa pigo moja akafa mara ile. Ghafla tandu liligeuka mwanadamu, yaani msichana mzuri….baada ya hayo msichana alielekeza kidole chake cha shahada chini. Mara moja aridhi ilipasuka akaingia ndani yake. Alipokwishaingia ndani ardhi ilijifunga sawia… (uk. 17-18).

Katika riwaya hiyo ya *Adili na Nduguze,* wahusika hawa (tandu na nyoka) wamesawiriwa kiuhalisiajabu. Kupitia wahusika hawa mtafiti ameibua dhamira ya

Itikadi. Msanii ameonesha namna itikadi za mifumo hasa ya kiuchumi ulimwenguni ilivyoibua mikinzano na migogoro. Wadau wa mifumo hii ilitoa misaada kuwasaidia wale walioiunga mikono na kujenga uadui kwa wasiokubaliana nayo.

Kama ilivyoelezwa hapo kabla, muhusika tandu amewakilisha mfumo wa kibepari na muhusika nyoka ni ishara ya mfumo wa ujamaa. Adili amewakilisha nchi za Afrika. Hivyo kifo cha nyoka kimeonesha namna ujamaa ulivyomaliza nguvu yake baada ya mapambano makali. Pia, msaada alioupata Adili kutoka kwa jini Huria ni ishara ya misaada katika bara la Afrika kutoka kwa nchi za kibepari. Hata hivyo misaada hiyo ya jini Huria ni ishara ya misaada yenye masharti magumu kwa nchi za Afrika, Adili akiwa mfano wa muhanga wa masharti hayo magumu. Kidhati masharti hayo huwa si ya hiari na ndio yakamfikisha Adili upeo wa kuyaadhibu manyani ambayo ni ndugu zake wa damu bila kufurahia hilo. Kuhusu mifumo hii ya kiuchumi ulimwenguni Wafula (1999), anawataka Waafrika wawe makini kinyume chake wataendelea kuishi katika hali ngumu kutokana na ukandamizaji na unyonyaji unaofanywa na mataifa tajiri.

Kwa kuhusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti ameona kwamba kile kinachojadiliwa na mtunzi ndicho tunachokishuhudia hadi leo katika ulimwengu. Waitifaki wa mfumo wa ujamaa na wale wa mfumo wa ubepari hawatangamani pamoja. Mifumo hii kila mmoja umekuwa ukiuona mfumo mwengine kwamba umeleta uadui ulimwenguni. Vita kuu ya dunia ilisababishwa na mfumo huu wa tofauti za mitazamo ya kiuchumi iliyoongozwa na Urusi kwa upande wa ujamaa na Marekani kwa upande wa ubepari.

4.6.2.6 Dhamira ya Utabaka na Usaliti

Utabaka ni hali ya kuigawa jamii katika tabaka mbalimbali kama vile tabaka tawala na tabaka tawaliwa. BAKIZA (2010) wanaeleza, Usaliti ni tendo la mtu kuchukua siri za pande na kuzipeleka upade mwengine wa adui. Mtafiti amebaini kuwa riwaya ya *Adili na Nduguze* imetumia wahusika wa uhalisiajabu ili kuibua dhamira za mtunzi. Kama asemavyo Wamitila (2013), kwamba wahusika wanyama kwa kiwango kikubwa hutumika katika kazi zenye mielekeo ya uhalisiajabu ili kuibua dhamira za mtunzi. Katika utafiti huu dhamira ya Utabaka na Usaliti imejitokeza kwa wahusika mbalimbali ambao kwa udhati hawakuwa na mapenzi ya dhati kwa jamii zao. Miongoni mwa wahusika hao ni pamoja na Manyani. Hivyo, katika riwaya hii mtunzi ametumia wahusika hawa kama ifuatavyo:

4.6.2.6. 1 Manyani

Manyani ni wahusika wa uhalisiajabu. Imeelezwa kuwa manyani walikuwa binadamu na ni ndugu zake Adili. Hata hivyo waligeuzwa manyani kwa kuandamwa na laana ya jini Huria kutokana na kutaka kumtosa Adili baharini (Uk. 38- 39). Kupitia wahusika hawa msanii anaibua dhamira ya usaliti. Mwandishi ameeleza kuwa wahusika Mwivu na Husda ambao ni ndugu zake Adili walimsaliti Adili na hata kufikia kumtosa baharini kwa sababu ya kutaka mwanamke na choyo cha kutaka mali.

Sambamba na hayo, uhalisiajabu wa wahusika manyani kupanda farasi kila nyani akiwa na farasi wake mwenyewe umeashiria dhamira ya utabaka.Watu waliona ajabu kubwa kutokana na manyani kushirikiana na binadamu wakiwa wako katika msafara na wao wakiwa wamepanda farasi. Mtafiti amegundua kuwa msanii ameonesha,

hadi sasa jamii haijatangamana pamoja na kushirikiana kati ya wenye nacho na wanyonge. Tukio hili linasimuliwa na mwandishi:

> "…yeye alipanda farasi mmoja na mmoja kwa kila mnyama. Ikibali alipanda farasi wake yeye mwenyewe… Nyuma yao yaliandamana manyani juu ya farasi… alistaajabu. Farasi kupandwa na mnyama ulikuwa upeo wa miujiza…wakati umefika wa mawe kusema miti kujibu na wanyama kuwa watu…" (uk. 9).

Katika nukuu hii, msanii ameonesha namna wakoloni walivyowagawa watu kimatabaka. Tabaka la chini la Waafrika hawakuonekana watu na walionekana kama wanyama. Hii ni kasumba ya muda mrefu ya Wazungu dhidi ya Waafrika. Kama asemavyo Wafula (2007), kwamba Wazungu waliliona bara la Afrika kuwa ni bara jeusi lililojaa kila aina ya ushenzi, watu wake wasiojua ustaarabu na ni sawa na wanyama.

Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, mtafiti ameona kwamba, mawazo haya yapo hadi leo kwa baadhi ya Wazungu. Mathalani ni hivi karibuni tu Raisi wa Marekani Trump (2018) aliwatusi Waafrika na Waarabu na kudai kuwa ni sawa na wanyama. Kimsingi haya ni matusi ya kihistoria ambayo yanapaswa kupingwa na kila mtu wa bara hili la Afrika. Kwa mnasaba wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, mtafiti amebaini kuwa kile alichokizungumza msanii ndicho kinachoyakabili mataifa machanga leo hii. Mataifa haya Tanzania ikiwemo yamekuwa mhanga wa mataifa yenye nguvu.

Jadweli 05: Muhtasari wa Dhamira za Uhalisiajabu katika Adili na Nduguze

Nambari	**Dhamira za Uhalisiajabu katika riwaya ya Adili na Nduguze**
01	Dhamira ya Uongozi bora
02	Dhamira ya Uongozi Mbaya
03	Dhamira ya Wivu na Husda
04	Dhamira ya Ukoloni
05	Dhamira ya Itikadi
06	Dhamira ya Utabaka na Usaliti

Chanzo: Data kutoka riwaya ya *Adili na Nduguze*. Septemba 2018

Jadweli 06: Muhtasari wa jumla wa Dhamira za Uhalisiajabu katika riwaya za Kusadikika na Adili na Nduguze

Na	Dhamira za Uhalisiajabu	Kusadikika	Adili na Nduguze
01	Dhamira ya Ukandamizaji na Unyonyaji	√	×
02	Dhamira ya Maendeleo na Ukuaji wa Huduma bora za Kijamii	√	×
03	Dhamira ya Tamaa na Uchoyo	√	×
05	Dhamira ya Umuhimu wa Elimu ya Uanasheria	√	×
06	Dhamira ya Ukombozi	√	×
07	Dhamira ya Ubadhirifu wa Mali ya Umma	√	×
	Dhamira ya Uongozi Mbaya	√	√
08	Dhamira ya Uongozi bora	×	√
10	Dhamira ya Wivu na Husda	×	√
11	Dhamira ya Ukoloni	×	√
12	Dhamira ya Itikadi	×	√
13	Dhamira ya Utabaka na Usaliti	×	√

Chanzo: Data kutoka riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Septemba, 2018

4.7 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amewasilisha na kufanya uchambuzi wa kina wa data za utafiti alizozikusanya. Sura hii imefafanua kwa undani usuli wa Shaaban Robert, muhtasari wa riwaya ya *Kusadikika* na muhtasari wa riwaya ya *Adili na Nduguze*. Vilevile sura hii imechambua kwa kinavipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya ya*Kusadikika*na baadae riwaya ya *Adili na Nduguze*kwa kurejelea nadharia ya Uhalisiajabu. Pia, sura imewasilisha na kuchambuadhamira za uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na

*Adili na Nduguze*kwa kuongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.Mwisho ni hitimisho la sura. Kwa kufanya hivyo mtafiti ameamini kwamba ameweza kufanikisha vyema malengo na maswali ya utafiti huu ipasavyo. Hivyo sehemu inayofuata ni sura ya tano ambayo imewasilisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii ni sura ya mwisho ambayo imehusu vipengele vya msingi: Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo ya utafiti huu. Hivyo basi katika sura hii ufafanuzi wa vipengele hivyo umezingatiwa vyema kwa lengo la kuipa uhai sura na kuifanya iwe na umuhimu mkubwa katika utafiti huu. Ufafanuzi wa vipengele vilivyomo katika sura hii ni kama ifuatavyo:

5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulihusu mada ya utafiti isemayo: *Kuchunguza Uhalisiajabu na Dhamira katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze.* Utafiti huu umejengwa kwa sura tano zifuatazo: Sura ya Kwanza ni Utangulizi wa jumla. Sura ya pili ni Mapitio ya Kazi Tangulizi na mkabala wa Kinadharia. Sura ya tatu ni Mbinu za Utafiti. Sura ya nne ni Uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti. Sura ya tano ni Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo. Kwa muhtasari ufafanuzi wa sura hizo ni kama ifuatavyo:

Sura ya kwanza ilihusu Utangulizi wa jumla. Vipengele vya kiutangulizi vilivyojadiliwa katika sura hii niusuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, muundo wa tasnifu na Hitimisho.Utafiti huu uliongozwa na lengo kuu na malengo mahsusi. Lengo kuu lilikuwa ni: *Kuchunguza Uhalisiajabu na Dhamira katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze*. Malengo Mahsusi yalikuwa mawili ambayo ni *mosi; Kubainisha vipengele vya Uhalisiajabu katika riwaya za Kusadikika na Adili na Nduguze. Pili; Kubainisha*

Dhamira za uhalisiajabu katika riwaya za Kusadikika na Adili na Nduguze. Hivyo basi, kutokana na malengo mahususi haya, utafiti huu uliongozwa na maswali mawili ya utafiti ambayo ni *(i) Ni vipengele vipi vya uhalisiajabu vilivyobainishwa katika riwaya za Kusadikika na Adili na Nduguze? (ii) Ni dhamira zipi zauhalisiajabu zilizobainishwa katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze?*

Sura ya pili ilihusu Mapitio ya Kazi Tangulizi na Mkabala wa Kinadharia. Sura hii ilijumuisha vipengele vifuatazo: Utangulizi, Dhana ya uhalisiajabu katika fasihi, maandiko kuhusu riwaya zinazotafitiwa na pengo la utafiti huu. Pia, katika sura hii uchambuzi wa nadharia ya Uhalisiajabu na Mwitiko wa Msomaji ambazo zimeongoza utafiti huu umefanyika. Mwisho sura imemalizia kwa kutoa hitimisho.

Sura ya tatu imehusu Mbinu za utafiti. Sura hii imechambua kwa kina vipengele muhimu vifuatavyo: Utangulizi, Eneo la utafiti, Sampuli na usampulishaji, Mbinu za ukusanyaji wa data, Mbinu za uchambuzi wa data. Mwisho ni hitimisho.

Sura ya nne ilihusu Uwasilishaji, Uchambuzi na mjadala wadata za utafiti. Vipengele vilivyojadiliwa katika sura hii: Utangulizi, Usuli wa mwandishi – Shaaban Robert, muhtasari wa riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*, uwasilishaji na uchambuzi wa data ambapo data zimefanyiwa uchambuzi na kuwasilishwa kutegemea malengo mahususi na maswali ya utafiti. Kwanza mtafiti amefanya uchambuzi wa vipengele vya uhalisiajabu kama vilivyobainishwa katika riwaya *ya Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Kufanya hivi kumemuwezesha mtafiti kukamilisha lengo mahsusi la kwanza sambamba na kujibu swali la kwanza la utafiti huu akiongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu.Baada ya hapo, mtafiti amechambua dhamira za Uhalisiajabu kama

zilivyobainishwa katika riwaya ya *Kusadikika*na *Adili na Nduguze* akihusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Uchambuzi huo umeongozwa na lengo mahsusi la pili lisemalo: Kubainishadhamira za uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Lengo hilo la pili limewiana na swali la pili la utafiti lisemalo: Ni dhamira zipi za uhalisiajabu zilizobainishwa katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.* Mwisho sura imemalizia kwa hitimisho.

Sura ya Tano ni Muhtasari wa Utafiti, Hitimisho na Mapendekezo. Sura hii imeeleza kile kilichogundulika katika utafiti huu kutegemea mada ya utafiti. Pia, sura hii imetoa muhtasari wa hatua kadhaa zilizotumika hadi kufanikisha utafiti huu. Kwa ujumla utafiti huu umegundua kwamba Shaaban Robert ametumia vipengele na dhamira za uhalisiajabu katika kusanii riwaya za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*.

5.2.1 Lengo Mahsusi La Kwanza

Lengo mahsusi la kwanza la Utafiti huu lilikuwa ni: Kubainishavipengelevya uhalisiajabukatika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze. Lengo hili liliongozwa na swali la msingi la kwanza lisemalo: Ni vipengele vipi vya uhalisiajabu vilivyobainishwa katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze?*

Kwa muongozo wa nadharia ya Uhlisiajabu, matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa Riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze* imetumia vipengele vya uhalisiajabu ambavyo ni; utatizaji wa wakati, mtindo wa udenguzi na uumbuzi, mtindo wa kihalisiajabu, masimulizi ya kihalisiajabu, usawiri wa wahusika wa kihalisiajabu, utambulisho na mwanda wa kihusika, motifu za safari za kihalisiajabu na mandhari za kihalisiajabu.

5.2.2 Lengo Mahsusi la Pili

Lengo mahsusi la pili la utafiti huu lilikuwa ni: Kubainisha dhamira za uhalisiajabu katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze.* Lengo hili liliongozwa na swali la pili la utafiti lisemalo: Ni dhamira zipi za uhalisiajabu zilizobainishwa katika riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze?*

Kwa kuhusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa riwaya ya *Kusadikika na Adilina Nduguze* zimebainisha dhamira mbalimbali za uhalisijabu. Kwa mfano katika riwaya ya *Kusadikika* dhamira zilizobainishwa ni pamoja na: Dhamira ya ukandamizaji na unyonyaji, dhamira ya maendeleo na ukuaji wa huduma bora za kijamii, dhamira ya tamaa na uchoyo, dhamira ya umuhimu wa elimu ya uanasheria, dhamira ya ukombozi, dhamira ya ubadhirifu wa mali ya umma na dhamira ya uongozi mbaya. Kwa upande wa riwaya ya *Adili na Nduguze,* dhamira zilizobainishwa ni hizi zifuatazo: Dhamira ya uongozi bora, dhamira ya uongozi mbaya, dhamira ya wivu na husda, dhamira ya ukoloni, dhamira ya itikadi, dhamira ya utabaka na usaliti.

5.3 Hitimisho

Kwa kuhitimishia, mtafiti amebaini kwamba riwaya ya *Kusadikika* na *Adili na Nduguze* ni riwaya za Kiswahili ambazo zimetumia vipengele kadhaa vya uhalisiajabu. Kimsingi riwaya hizi zimefumwa katika matukio ya kihalisiajabu ambayo yamechota dhamira muhimu kwa jamii. Mtafiti kwa kutumia vipengele hivyo vya uhalisiajabu na dhamira amejidhihirisha kuwa Shaaban Robert ni mwandishi nguli na aliweza kufikisha ujumbe kwa jamii iliyomzunguka ambayo kwa wakati ule ilikuwa imetawaliwa na wakoloni ambao walikuwa wakiwaonea na

kuwanyanyasa Waafrika. Kwa udhati ni kwamba riwaya teule za *Kusadikika* na *Adili naNduguze*zimejaa uhalisiajabu jambo ambalo ukiondoa uhalisiajabu kazi hizo hubakia kuwa chapwa kisanii.

5.4 Mapendekezo

Utafiti huu umehusu: *Kuchunguza Uhalisiajabu na Dhamira katika riwaya ya Kusadikika na Adili na Nduguze*. Ni imani ya mtafiti kwamba amefikia malengo yaliyoyakusudiwa. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa hakuna mwisho wa utafiti. Kadri tafiti zinavyofanyika ndio kuzuka kwa haja ya tafiti nyengine zaidi. Kwa sababu hiyo mtafiti amependekeza maeneo yafuatayo kuendelea kufanyiwa utafiti:

5.4.1 Mapendekezo ya Kitaaluma

Wanataaluma kama vile wahadhiri, walimu, watunga mitaala, wasomi wengineo na wanafunzi hasa wa somo la Fasihi wana nafasi kubwa ya kukuza taaluma zao kwa kuzingatia maeneo muhimu ambayo bado hayajatafitiwa kwa mujibu wa utafiti huu. Kwa mfano, tafiti nyengine zinaweza kufanyika katika uwanja wa fani na maudhui, utafiti linganishi katika kazi za mtunzi teule yaani Shaaban Robert, na watunzi wengine, kuchunguza miktadha na hali za kisiasa za wakati wa maandishi ya Shaaban Robert nakadhalika.

5.4.2 Mapendekezo kwa Serikali

Kwa upande wa serikali ina wajibu wa kuhamasisha umuhimu wa kufanya tafiti za kitaaluma ikiwemo eneo maalumu la Fasihi ili kuweza kuimarisha taaluma hiyo katika maendeleo ya elimu nchini Tanzania na kwengineko duniani. Juhudi hizo za makusudi zitasaidia kuamsha ari ya wanajamii kujifunza na kuweza kuisaidia serikali

katika maendeleo ya taifa kwa kuongeza idadi ya wasomi (wataalamu) waliobobea katika fani husika. Pia, serikali ione umuhimu wa kuyafanyia kazi matokeo ya tafiti mbali mbali badala ya kubakia maktabani kama kumbukumbu ambazo wakati mwengine humalizia kutafunwa na panya au wadudu wengineo au kuharibika kwa namna nyengineyo.

MAREJELEO

Ambrose, B. M. (2014). Kuchunguza Dhamira za Kisiasa katika Riwaya za Shaaban

Robert: Mfano wa Kusadikika na Kufikirika. Tasinifu ya shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Chuachua. R. na wenzake (2009). *Shaaban Robert*: *Visasili na Ukoloni, Katika Mulika*. Dar-es-salaam: TUKI.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*. Dar es Salaam: TATAKI.

Cooper, B. (1988). *Magical Realism in West African Fiction.* New York: Routledge.

Cresswell, J. W. (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Danow, K.D. (1995). *The Spirit of the Carnival; Magical Realism and the Grostesque*. Kentucky University of Kentucky Press.

D' Haen, Theo L. (2005). *Magic Realism and Post modernism.* Decentering Priviledged Centers.

Enon, J. C. (1998). *Education Research Statistics and Measurement*. Kampala: Makerere University.

Faki, A. M. (2015). Sifa za Utendi wa Kiswahili: Mfano Utendi wa Fumo Liyongo. Tasnifu ya M.A Kiswahili Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania.

Furlong, N. (2000). *Research Methods and Statistics*: *An Intregrated Approach*. New York: Hartcourt Colledge Publishers.

Garnier, X. (2012). Talking About Oneself to Act in the World: A Swahili Autobiography Shaaban Robert, Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini ("My Life and After Fifty Years"). Katika Jarida la Swahili Forum Na. 19, ku. 106-116.

Herman, D. na wenzake. (2005). *Routledge Encyclopedia of Narrative Theory*. Abingdon: Routledge

Kezilahabi, E. (1976*).* Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya.Tasinifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: Introduction*. Kenya: Paulines Publication Africa.

Kothari, C. R. (1990). *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kyando, L. (2013). *Majina Sadifa ya Wahusika katika Kusadikika na Kichwamaji,* katika

Mulika namba, 31, TATAKI, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, kur. 37-50.

Madumulla, J. S. (2011). *Riwaya ya Kiswahili Nadharia, Historia na Misingi ya Uchunguzi*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Mjema, R. (1990). "*Kusadikika*," katika *Mulika* namba 22, Daer es Salaam: TUKI, Kur. 26-31.

Mulokozi M.M (1996). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: Dar-es Salaam Tanzania.

Nyamunda, V. A. (2005). Uhakiki wa Bina-Adamu na Musa Leo. Tasnifu ya M.A Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ponera, A. S. (2010). *Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana Yake, Sababu za Kutumiwa, na Athari Zake kwa Wasomaji*. Shahada ya Uzamili ya Sayansi Jamii katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma,

Robert, S. (1966). *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Dar es Salam: Mkuki na Nyota Publishers.

Robert, S. (1971). *Kusadikika* (Toleo la tano). Dar es Salam: Printpak Tanzania Ltd

Robert, S. (1980). Adili na Nduguze. (Chapa ya kumi na nne). Dar es Salam: Dar es Salam Publishing House.

Salim, M. A. (2015). Kuchunguza Ufasihi Simulizi Unaojitokeza Ndani ya Hadithi za *Kusadikika na Adili na Nduguze*. Tasnifu ya shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Shaaban, R. (1991). *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers

Shaaban, R. (1991). *Kusadikika*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Shaaban, R. (1980). *Adili Na Nduguze (chapa ya 10).* Dar es Salaam: Publishing House.

Shaaban, R.(1959). Kufikirika.

Shaaban, R.(1949). *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Khamsini*.

Shaaban, R.(1969). *Mwafrika Aimba*

Sengo T.S.Y na Kiango S.D. (1977). *Hisi Zetu.* Dar-es salaam: TUKI.

Sengo, T. S. Y. (1975). *Shaaban Robert*: *Uhakiki na Maandishi Yake*. Nairobi: Foundation Books

Senkoro, F. E.M.K (1976). *Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili*. Dar-es-salaam: TUKI

Senkoro, F. E.M.K(1982). *Fasihi*. Dar-es-salaam: Press Publicity Centre

Taib, A. H. (2008). *Mkabala wa Kiislamu katika Uchanganuzi na Uhakiki wa Fasihi ya Kiswahili.* Dar-es-salaam: CHAKAMA.

Waliaula, K. (2010). *Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe*: *Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum.* Swahili Forum 17(2010): 143-157.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phonex Publisher Limited

Wamitila, K. W. (2013). *Mikakati ya Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili.* Katika Mulika Na. 32, 1-12

Wafula, R. M. (1999). Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake.Nairobi: Phonex Publishers Limited.

Wanjiru (2013). Uhalisiajabu katika Tamthiliya ya Ngoma ya Ng`wanamalundi. Tasnifu ya M.A Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Zamora P.L. & Faris B.W. (1995). *Margical Realism*: *Theory, History and Community*. London:Duke University Press.